Pili, kipengele kingine kinachowafananisha ni matumizi ya taswira. Data za utafiti zinaonesha kuwa waandishi teule wamekuwa wakitumia taswira za kuonekana katika kuzijenga kazi zao. Katika riwaya ya *Nyota ya* Rehema, ipo taswira inayosema "Upesi Rehema alirusha mikono yake kujikinga; na kutanabahi kwa mara ya mwanzo kuwa mwili wake ulikuwa wazi. Alikuwa uchi! Alipaparika kutafuta cha kumsitiri na kutaka kuzuka pale alipolazwa, lakini papo hapo mkono mmoja wa yule mtu na huku mwingine ukifanya kazi katika kifua chake kiwazi… Alipofunua tena macho yake alikuwa peke yake. Aliangazaangaza asione kitu ispokuwa mshikamano wa makuti uliomzunguka…" (uk. 27). Matumizi haya, pia yapo katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* kama anavyoeleza msanii *"Shati lake lililokuwa limepasuka lilikuwa likipepea hewani"* (uk. 3).

Pia, waandishi teule wanafanana katika mtindo wa takriri neno wenye kushadadia ujumbe walioukusudia. Katika riwaya ya *Nyota ya Rehema,* data za utafiti zinaonesha kuwepo kwa takriri inayosema *"...Pengine atakutana na mtu mwingine mwenye huruma kama Sulubu…Pengine ataweza kufika mjini …Pengine atamwona yule Mwatima…Pengine atamsaidia… Na katika mkururo huu wa 'Pengine – pengine' usingizi ulimwiba na kumchukua katika pumbazo zake"* (uk. 38)". Kwa upande wa riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo,* matumizi haya yanajitokeza kama vile *"Walisikia watu wakipiga kelele! Piga!, Piga!, Piga!, Ua!, Piga mbwa*!" (uk. 50).

Kipengele kingine kinachowafananisha waandishi hao ni matumizi ya nidaa. Data zinaonesha kuwa waandishi teule wametumia mtindo wa nidaa kwa kuteua maneno yanayoonesha utabaka. Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* data zinaonesha kuwa mbinu hii imejitokeza kama ifuatavyo: *"Mm! Sema sasa! Mm! Sema sasa! Una usemi gani? Niite bwana ili nikuache!...* (uk. 26). Matumizi kama haya, pia yanajitokeza katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* ambapo data

zinaonesha namna Suleiman alivyotumia mbinu hii anapoeleza hivi: *"Poeni wananchi! Poeni wananchi! Dhuluma imeshapinduliwa!* (uk. 168). Kimsingi, matumizi haya ya nidaa yanaambatana na takriri ili kutilia msisitizo wa yale yanayojadiliwa.

Pia, data zinaonesha kwamba Kezilahabi na Suleiman wanafanana katika matumizi ya mtindo wa kariha. Mtindo unatumia maneno yenye matusi. Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* yapo matumizi ya kariha kama yanavyobainishwa, *"Tumaini alianza kupapasa shanga za kiuno"* (uk. 24). Pia, katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*, data za utafiti zinaonesha matumizi ya mtindo wa kariha kama mwandishi anaeleza kuwa Rehema *"Alikuwa uchi"* (uk. 27). Kifungu hiki cha maneno pia kinajenga taswira ya kariha. Matumizi ya kariha ni zao la waandishi wenye mwelekeo wa kuandika kazi zao kwa mkabala wa Usasaleo na Usasabaadaye kama anavyoeleza Mbarouk (2017) kwamba Usasaleo na usasabaadaye hulenga kueleza mambo wazi wazi bila kujali maadili na miiko ya jamii inayohusika.

Waandishi wanamuathiriano na muingiliano wa mitindo ya matumizi ya lugha jambo linalowafanya kuonekana kama watu wanaoandika jambo la aina moja kwa namna tofauti. Kama ilivyokwishaelezwa hapo kabla kwamba matumizi hayo yanatokana na mwingilianomatini wa kimtindo unatokana na sababu za kihistoria, kiuchumi, kiutamaduni, kimazingira na kielimu. Huu ndio msingi wa Kristiva (1990) katika mkabala wa Mwingiliano matini kueleza kwamba hakuna matini yoyote inayojitegemea na kujitosheleza bali kuna muathiriano wa mtunzi mmoja na mwingine.

Mbinu Nyingine za Kimtindo
Suleiman na Kezilahabi wametumia mbinu nyingine za kimtindo zenye kuwafananisha. Vipengele hivyo vinahusu matumizi ya barua, hotuba, masimulizi, nyimbo, dayolojia, ndoto, matumizi ya majina sadfa pamoja na motifu za kisafari. Katika kipengele cha barua, data zinaonesha kuwa waandishi wote wanatumia barua kama mtindo wa kusana kazi zao. Suleiman anatumia barua ili kujadili suala la mapenzi (uk. 58). Hata hivyo, Suleiman ametumia mtindo huo kwa kiwango

kidogo tukilinganisha na Kezilahabi ambaye anatumia barua kwa mawanda mapana zaidi. Katika riwaya zote teule za Kezilahabi mtindo huu unatumika kujadili suala la mapenzi na uhusiano katika jamii.

Mtindo wa barua unaofanywa na waandishi teule unadhihirisha ukiushi wa uandishi wa jadi wa riwaya ambao unalenga kukiuka misingi ya jadi na kuingiza katika mtindo wa usasabaadaye kama anavyoeleza Mbarouk (2017) kwamba kazi za usasabaadaye hujitokeza vipande vipande yaani, mwingilianomatini ikiwa na maana ya uchanganyaji wa elementi nyingi kama inavyowasilishwa na fujo nyingi au maelezo mengi yaliyojaa katika jamii za Usasabaadaye. Anaendelea kueleza kwamba inawezekana kuwa mchanganyiko wa tanzu nyingi ndio unaounda usimulizi wa kipekee. Pia, kuna matumizi ya hotuba iliyitumika kujadili masuala ya kijamii, likiwemo suala la kisiasa (uk.115). Matumizi haya yanajitokeza pia katika riwaya ya *Kiu*, ambapo hotuba imetumika kuonesha ushirikiano katika masuala ya kijamii. Mtindo wa hotuba unatumika kujadili uhusiano wa kijamii katika maisha yao ya kila siku.

Masimulizi ni mtindo wa wahusika kupewa nafasi ya kusimulia visa na matukio. Watunzi wanabaki kama shuhuda wa visa na matukio yanayosimuliwa. Matumizi ya kuwapa wahusika nafasi ya kusimulia matendo ni mtindo wa waandishi nguli katika kuandika riwaya. Mtindo huu huwa unakiukwa na waandishi chipukizi ambapo huchukua nafasi ya wao kusimulia. Madumulla (2009) anaeleza kuwa waandishi chipukizi hujikuta wakisimulia matendo ya wahusika kama kwamba wao ni shuhuda wa visa na matukio hayo. Jambo hili linafifisha uandishi wa utanzu wa riwaya.Mfanano mwingine upo katika matumizi ya nyimbo kama sehemu ya mtindo wa watunzi. Data zinadhihirisha kuwa watunzi teule wanatumia mbinu ya nyimbo katika kazi zao kupeleka ujumbe unaohusu mapenzi. Matumizi ya nyimbo yanajitokeza katika riwaya ya *Kiu* (uk. 47), ambayo inasawiri malezi na mapenzi. Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (uk. 10), data zinaonesha kuwa kuna nyimbo zinajadili suala la mapenzi. Mifano hii inaonesha kuwa watunzi teule wanapojadili suala la mapenzi wanatumia nyimbo ili kushadidia suala hilo.

Mtindo wa matumizi ya dayalojia pia unatumiwa na waandishi katika kazi zao zote teule. Matumizi ya dayalojia inatumika kuwajengea uwezo wahusika wa kazi zao kufanya mijadala ndani ya riwaya kama ilivyo katika tanzu za fasihi. Mtindo huu ni kama sehemu ya ukiushi wa kimuundo na mtindo. Wamitila (2002) anaeleza kwamba kazi za urasimi mpya kama riwaya hukiusha muundo wa kijadi wa masimulizi na badala yake kuchanganya vitanzu vingine visivyofungamana na kaida maalumu za utunzi zilizokuwa zikisisitizwa wakati wa urasimi mkongwe. Hata hivyo, mtindo huu huijenga kazi ya fasihi kwa upekee unaosaidia kuusuka ujumbe uliokusudiwa kwa mafanikio makubwa kisanaa.

Makala hii imebaini kuwepo kwa majina sadfa kama sehemu mojawapo ya mtindo wa waandishi teule. Waandishi teule wametumia mtindo wa kuwapa majina wahusika wao yanayosadifu matendo, tabia na sifa ili kusawiri ujumbe maalumu. Mathalani, jina la "Sulubu" katika *Nyota ya Rehema* limetokana na kufanya kazi zenye kutumia nguvu. "Cheusi" katika riwaya ya *Kiu,* jina lake linatokana na sifa ya mikosi na misukosuko iliyokuwa inamkumba katika maisha yake. Tegemea katika *Dunia Uwanja wa Fujo*, jina lake linasadifiwa kutokana na tabia yake ya kuweka matumaini ya kupata mahitaji kutoka kwa mtu mwingine. Mtindo huu wa kuwapa majina wahusika unaofanywa katika riwaya teule unadhihirisha ubunifu wa hali juu wa watunzi kama anavyoeleza Kabije (1995) kwamba majina ya wahusika yanaweza kuwa na upekee katika muunganiko wake na matendo, mazungumzo, muonekano wa nje, tabia na mazingira yanayomzunguka mhusika.

Pia, kuna matumizi ya motifu ya safari ya msako katika kazi za waandishi teule. Waandishi wote wanatumia mbinu ya motifu ya safari na msako kama mtindo unaotumika kusukuma mbele visa na matukio yanayojenga maudhui ya kazi zao. Suleiman anatumia mtindo wa motifu wa safari za msako wa uhuru katika jamii za Visiwani Zanzibar zinazofanywa na wahusika wake dhidi ya dhuluma na uonevu. Matumizi kama haya yamefanywa na Euphrase Kezilahabi katika riwaya ya *Dunia Uwaja wa Fujo,* ambapo "Mulele" anaondoka

nyumbani kwake kwenda kumsaka "Tumaini" (uk. 52). Ntarangwi (2004) anaeleza kwamba motifu za safari na msako zina maana halisi inayodhihirisha ukweli wa matukio ya jamii yanayotokea kila siku, hasa pale wahusika wanapokuwa safarini. Huu ndio msingi wa nadharia ya Mwingilianomatini kueleza kwamba ujenzi wa kazi za fasihi sio urejelezi wa kazi fulani katika kazi nyingine tu, bali ni mwingiliano wa mitindo ya kiuashiriaji.

Hivyo, kufanana kwa matumizi ya vipengele vya mtindo katika riwaya teule kumechagizwa na ukweli kwamba riwaya teule zimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili na zimeandikwa kwa kuzingatia muktadha wa jamii za Tanzania. Mawazo haya yanaelezwa na Saleem (2013) kwamba matukio ya kihistoria, desturi, utamaduni na sababu za kijiografia zinaweza kusababisha watunzi wa kazi za fasihi kufanana katika mielekeo ya kazi zao za fasihi. Matokeo yanaonesha kuwa wanatumia mbinu hizi kwa viwango vinavyofanana licha ya kuwepo kwa tofauti ndogo ndogo ambazo zinatokana na sababu kadhaa.

Kutofautiana kwa Mtindo kwa Waandishi Teule
Katika sehemu hii, makala hii imechunguza kipengele cha matumizi ya mbinu za kimtindo yanavyowatofautisha watunzi wa riwaya teule. Makala hii imebaini kuwa, riwaya hizi zinatofautiana katika viwango mbalimbali vya kimtindo. Tofauti hizi zinajitokeza kutokana na waandishi hao kutotumia kabisa baadhi ya mitindo kwa kiwango kikubwa kuliko msanii mwingine kama mbinu ya kufikisha ujumbe. Mara nyingine, watunzi wametofautiana kutokana na uteuzi maalumu wa maneno na hata miundo ya tungo zao. Jilala (2016) anaeleza kwamba Fasihi Linganishi hutumika kulinganisha kazi mbalimbali kwa kutumia vigezo mbalimbali. Msingi huu ulitupa fursa ya kuchunguza tofauti ya watunzi teule.

Kutofautiana Kimtindo Baina ya Watunzi Teule
Kila mwandishi wa kazi ya sanaa hutofautiana na mwandishi mwingine katika ujenzi wa vipengele vya maudhui na fani. Mtindo ndio humfanya mtunzi kuwa na upekee katika kuwasilisha masuala mbalimbali ya kijamii na namna anavyoyawasilisha. Kutokana na

ukweli huo, waandishi wa riwaya teule wametofautiana katika vipengele kadhaa. Mathalani, riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* imetumia mtindo wa hotuba, mashairi, hadithi na magazeti. Kwa upande wa riwaya ya *Kichwamaji*, mtunzi ametumia mtindo wa matangazo, masimulizi, hadithi, magazeti, ndoto na uhalisiajabu. Kimsingi, mitindo hii haikutumiwa na Suleiman katika riwaya zake teule zilizochunguzwa.

Makala hii inaonesha kuwa waandishi hawa wametofautiana katika kipengele cha mtindo wa upenyezi, licha ya kuwa waandishi wote wanaibua itikadi katika mielekeo tofauti. Kezilahabi ametumia mtindo wa upenyezi kuhusu falsafa ya maisha ambapo anahusisha mjadala unaodokeza hali ya kuwepo au kutokuwapo kwa mamlaka na nafasi ya Mwenyezi Mungu, hasa unapochunguza uhusiano wake na jamii ya mwanadamu hapa duniani. Katika mjadala huo, anafikia hitimisho kuona kuwa hakuna Mungu. Kwa upande wa Suleiman, anaitumia mbinu hii ili kuonesha kuwepo kwa nafasi na mamlaka kamili ya Mwenyezi Mungu, na kwamba ndiye anayevisaidia viumbe, akiwemo binadamu.

Tofauti nyingine imejidhihirisha katika kipengele cha matumizi ya majina sadfa. Waandishi wote wamejenga wahusika wao kwa kutumia majina sadfa. Pamoja na matumizi ya majina sadfa katika kazi zote, tofauti inayojitokeza ni namna wasanii hao wanavyotumia majina hayo katika ujenzi wa dhamira za kazi zao. Uteuzi wa majina ni moja ya tofauti ambayo imetumika katika kujenga uzito wa dhamira ya riwaya hizo. Suleiman anatumia majina sadfa ya Uswahilini, tofauti na Kezilahabi. Muhamed katika riwaya ya *Kiu,* ametumia jina la "Mwinyi" ili kuonesha Umwinyi unaofanywa na mabepari. Kwa upande wa Kezilahabi, anawapa wahusika wake majina yanayoegemezwa katika falsafa ya maisha. Kwa mfano, ametumia jina la "Kazimoto" ili kusawiri hali ya kufanya kazi kwa bidii. Huu ndio msingi wa hoja ya Wafula (2007) kwamba nadharia ya udhanaishi imejengwa katika misingi inayomtaka mtu afanye inavyowezekana ili kushinda vikwazo vyovyote vya maisha. Kutokana na hali hii, "Kazimoto" anafanya bidii ili kushinda hali ngumu ya maisha.

Pia, waandishi teule wanatofautiana namna ambavyo watunzi walivyotumia mtindo wa mashairi katika kuunda kazi zao. Katika *riwaya ya Kichwamaji,* msanii ametumia mbinu ya shairi lenye kufuata mtindo wa kisasa unaolegeza matumizi ya vina na mizani. Kwa upande wa riwaya ya *Kiu* na *Nyota ya Rehema*, hakuna matumizi ya mashairi. Hali hii inawafanya watunzi wa riwaya teule watofautiane katika matumizi ya kipengele hiki. Pia, waandishi teule wanatofautiana katika kutumia mtindo wa matumizi ya uhalisiajabu. Kezilahabi anatumia uhalisiajabu katika riwaya ya *Kichwamaji*. Kalia anayesimulia namna anavyokwenda mbinguni na namna Mungu alivyokuwa akiwaruhusu siku nyingine kuja ardhini (uk. 74). Kwa upande wa Suleiman, hakutumia kabisa mbinu ya uhalisiajabu katika kazi zake zote teule. Vipengele vyingine vinawatofautisha Kezilahabi na Suleiman ni matumizi ya matangazo, magazeti na majibizano ndani ya riwaya. Vipengele hivi vimekuwa vikitumiwa na Kezilahabi, lakini Suleiman hakutumia mbinu hizi katika riwaya zake teule zilizochunguzwa. Aidha, Kezilahabi amekuwa akitumia sajili nyingi zaidi akilinganishwa na Suleiman. Waandishi hawa wanaonekana kutofautiana katika matumizi ya vipengele vingine vya mitindo ya matumizi ya lugha.

Mtindo wa Matumizi ya Lugha
Suleiman amekuwa akitumia vipengele vingine vya lugha kama vile lahaja, kinira, tabdila, oksimora, udondoshaji, mazida na haipofora ambavyo havijitokezi katika riwaya teule za Kezilahabi. Hii inaonesha kwamba Suleiman amekuwa na umilisi mkubwa katika kutumia lugha ya Kiswahili. Hii inatokana na kwamba Kiswahili ni lugha yake ya kwanza tofauti na Kezilahabi (Mkerewe) ambaye Kiswahili ni lugha yake ya pili. Aidha, tofauti nyingine zilizojitokeza katika matumizi ya tamathali za usemi ambapo wasanii wanatofautiana katika vipengele viwili ambapo Suleiman anatumia sana chuku na Kezilahabi akitumia zaidi tafsida.

Hitimisho
Kwa ujumla, makala hii imechunguza namna mitindo inavyofanana na kutofautiana katika riwaya teule. Data zilizochunguzwa zinaonesha kuwa, waandishi teule wanafanana na kutofautiana katika vipengele

mbalimbali kutokana na kuwepo kwa tofauti zao za kihistoria, kielimu, kifalsafa, kijiografia na wakati wa uandishi wa kazi zao. Kezilahabi ni tajiri katika mitindo ya sajili akilinganishwa na Suleiman. Kwa upande mwingine, Suleiman anaonekana kuwa na umilisi zaidi katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, mitindo ya kazi zao ina muachano mkumbwa katika historia ya kukua na kukomaa kwa maendeleo ya fasihi ya Kiswahili.

Marejeleo

Ali, A. R. (2015). Kuchunguza Dhana Zilizobebwa na Wahusika na Zinavyolandana na MajinaYao katika Riwaya ya Kiu ya Haki. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Bakhtin, M. (1981). *The Dialogic Imagination.* Four Essay, Austin: University of Texas.

Balisidya, M. L. (1982). *The Image of the Woman in Tanzania Oral Literature.* TUKI, Toleo Na. 49/2.uk. 1- 3.

Bosibori, B. T. (2016). Mwingilianomatini Kati ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Mstahiki Meya. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

De Saussure, F. (1917). *A Course in General Linguistics.* Lasalle: Open Court.

Enkvist, N. E. (1973). *Linguistics Stylistics*. The Hague: Mouton.

Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi: Nadharia, Mbinu na Matumizi*. Dar esSalam: Daud Publishing Company.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichwamaji.* Dar es Salam: East Africa Publishing House.

Kezilahabi, E. (1975). *Dunia Uwanja wa Fujo*. Dar es salaam: East Africa Publishing House.

Kimambo, S. (2015). *Kuchunguza Matumizi ya Lugha katika Riwaya ya Kiswahili*: Uchunguzi Kifani Riwaya ya *Vipuli vya Figona Siri za Maisha*. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kristeva, J. (1980). *Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art*. New York: Columbia Universiyy Press.

Ligembe, N. E. G. (1995). *The Use of Metaphor in Penina Muhando`s Linaubani. AStylistics Analysis.* A Research for Master Degree (Unpublished). University of Dar es Salaam.

Kabije, F. M. (2013). *Dhima za Ufutuhi katika Riwaya za Shaaban Robart*. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salam.

Kyando, L. (2013). *Majina Sadfa ya Wahusika katika Kusadikika na Kichwamaji*. Katika *Mulika* namba, 31, TATAKI: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kur. 37 - 50.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia Historia na Misingi yaUchambuzi.* Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Mbarouk, S. S. (2017). *Usasabaadaye Katika Riwaya ya Walenisi.* Katika Jarida la Sumait University Journal, Na.3, uk. 1 - 16.

Mbonde, J. P. (2002).*Uhakiki na Uchambuzi wa Tamthiliya, Riwaya na Ushairi*. Dares Salam: Mkuki na Nyota Publishers.

Mlacha, A. C. (1986). *Mwongozo wa Nyota ya Rehema*. (Tasinifu ya M.A Kiswahili) Nairobi University. Imepakuliwa kutoka: www. maktaba.ku.ac.ke. Tarehe 2 March, 2020. Saa 4.52 jioni.

Muhammed, S. A. (1990). *Kivuli Kinaishi*. London: Oxford University Press.

Mohamed, S. M. (1972). *Kiu*. Nairobi: East African Publishing House.

Mohammed, S. M. (1976). *Nyota ya Rehema*. Nairobi: Oxford University Press.

Mulokozi, M. M. (1983). *Dunia Uwanja wa Fujo*. Katika Jarida la Taasisi ya Uchunguziwa Kiswahili. Na 50/1 ukr. 1-12.

Mwanjala, S. M. (2011). *Dhana ya Maisha katika Riwaya Mbili za E. Kezilahabi:Kichwamaji na Dunia Uwanja wa Fujo*. Imepakuliwa kutokawww. afrika. univie.ac.at tarehe 2/3/2020. Saa 11:00 alasiri.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustana College.

Noronha, L. (2009). *Uchambuzi wa Riwaya ya Kiu*. Imepakuliwa kutokawww. afrika. univie.ac.at tarehe 22/5/2020 saa 10:00 alasiri.

Nyaosi, K. N. (2008). *Taswira ya Ndoa katika Riwaya mbili za Kiswahili: Kiu na Msimuwa Vipepeo.*Tasinifu ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Onchangu, R. N. (2013). *Mtindo katika Riwaya na Hadithi Fupi za Clara Momanyi*. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Dar es Saalam.

Saleem, M. (2013). *Maudhui na Fani katika Tamthiliya za Kiswahili: Utafiti Linganishiwa Tamthiliya ya Mashetani na Kivuli Kinaishi*. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Dar es Saalam.

Sengo, T. S. Y., na Kiango, S. D. (2012). *Hisiya Zetu*. Dar es Salam: ChuoKikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi Nadharia na Tahakiki*. Dar es salaam: Dar es salaam University Press.

Shafi, A. S. (1979). *Kuli.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Wafula, R. M., na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: The Jomo Kenyatta foundation.

Wamitila K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publisher.

Wamitila K. W. (2010). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.*Nairobi: Vide - Muwa Publishers Ltd.

Wamitila K. W. (2013). *Mikakati ya Uhalisiaajabu katika Riwaya ya Kiswahili: MulikaNa. 32 ukr. 1-12*. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salam.

Kufanana kwa Matumizi ya Lugha katika Diwani ya *Dhifa* na *Wasakatonge*

Emhemad Abdallah Alhabib
Idara ya Lugha na Fasihi, Chuo Kikuu cha Sebha Libya
Baruapepe: *alfasi20@yahoo.com*

Omary Mohamed Maguo
Idara ya Lugha na Fasihi, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
Baruapepe: *omarymohamed36@gmail.com*

Ikisiri

Ushairi wa Kiswahili katika mazingira ya Afrika Mashariki unatumika kama chombo kinachomudu mahitaji na harakati za kijamii kwa kutumia mbinu za kisanaa. Baadhi ya mbinu hizo ni matumizi ya mitindo kama vile lugha, muundo, wahusika na mandhari. Makala hii imechunguza kipengele cha matumizi ya lugha katika diwani teule za *Dhifa* (2008) na *Wasakatonge* (2004). Baadhi ya vipengele vilivyojadiliwa katika makala hii ni sitiari, tashibiha, jazanda na takriri. Kilichochunguzwa hapa ni kufanana kwa vipengele vya matumizi ya lugha kwa kurejelea diwani zilizobainishwa. Data za msingi za makala hii zilikusanywa katika diwani teule kwa kutumia mbinu wa usomaji makini. Mapitio ya data za upili zilizotumika kurejelea na kuthibitisha data za msingi zilipatikana kwa mbinu ya upitiaji wa nyaraka. Uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa uliongozwa na nadharia ya Simiotiki. Makala inahitimisha kuwa ushairi wa Kiswahili una utajiri mkubwa uliojilimbikiza katika vipengele vya lugha. Lugha ndicho chombo cha mawasiliano yanayohitilafiana kulingana na muktadha, pamoja na utamaduni wa jamii inayohusika.

Utangulizi

Lugha ni kipengele muhimu kinachotofautisha sanaa ya fasihi na sanaa nyingine. Fasihi ya Kiswahili ina utajiri mkubwa uliojilimbikiza katika vipengele vya lugha (Omary, 2013). Lugha ndicho chombo cha mawasiliano ambayo huhitilafiana kulingana na mazingira, pamoja na utamaduni wa jamii inayohusika. Mawasiliano hufanywa kisanaa

katika kazi za kifasihi kwa kuzingatia muktadha mahsusi wa jamii. Maelezo haya yanatoa mwelekeo unaoisukuma mbele makala hii iliyolenga kufafanua kufanana kwa vipengele vya lugha katika diwani teule za *Dhifa* (2008) ya Euphrase Kezilahabina ile ya *Wasakatonge* (2004) ya Mohamed Khatibu.

Wasanii huyalinganisha mambo mbalimbali na hali za maumbile na jamii ili kutoa mafunzo na kuufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa jamii iliyolengwa. Kwa kawaida, kazi ya kifasihi huwa na mawazo, pamoja na usanii unaoweza kujibainisha katika vipengele mbalimbali. Msokile (1992) akisisitiza hoja hiyo, anaeleza kuwa kazi yoyote ya fasihi sio fikira na mawazo tu; pamoja na hayo, ni ufundi na usanii uliomo. Usanii huo huambatana sana na mcharazo wa matumizi ya lugha ambao unajidhihirisha katika vivuli mbalimbali vya maana, tamathali na jazanda zinazochorwa kutegemea tamaduni za wasanii wanaohusika. Fasihi si fikira na mawazo tu, bali lazima kuwe na kiungo kingine kama ilivyodokezwa katika aya iliyotangulia. Aidha, sharti kuwepo na muundo, usanii wa lugha, ubunaji wa visa na vitu, ufinyanzi wa wahusika na wasilisho la wakati, majira na mabadiliko ya mazingira ili kuiteka hadhira (Simala, 2004). Jumla ya mambo haya yote yanaonesha uhusiano mkubwa uliopo baina ya vipengele vya fani na maudhui katika kazi yoyote ya kifasihi.

Katika kipengele cha matumizi ya lugha tumechunguza kipengele cha tamathali za semi. Mojawapo ya majukumu yake ni kuiburudisha na kuzindua akili ya msomaji au msikilizaji na kuacha athari ya kudumu katika hisi na mawazo yake (Ngure, 2003). Katika sehemu inayofuata tumejadili tamathali za semi kwa kuziweka katika muktadha mpana wa tanzu zilizochunguzwa. Mjadala ulilenga kufafanua vipengele vya matumizi ya lugha kwa kurejelea diwani za *Dhifa* na *Wasakatonge*. Baadhi ya vipengele vya lugha vilivyojadiliwa katika makala hii ni sitiari, tashibiha, jazanda na takriri.

Mbinu na Upeo wa Makala
Katika miaka ya hivi karibuni, ushairi huru umepata muktadha na uwanja mpana zaidi kimatumizi. Kadiri siku zinavyozidi kwenda

mbele, baadhi ya waandishi wa ushairi wa kimapokeo wameanza kutunga mashairi yanayokaribiana na mashairi ya huru. Makala hii imeshughulikia kipengele cha matumizi ya lugha katika diwani teule za *Dhifa* (2008) na *Wasakatonge* (2004). Kilichochunguzwa hapa ni kufanana kwa vipengele vya matumizi ya lugha kwa kurejelea diwani teule zilizobainishwa. Data za msingi za makala hii zilikusanywa katika vitabu teule kwa kutumia mbinu wa usomaji wa nyaraka. Mapitio ya data za upili zilizotumika kurejelea na kuthibitisha data za msingi zilipatikana pia kwa mbinu ya usomaji wa nyaraka. Uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa uliongozwa na nadharia ya Simiotiki.

Mwega wa Uhakiki Kinadharia
Semiotiki ni nadharia inayoshughulika na ishara pamoja na uashiriaji katika kazi za kifasihi (Cameron, 1985). Aidha, ni taaluma ya mfumo wa alama katika mawasiliano ya kutumia lugha Ishara zinazojitokeza katika fasihi huundwa na mtunzi kwa kuzingatia muktadha wa jamii na binadamu ndiye mtengenezaji wa alama mbalimbali za ishara ambazo huzitumia katika mawasiliano yake ya kila siku (Elam, 1980). Hadhira inayolengwa hutengeneza maana mbalimbali kupitia ubunifu na tafsiri zao juu ya alama na ishara inazokutana nazo katika kazi za kifasihi inazozisikiliza au kuzisoma. Nadharia hii iliasisiwa na mwanaisimu wa Ki-Swizi, Ferdinand de Saussure, pamoja na Charles Pierce (Nazarova, 1996).

Katika makala hii, mtafiti amechunguza kipengele cha lugha kuwa ni chombo muhimu cha kifasihi; na kwamba fasihi ina athari kubwa katika jamii inayohusika. Kwa kurejelea nadharia teule, waandishi wa diwani teule waliwekwa katika muktadha wao wa kawaida, ulio wazi na halisi ili kujua mwenendo na shughuli zao kupitia kipengele cha lugha, kwa kuwa, mashairi yao ni viungo vyao. Jamii iliyolengwa iliwekwa katika ulimwengu wake wa kawaida, kweli na wazi ili kufanya uchambuzi na uhakiki wa kina. Kwa hiyo, nadharia hii imetumika kuchunguza kipengele cha matumizi ya lugha katika mashairi kwa kurejelea diwani teule zilizochunguzwa.

Kufanana kwa Matumizi ya Lugha katika Diwani Teule
Lugha ni kipengele muhimu katika kazi ya fasihi kwa kuwa ndio mzizi wa kazi ya fasihi; bila yenyewe kuwepo haiwezekani kuwa na fasihi (Wamitila, 2008). Kwa kawaida, msanii hutumia lugha kuyaibusha mawazo yake. Waandishi wa diwani za *Dhifa* na *Wasakatonge* ni miongoni mwa watumiaji wa vipengele mbalimbali vya lugha. Makala hii imeteua baadhi ya vipengele vya lugha ili kuwakilisha eneo kubwa lililobaki. Katika sehemu hii tumewasilisha baadhi ya vipengele vya lugha vinavyojitokeza katika diwani teule za *Wasakatong*e na *Dhifa*.

Matumizi ya Sitiari
Sitiari ni tamathali ya semi ya ulinganisho ambayo inalinganisha vitu viwili kana kwamba vitu hivyo vinafanana kabisa bila ya kuwa na tofauti hata kidogo (Njogu na Chimerah, 1999). Katika diwani ya *Wasakatonge* kuna matumizi ya sitiari katika mashairi kadhaa kama ilivyobainishwa katika shairi la '*Usiku wa Kiza'*:

> Meniondokeya, wangu mahabuba,
> Nilikuzoweya, kwa yako mahaba,
> Nnajikondeya, sili nikashiba.
>
> Sili nikashiba, mwili ukajaa,
> Sinayo haiba, sura mesinyaa,
> Wewe ndiyo tiba, unayenifaa (uk. 27).

Beti hizi mbili zinadhihirisha matumizi ya sitiari ambapo mapenzi yanaoneshwa kuwa na uwezo wa kumfanya mtu akala chakula, lakini hashibi na wakati huo huo mapenzi yanaweza kuwa tiba ya kutibu maradhi aliyonayo mtu. Sitiari hii ambayo inayafananisha mapenzi kuwa ni sawa kabisa na dawa yenye uwezo wa kutibu maradhi. Sitiari hii imesaidia kusisitiza kuwa mapenzi ni kitu chenye nguvu katika maisha ya binadamu na haitakiwi kukifanyia mchezo hata mara moja. Shairi la '*Machozi ya Dhiki'* linafafanua zaidi:

> Machozi ya dhiki, yanibubujika,
> Huku nahiliki, sana nateseka,
> Wangu muashiki, umeadimika,
> Wala sidhihaki, nnadhulumika (uk. 28).

Shairi hili lina ubeti mmoja tu na mstari wa kwanza wa ubeti huu una matumizi ya sitiari ambayo ni machozi ya dhiki. Kinachoelezwa hapa ni kwamba kukosa mapenzi kutoka kwa mtu umpendaye inaweza kuwa ni ugonjwa mkubwa ambao unaweza kumfanya mtu akawa anatokwa na machozi yasiyoonekana. Machozi ya dhiki ni ufanano wa hali dhalili ambayo haisemeki kabisa inayomfanya mtu kushindwa hata kutimiza majukumu yake katika jamii. Shairi la '*Buzi Lisilochunika*' nalo lina matumizi ya sitiari kama inavyoelezwa:

> Hili buzi buzi gani, buzi lisilochunika,
> Halina ngozi laini, inayoweza kutoka,
> Lina manyoya mwilini, ambayo yamefunika (uk. 45).

Ubeti huu unabainisha bayana kuwa buzi linalosemwa hapa ni mtu ambaye hatoi fedha zake kwa wanawake ovyo ovyo kwa lengo la kupewa mapenzi. Kitendo cha mtu, hasa mwanaume kuwa mgumu katika kutoa fedha kwa wanawake wenye tabia ya kuhongwa ndio kinamfanya aitwe buzi lisilochunika ngozi yake. Mbuzi anapochinjwa, tunatarajia kuona akichunwa ngozi yake; kisha nyama hugawanywa katika vipande tayari kwa matumizi. Wakati mwingine, hutokea kukawa na mbuzi ambaye ngozi yake ni ngumu na ni vigumu kuichuna. Wapo wanaume ambao hawatoi fedha kwa wanawake wa nje ya ndoa au hata ndani ya ndoa. Hawa ndio ambao wanaitwa kuwa ni mabuzi. Katika diwani ya *Dhifa*, kuna matumizi ya sitiari kama ilivyobainishwa katika shairi la '*Njia Tuliyopitishwa*'. Shairi linaeleza:

> Ingawa hatuna machozi ya moto,
> Yatayofuta aibu hii tukufu,
> Bendera ya haki itapepea daima,
> Daima tutakuwa na kuwako,
> Mbele ya umoja thabiti,
> Milima na vichuguu hulala (uk. 3).

Mshororo wa kwanza ndio ambao una matumizi ya sitiari hususani maneno 'machozi ya moto', ambayo imetumika kuonesha kuwa haki katika jamii ni kitu ambacho kinatakiwa kupiganiwa bila ya kuchoka.

41

Machozi ya moto ni kauli ambayo inatoa hamasa kwa wananchi kuhakikisha kwamba hawaachi kupigania haki zao kwa kuwa palipo na haki uongo hujitenga. Matumizi mengine ya sitiari yanaonekana katika shairi la '*Kijumba*':

> Hofu ya kuvuka ni ya wakuzikao,
> Wasojua utamu wa sahau,
> Kufa ni kufungua kamba za viatu,
> Zilizokushinda kufungua muda mrefu,
> Wakati vipya vyasubiri,
> Vilio ni simama deedee,
> Nikupe mkaatee! (uk. 21).

Sitiari inajitokeza pale inapoelezwa kuwa 'kufa ni kufungua kamba za viatu', ambazo zilimshinda mtu kufungua muda mrefu kitu ambacho kinatufanya tuone kuwa kifo ni kitu cha kawaida sana. Katika hali ya kawaida, kifo ni kitu ambacho kinaogopwa sana katika jamii. Mshairi anakieleza kifo kuwa ni kitu cha kawaida sana ambacho watu hawapaswi kukiogopa. Pia, vilio ambavyo wanakuwa wakilia wafiwa baada ya kuondokewa na mpendwa wao vinalinganishwa na michezo ya watoto ambao hauna maana yoyote. Kwa maneno mengine ni kuwa hakuna haja ya watu kulia msibani kwa sababu ni jambo la kawaida mno kwani kila binadamu ataonja mauti.

Matumizi ya Tashibiha
Tashibiha ni tamathali ya usemi ambayo inalinganisha vitu kwa kutumia viunganishi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kama, kama vile, sawa sawa na, kana kwamba mithili ya, mfano wa, kutaja kwa uchache (King'ei, 2002). Shairi la '*Mahaba*' lililopo katika *Wasaka Tonge* ni mfano mzuri wa matumizi ya tashibiha ambapo kuna beti 4 na zote zina matumizi ya tashibiha, hususani katika mshororo wa kwanza wa kila ubeti kama ilivyooneshwa katika beti hizi:

> Kama mahaba mzigo, nitwike usinituwe,
> Lau ni pande la gogo, liache silipasuwe,
> Kama mahaba kipigo, ni radhi kinisumbuwe,
> Kama mahaba maudhi, nipe ili uenziwe,

Hata madhila naridhi, wala usishutumiwe (uk. 1).

Matumizi ya tashibiha katika beti za shairi hili yapo wazi ambapo mapenzi yanafananishwa na mambo mbalimbali ambayo kwa hakika yanaonesha kuwa mapenzi ni kitu chenye nguvu sana katika jamii. Mathalani, kuna mshororo mmoja unasema, kama mapenzi ni mzigo, basi mbebaji asituliwe mzigo huo aendelee kuubeba tu katika maisha yake yote. Kubeba mzigo kwa muda mrefu bila ya kuutua ni adha kubwa ambayo inaweza kumfanya mtu kupata madhara katika mwili wake. Haijalishi kwa mtu mwenye mapenzi ya dhati kwa ampendae, atavumilia tu. Hapa kinachoelezwa ni hali ya uvumilivu katika suala zima la mapenzi. Mapenzi wakati mwingine hukumbwa na changamoto na kuwa ni mithili ya mzigo mzito ambao wakati mwingine ni kuubeba ni vigumu. Pia, katika shairi '*Kansa*' mwandishi anaeleza:

Imekuwa ni donda, donda lisotibika,
Limeanza kuvunda, kuvunda kupasuka,
Lanuka kama ng'onda, ng'onda asokauka (uk. 4).

Mshororo wa mwisho wa ubeti huu ndio ambao unadhihirisha matumizi ya tashibiha ambayo inarejelea madhara ya uongozi mbaya katika jamii. Uongozi mbaya wa kujihusisha na vitendo vya rushwa ni sawa na ugonjwa wa kansa (Songoyi, 1988). Kansa ikiishaingia mwilini na kusambaa sehemu kubwa ya mwili ni vigumu sana kuitibu. Hivyo, viongozi wengi wa ngazi zote za utawala wakijiingiza katika rushwa na ufisadi inakuwa si jambo jepesi kukomesha hali hiyo. Hii inakuwa sawa sawa na ugonjwa wa kansa.

Matumizi ya tashibiha yanajitokeza kwa kiasi kikubwa katika mashairi ya *Dhifa* jambo linaloashiria kuwa mtunzi ni bingwa wa matumizi ya tashibiha. Shairi la '*Kwa Walimu Wote*' lina matumizi ya tashibiha katika ubeti wa mwisho wa shairi hilo:

Sikilizeni kwa makini,
Umoja hatuna,
Twasambaratika kama nyumbu,

43

> Tulichonacho ni woga,
> Na kinachotuunganisha ni unafiki,
> **Lakini tusikate tamaa kama mbuni,**
> Tukiupata umoja bado tunayo silaha,
> Kura (uk. 1 - 2).

Maneno katika mistari iliyokelezwa wino katika dondoo hapo juu ndiyo ambayo yanathibitisha uwepo wa tashibiha katika shairi linalohusika. Shairi hili linawalenga walimu ambao wanadaiwa kuwa hawana umoja pale wanapokuwa wanapigania haki zao za msingi. Hali hiyo inafananishwa na namna nyumbu wanavyosambaratika wanafukuzwa na simba ama chui. Kila mmoja hukimbia kwa kutumia njia yake na yule ambaye ni dhaifu hukamatwa kiurahisi na kuliwa. Walimu wanapokosa umoja miongoni mwao, basi na utatuzi wa changamoto na madai yao pia huwa ngumu kutatuliwa kwa haraka. Matumizi mengine ya tashibiha yanajitokeza katika shairi la '*Mpiga Zeze*':

> Nilikuwepo Maira alipoliwa na simba,
> **Alipiga kelele kama mbuzi,**
> Hadi simba alipong'oa ulimi wote,
> Kuzima domo lake pana (uk. 8).

Mshororo uliokolezwa wino una matumizi ya tashibiha ambapo inaelezwa kuwa kitendo hicho cha kuliwa na simba kilikuwa ni cha uchungu mkubwa kwa muhusika. Tashibiha hii imetumika kutoa msisitizo wa dhamira kwa msomaji na msikilizaji wa shairi hili. Matumizi mengine ya tashibiha tunayapata katika shairi la "*Mke wa Waziri* (Wimbo wa Harusi)" lililopo katika ukurasa wa 13 pale anaposema:

> **Chogo limechongoka kama senene,**
> Aendaye kwenye harusi ya mende,
> Na kutusanifu kwa mawani meusi,
> **Kama nyani achezaye sarakasi**.

Mishororo iliyokolezwa wino ina matumizi ya tashibiha ambapo ile ya kwanza imetumika kama lugha ya utani lakini inaeleza dhamira fulani kwa wasomaji na wasikilizaji wa shairi hilo. Pia mshororo wa nne nao pia una tashibiha ambayo ni ya kimzaha, lakini ina ujumbe ndani yake. Baadhi ya viongozi wanapopata madaraka hujisahau na kujiona wao ni bora na watukufu zaidi kuliko wale ambao wamewachagua na kuwapa nafasi hizo za uongozi. Matumizi ya tashibiha yanaendelea kujitokeza katika mashairi mengine kama '*Wakati Fulani'*, '*Mtakaso*' na '*Niliona*' yaliyopo katika ukurasa wa 15, 19 na 33. Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa mashairi katika diwani ya *Dhifa* yana matumizi makubwa ya tashibiha.

Lugha ya Mafumbo

Kwa kawaida, kazi ya ushairi inajulikana kama sanaa ilijaa matumizi ya mafumbo. Katika ushairi huwa kunakuwa na matumizi ya lugha ya mafumbo ambapo jambo linaloelezwa mara nyingine huwa sio hilo, bali kuna jambo jingine ndani yake (Alhabib, 2012). Shairi la '*Vitamu*' ambalo lipo katika ukurasa wa 44 wa diwani ya *Wasaka Tonge* limeundwa kwa lugha ya mafumbo:

> Vitamu vinapopikwa, vyema vikaandaliwa,
> Viungo vikapachikwa, vizuri kuchanganyiwa,
> Vya kupaza na kupakwa, kwa utamu hunogewa.

Ubeti huu umetumia lugha ya mafumbo ambapo vitamu vinavyosemwa hapa ni tendo la ndoa ambapo inaelezwa kuwa ni vizuri wahusika wakaandaana kabla ya kuingia moja kwa moja katika tendo hilo. Maandalizi ni muhimu kwa pande zote mbili ili kuweka mambo vizuri. Jambo hili limesemwa mahali pengi, ikiwa ni pamoja hata na wataalamu wa masuala ya ndoa na mahusiano. Shairi la '*Sivui Maji Mafu*' limeundwa kwa lugha ya mafumbo kama ilivyobainishwa katika mafungu haya:

> Uvuvi wa maji mafu, hauna hata tijara,
> Samaki wake hafifu, hapana ila hasara,
> Ni kazi ya usumbufu, wavuvi unatukera.
>
> Kuvua pono ni tusi, na kauzu toratora,

> Vikolekole vyepesi, ni kitoweo uchwara,
> Vijipweza na vingisi, kwangu si vyakula bora.
> …
> Huvua mikarambisi, misamaki ilofura,
> Mijipapa sio tasi, mijodari na sangara,
> Vitowezi wasiwasi, mimi vyanikerakera (uk. 33).

Beti hizi tatu zinazungumza juu ya watu wazima kuwa na mahusiano ya kimapenzi na watoto wadogo ambao wamewazidi umri. Mafumbo yamejengwa kupitia majina ya samaki yaliyotajwa kwenye beti zinazohusika kuonesha kuwa katika jamii wapo watu ambao huwa na mahusiano ya kimapenzi na watoto wadogo. Jambo jema kwa watu wazima kuwa na mahusiano ya kimapenzi na watu wazima wenzao ambao wanalingana au kukaribiana kwa umri kuliko kuwa na mahusiano na mtu ambaye anaweza kuwa mtoto au mjukuu kwa mhusika. Haya yanatibitishwa katika ubeti wa 4 wa shairi hapo juu. Samaki aina ya mikarambisi ni samaki wakubwa wanaohusisha jodari na sangara. Samaki hawa wanafananishwa na watu wazima ambao tayari wanaelewa maana ya mapenzi na sio watoto wadogo ambao bado hawajapevuka kikamilifu.

Matumizi ya lugha ya mafumbo yanajitokeza pia katika mashairi mengi ya diwani ya *Dhifa* ambapo mshairi anaeleza dhamira zake kwa lugha ya kufichaficha. Shairi la '*Madomo Mapana*' linaeleza:

> Ng'ombe amekamuliwa na Wazungu,
> Waarabu, Wahindi, na Wao,
> Sasa anatoa damu,
> Vilivyobaki ni chai ya rangi,
> Na madomo mapana zaidi,
> Yaliyo bado hai,
> Kuimba nimeimba (uk. 7).

Shairi hili limetumia maneno ya kawaida kabisa, lakini yenye mafumbo ndani yake ambapo ng'ombe anayetajwa hapa ni nchi ambazo zilitawaliwa na Wakoloni ambao walinyonya rasilimali za Makoloni

kwa lengo la wao kuzipatia maendeleo nchi zao za huko Ulaya. Pamoja na rasilimali za nchi kunyonywa na Wakoloni, pia wapo baadhi ya viongozi ambao nao wamebadilika na kuwa wahujumu wa mali, rasilimali na maendeleo ya jamii na taifa (Shivji, 2002). Hawa ndio ambao wanatajwa na kuelezwa kuwa ni madomo mapana ambayo bado yapo hai. Shairi lingine ambalo lina matumizi ya lugha ya mafumbo ni '*Zimwi*' linaeleza:

> …
> Zimwi litujualo limetula likatwisha,
> Mchangani limekunguwaa kivulini,
> Likiota pa kujisaidia,
> Nzi watambaa wakinyonya udenda,
> Watoto ndani wahesabu mali,
> Wakifikiria pa kutoboa (uk. 40).

Ubeti huu una matumizi ya lugha ya mafumbo na hususani kutumiwa kwa 'Zimwi', ambapo anaweza kuwa ni kiongozi ambaye ameiongoza jamii yake vibaya. Kiongozi ambaye kazi yake ni kula rushwa na kusababisha wananchi wake kuendelea kuwa maskini. Viongozi wa aina hii wapo katika jamii na wanapaswa kukomeshwa. Kipengele cha jazanda kimeelezwa katika diwani ya *Dhifa*. Jazanda huelezwa kama ni tamathali ya semi ambayo inalinganisha vitu viwili bila kutumia kiunganishi (Rajabu, 2012). Matumizi ya tamathali hii yanajibainisha katika katika shairi la '*Jibwa*' lililodondoa fungu lifuatalo:

> Jibwa likianza kula mayai,
> Jua wizi limefuzu,
> Kesho litakula kitovu,
> Cha mtoto wako pekee,
> Jibwa jizi fisi (uk. 5).

Mshororo wa mwisho ndio ambao una matumizi ya jazanda ambapo mbwa anafananishwa na fisi, lakini bila ya kutumia kiunganishi. Fisi ni mnyama ambaye kazi yake kubwa ni kuvizia na kula masalia ya mnyama aliyeliwa na wanyama kama simba, chui na mbwa mwitu.

Katika mukatadha huu anarejelewa mtu mwenye mamlaka na madaraka ya kuitumikia jamii, lakini kazi yake kubwa ni kutumia rasilimali za jamii yake kwa maslahi binafsi. Kiongozi huyo anachukua kila kitu na kuiacha jamii katika hali ya umaskini.

Lugha Isiyo ya Tafsida
Lugha ya tafsida ni ile ambayo inatumika kutaja vitu au mambo ambayo katika hali ya kawaida hayawezi kutajwa katika hadhara bali katika faragha. Watunzi wengi wa kazi za fasihi hutumia lugha ya tafsida, lakini Kezilahabi hutumia lugha isiyokuwa ya tafsida katika baadhi ya kazi zake. Mfano mzuri katika diwani ya *Dhifa* kupitia shairi la '*Niliona*':

> Mawazo yakitimua mbio,
> Pumbu na shanga vikionekana,
> Kama mbwa wafukuzao cheche,
> Na baada ya muda kurudi wakichechemea,
> Na kulialia, damu zikiwachuruzika,
> Kwa mwindaji asiye jina,
> Aliyedhihirisha kwa ishara niliona (Uk. 33).

Dondoo hili lina matumizi ya lugha ya wazi ambayo si ya tafsida hususani katika mshororo wa pili. Pumbu ni kiungo katika sehemu ya uume na kwa jina jingine huitwa korodani. Matumizi ya lugha ya aina hii ni nadra sana kuyakuta yakitokea katika fasihi ya ukanda wa Pwani katika mashairi kama ya diwani ya *Wasakatonge*. Hali hii ni kwa kuwa kwa mujibu wa mila na desturi za Waswahili hairuhusiwi kabisa kutaja maneno ya faragha kwa lugha isiyokuwa ya tafsida. Huo ndio ustaarabu wa Waswahili.

Lugha ya Takriri
Takriri ni lugha ya marudiorudio ambayo hujitokeza katika njia mbalimbali kama vile takriri silabi, neno, aya na wakati mwingine katika sentensi nzima kurudiwarudiwa. Kwa minajili ya malengo ya makala hii tumeona tutolee mfano shairi la '*Afrika*' (uk. 6) kama linavyoeleza:

> Lini?
> Afrika utakuwa,
> Bustani ya amani,
> Ukabila kuuzika,
> Udini kuufyeka
> Ni lini?
> Lini?
>
> Afrika utakuwa,
> Ziwa la utulivu,
> Kufisha uonevu,
> Kumaliza uovu,
> Ni lini?

Mshororo wa kwanza unajirudia kila mwanzoni mwa ubeti na mwishoni mwa ubeti. Nchi za Afrika zinatakiwa kushughulikia masuala yanayohusu ukabila na uonevu kwa haraka sana kwani mambo hayo hayana nafasi tena katika kipindi hiki cha maendeleo ya sayansi na teknolojia (Alan, 2016). Pia, mshororo wa pili nao unajirudia na katika beti zote kumi na mbili kwa namna ileile. Hapa unapatikana msisitizo mkubwa juu ya Afrika kuhakikisha kuwa inakuwa ni mahali salama pa kuishi. Matumizi mengine ya takriri yanajitokeza katika shairi la '*Tonge la Ugali*':

> Wanasemana,
> Wanasutana,
> Wanakanyana,
> Kwa tonge la ugali!
>
> Wanasegana,
> Wasuguana,
> Watukanana,
> Kwa tonge la ugali! (uk. 20).

Shairi hili lina jumla ya beti 4 na kila ubeti una mishororo minne na ule mshororo wa nne unajirudia katika beti zote. Kibwagizo "Kwa tonge la ugali," kimerudiwa katika beti zote kutoa msisitizo kwamba matatizo mbalimbali ambayo yanatokea katika jamii ya leo yanasababishwa kwa kiasi kikubwa na tamaa ya tumbo. Ile hali ya watu kutaka kupata zaidi kuliko wengine ndio ambayo huwajengea watu tabia ya ubinafsi, uroho na uchu wa mali na rasilimali za jamii na taifa (Karugendo, 2016). Njaa ni adui mkubwa wa binadamu kwani anaweza kufanya jambo lolote lile ili aweze kutibu njaa yake. Hata hivyo, zipo njaa nyingine ambazo ni za ziada na ndizo zinazowafanya watu kuwa wabinafsi.

Matumizi ya lugha ya tanakali sauti mara nyingi hujitokeza pale ambalo kuna kuwa na mwigo wa sauti unaotokana na kutendwa kitendo fulani. Katika diwani ya *Dhifa* yapo mashairi kadhaa ambayo yana matumizi ya tanakali sauti na shairi la 'Puuu!' ni mfano mzuri na hapa chini tumedondoa shairi hilo:

> Sitaki! Sitaki!
> Puuu!
> Sitaki! Sitaki!
> Puuu!
> (Kimya) (uk. 41).

Shairi hili linaweza kuelezwa kwa namna mbalimbali lakini ile tunayoiona sisi ni kama tukio la ubakaji ambapo aliyekuwa akibakwa ndiye aliyekuwa akisema "sitaki," lakini mbakaji alikuwa akimwangusha chini. Inaonekana azma ya ubakaji ilikamilika kwani inaelezwa kuwa baada ya mabishano na mapambano kisha kukawa kimya. Hapo katika kimya inaonekana ndipo kitendo hicho kiovu kikafanyika ambacho kwa dhati kabisa hakikubaliki katika jamii. Shairi lingine ambalo lina matumizi ya tanakali sauti ni '*Pa*!' ambalo ndilo shairi la mwisho katika diwani hii. Shairi hili (uk. 60) tumelidondoa kama ifuatavyo:

Pa! Pa! Pa!
(Kimya)
Pa!

Shairi hili linaweza kuelezwa kwa namna nyingi lakini kikubwa ni kama mtu aliyejifungia ndani ya nyumba kisha akawa anajipigiza chini au ukutani kutokana na sababu mbalimbali pengine wivu wa mapenzi, hali ngumu ya maisha, msongo wa mawazo na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Wakati mwingine, inawezekana hata mtu akawa hajipigi ukutani wala kujipigiza chini lakini ule ugumu wa maisha unamfanya asikie sauti kama hii katika mawazo yake. Ugumu wa maisha si jambo jema sana katika jamii linaathari nyingi sana.

Matumizi ya Tashihisi
Tashihisi ni tamathali ya semi ambayo inavipa urari wa kutenda kama binadmu viumbe ambavyo havina uwezo huo (Mulokozi, 1996). Katika ulimwengu wa fasihi ni jambo la kawaida kusikia miti inatajwa kuwa inacheka au inanung'unika, mbwa anasoma, sungura anaandika, fisi anacheka na jiwe linaongea. Katika diwani ya *Dhifa* kupitia shairi la '*Bonde*' lililopo katika ukurasa wa 29 tumeona matumizi ya tashihisi kama ifuatavyo:

Hapo zamani za kale palikuwa na giza,
Halafu kutoka mlima Kilimanjaro jua likachomoza,
Kwa tabasamu likang'ara juu ya nchi,
Pakawa na mwanga.

Halafu kutoka mlimani maneno makubwa,
Yalijiviringisha kwa nguvu za wazo,
Yakiangusha miti na nyumba za waliojua kusema,
Pakawa na ukimya.

Katika hali ya kawaida jua huwa halitabasamu bali ni wanadamu ndio wenye sifa na uwezo wa kutabasamu. Lakini, kupitia dondoo hapo juu hasa ubeti wa kwanza mshororo wa tatu tunaelezwa kuwa jua lilitabasamu. Hii inarejelea juu ya Mwenge wa uhuru kuwekwa juu ya

mlima Kilimanjaro kwa lengo kumulika nchi nzima ili pale penye chuki pawe na upendo na pale pasipokuwa na matumaini pawe na matumaini. Katika ubeti wa pili tunaambiwa kuwa maneno kutoka mlimani yalijiviringisha mpaka chini na kuangusha miti na nyumba za watu. Katika hali ya kawaida, maneno hayana uwezo wa kuvunja miti na nyumba ila kinachosemwa hapa ni kuwa, wanajamii walinyimwa fursa ya kuamua juu ya mambo mbalimbali kuhusu maisha yao na viongozi ndio ambao walikuwa wakiamua kila kitu kwa niaba yao.

Hitimisho
Makala hii imeshughulikia matumizi ya lugha katika diwani mbili za *Wasakatonge* na *Dhifa*. Kwa hakika, watunzi Mohamed Khatib na Euphrase Kezilahabi wanaonekana kuwa ni wapevu katika fani ya ushairi wa Kiswahili. Matumizi mzomzo ya lugha katika mashairi yao yameundwa kwa ustadi wa pekee unaosaidia kuufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa manufaa makubwa. Kupitia matokeo ya makala hii tumeweza kufafanua na kuthibitisha kwa vitendo na uhalisi kuwa matumizi ya lugha katika diwani ya *Wasakatonge* ni mashairi ya kati mbayo si ya kimapokeo wala ya kisasa. Kwa upande wa Kezilahabi, utunzi wa mashairi yake, kwa kawaida, si ya kimapokeo wala ya kati.

Marejeleo
Alan, I. (2016, Agosti 15 – 21). 'Tusifuate Nyayo za Musseven'. *MwanaHalisi*. Namba 352, uk. 3.

Alhabib, M. (2012). Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Taarabu. Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Cameron, D. (1985). *Feminism and Linguistic Theory*. London: Macmillan.

Elam, K. (1980). *The Semiotics of Theatre and Drama*. London: Methuen.

Karugendo, P. (2016, Mei 16 – 22). 'Tuliokoa Wenzetu, Sasa Tumeatamia Uovu'. *MwanaHalisi*. Na 339, uk. 2.

Kezilahabi, E. (2008). *Dhifa*. Dar es Salaam: Vide-muwa.

Khatibu, M. S. (2005). *Wasakatonge*. Dar es Salaam: TUKI.

King'ei, K. (2002). 'Suala la Uana katika Fasihi ya Kiswahili: Uhakiki wa Utafiti Kutoka Kenya katika Utafiti wa Kiswahili'. Moi University Press. Uk. 87 - 95.

Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha.* Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributor Limited.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Nazarova, T. (1996). *Linguistics and Literary Semiotics*. Moscow: Moscow State University Press.

Ngure, A. (2010). *Fasihi Simulizi katika Shule na Sekondari.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Omary, M. H. (2013). Nafasi ya Hadithi Simulizi katika Kufunza Maadili Mema Shule za Sekondari, Visiwani Zanzibar. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Rajabu, A. (2012). Misemo ya Kiswahili katika Vazi la Fulana: Uchambuzi wa Dhamira na Matumizi ya Lugha. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Shivji, I. (2002). Makuadi wa Soko Huria (Chachage, S. C), Hotuba ya Uzinduzi wa Kitabu. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI, katika Mulika 26, uk, 17 – 24.

Simala, K. I. (2004). 'Uzalendo wa Lugha ya Kiswahili Enzi za Utandawazi'. Dar es Salaam: BAKITA.

Songoyi, E. M. (1988). The Artist and the State in Tanzania: Study of Two Singers, Kalikali and Mwinamila. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Majina ya Kigeni Wanayopewa Watoto katika Jamii za Tanzania

Mussa E. Msamilah
Idara ya Taaluma, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu
Baruapepe: *mmsamilah@gmail.com*

Ikisiri

Mtoto anapozaliwa katika jamii yoyote hupewa jina linalokuwa utambulisho wake. Wazazi na wanajamii kwa ujumla huwapa watoto majina kutokana na sababu mbalimbali. Makala hii, imeshughulikia majina ya lugha za kigeni wanayopewa watoto katika jamii za Tanzania. Pia, imeleza sababu na athari za wazazi kutowapa watoto majina ya lugha za jamiilugha za Tanzania. Aidha, inaonesha uelewa wa Watanzania kuhusu majina kutoka katika lugha za kigeni wanayowapa watoto wao. Data za msingi zilizotumika katika makala hii zilipatikana uwandani kwa njia ya hojaji, mahojiano na majadiliano katika makundi. Mapitio ya nyaraka zilizotumika kufafanua na kujaziliza data za msingi yalipatikana kwa kutumia mbinu ya usomaji wa nyaraka zilizopo maktabani na mtandaoni. Makala hii inahitimisha kuwa kutowapa watoto majina ya lugha za jamiilugha za Tanzania kunashusha hadhi ya Watanzania, kupotea kwa utamaduni, uzalendo na utambulisho wa jamiilugha zinazohusika.

Utangulizi

Katika jamii mbalimbali duniani, mtoto anapozaliwa hupewa jina linalokuwa ni utambulisho wake. Msanjila na wenzake (2011) wanaeleza kuwa utambulisho ni jumla ya vigezo maalumu vinavyotumiwa kumtambulisha mtu, kundi la watu, jamii au taifa fulani ili kuonesha kuwa liko tofauti na taifa jingine, jamii fulani iko tofauti na jamii nyingine, kundi fulani liko tofauti na lingine au mtu fulani yuko tofauti na mtu wa kundi jingine, jamii nyingine au taifa jingine. Jina analopewa mtoto humtofautisha na watu wengine katika familia, ukoo na jamiilugha yake anamoishi. Kwa mujibu wa Gumperz (1972); Labov (1972); Hymes (1996) na Mekacha (2000) wanafasili jamiilugha kuwa ni watumiaji wa lugha wanaoishi katika eneo moja ambao hubainishwa kwa mahusiano yao ya kuendelea kutumia aina fulani ya lugha. Jina analopewa mtoto huambatana na majina ya mzazi na ukoo

ili kuwa na utambulisho imara. Hii ni kwa sababu jina moja linapotumika kuna uwezekano wa jina hilo hilo kutumiwa na mtoto mwingine hali inayofanya jina hilo kukosa utambulisho wa kipekee. Hivyo, ili kumtofautisha na watu wengine, familia nyingine, ukoo mwingine na jamiilugha nyingine hupewa jina lake linaloambatana na jina la ukoo ili kumfanya awe na utambulisho wa kipekee.

Utaratibu wa kuwapa watoto majina wanapozaliwa umekuwepo tangu enzi za ujima katika jamiilugha mbalimbali. Wakati wa enzi za ujima, majina waliyopewa watoto yalitokana na lugha za jamiilugha inayohusika. Hivyo, majina hayo yalibeba utamaduni wa jamiilugha husika. Sera ya Utamaduni ya Tanzania (1997:1) inaeleza kuwa lugha ni mojawapo ya nguzo za utamaduni ambapo nguzo nyingine ni mila na desturi, sanaa, michezo na historia ya jamii. Utamaduni ni uzoefu wa kimaisha wa watu wa jamii fulani ambao hutumia lugha moja kama njia ya mawasiliano (Jilala, 2014:2). Jilala anaendelea kueleza kuwa lugha ni kiwakilishi cha utamaduni ambacho hubeba dhana za kiisimu kama malighafi ya jamii inayohusika. Msamiati wa lugha kwa kiwango kikubwa hujenga maana za maneno kutokana na utamaduni wa jamii inamozungumzwa. Maana ya maneno hujikita katika uelewa wa utamaduni wa jamii inayotumia lugha inayohusika (Mwansoko, 1996:30). Hapana shaka kuwa majina waliyokuwa wanapewa watoto kabla ya wageni kufika nchini Tanzania yalikuwa yanaakisi utamaduni wa jamii zao.

Katika vitabu vya dini, kama vile *Biblia Takatifu,* utaratibu wa kuwapa majina watu ulianza pale Mungu alipomuumba binadamu wa kwanza ambaye alimwita Adamu. Mungu alimuumba msaidizi wake ambaye alipewa jina na Adamu ambalo ni Hawa (*Mwanzo*, 3:20). Utaratibu wa kumpa jina mtu mara anapozaliwa uliendelezwa na wazazi wa kwanza ambao ni Adamu na Hawa kwa kuwapa watoto wao majina kama vile Kaini na Habili (*Mwanzo*, 4:1-2). Tangu hapo, utaratibu wa kumpa mtoto jina anapozaliwa umerithiwa na vizazi na vizazi mpaka kizazi kilichopo sasa. Kabla ya ujio wa wakoloni nchini Tanzania lugha za asili zilitumika kwa mawasiliano miongoni mwa jamiilugha. Lugha za asili ambazo chimbuko lake ni nchini Tanzania na zinatumiwa na

makundi mbalimbali ya jamii yanayounda jamii pana ya Tanzania. Kila lugha ilitumika katika jamii inayohusika kutimiza mahitaji mbalimbali ya kimawasiliano (Mekacha, 2011). Katika kipindi hicho, majina ya watu wa jamii moja yalitofautiana na majina ya jamii nyingine kwa misingi ya lugha zilizotumika katika jamii hizo. Majina hayo yalitolewa kwa lugha ya jamii ambamo mtoto amezaliwa. Hivyo, jina alilopewa mtoto lilitokana na utamaduni wa mazingira ya jamiilugha hiyo.

Lefevere (1992) anaeleza kuwa lugha ni kielelezo cha utamaduni na maneno katika lugha hufungamana na utamaduni. Aidha, watu wa jamiilugha moja wana mtindo mmoja wa kufikiri na kuumba maana kulingana na mazingira yanayowazunguka (Ordudary, 2007). Hivyo, majina hayo hubeba maana mbalimbali ambazo kimsingi hueleweka kwa wanajamiilugha wenyewe kwa sababu wanajamiilugha hao wanachukuliwa kuwa wana maarifa, elimu na uzoefu wa maisha unaofanana. Maana za majina huwa na uhusiano na utamaduni wa mzungumzaji, mazingira ya jamiilugha ilipo, majira ya mwaka na matukio muhimu katika jamii inayohusika. Mtu anayepewa jina la jamiilugha linalotokana na jamii hiyo anabeba utambulisho wa jamii inayohusika popote anapokuwepo hata kama atakuwa nje ya mipaka ya kijiografia ya jamii hiyo. Huu ndio msingi wa Msanjila na wenzake (2011) kueleza kuwa lugha inayotumika katika majina ya jamii husaidia kubainisha utambulisho wa mtu na mahali atokapo.

Katika kipindi cha kabla ya Wakoloni majina waliyopewa watoto katika jamiilugha mbalimbali hayakutofautiana sana kutokana na ukweli kwamba lugha za asili zinashabihiana kimuundo na kimaana. Kutokana na kushabihiana huko, hata lugha zilizoonekana kuwa na hadhi kubwa kuliko nyingine hazikuziathiri lugha zilizoonekana kuwa na hadhi ndogo. Kuathiriana kwa lugha kulianza pale mwingiliano baina ya watu kutoka bara moja na lingine ulipowezekana. Uwezekano huo ulisababishwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Mwingiliano huo ukasababisha kuathiriana kwa tamaduni mbalimbali, hasa namna ya kumpa mtoto anayezaliwa jina, kuabudu, kula, namna ya kufikiri na kuyaona mambo. Baadhi ya wageni wa kwanza kufika katika pwani ya

Afrika Mashariki, hususani eneo la Tanzania kwa sasa, walikuwa ni kutoka bara la Asia (Waarabu, Wahindi na Waajemi). Wageni hao walipofika Pwani ya Afrika Mashariki, waliingiliana na wenyeji wa Pwani kama vile Wazaramo, Wandengereko, Wakwere, Wasambaa, Wazigua na Wabondei. Wageni hao kutoka bara la Asia walikuja kufanya biashara na kueneza dini ya Kiislamu.

Wageni kutoka Ulaya walifika Afrika Mashariki karne ya kumi na nane (Ogot, 1995). Wageni wa mwanzo walikuja katika makundi matatu ambayo ni wamisionari, mawakala wa Ukoloni na wanyabiashara. Mwaka 1885 baada ya mkutano wa Berlin uliofanyika Ujerumani wageni wengi walikuja Tanzania (wakati huo Tanganyika). Tanganyika ikawekwa chini ya utawala wa Mjerumani ambao ulianzisha mifumo yake ya utawala na elimu (Ogot, 1995). Baadaye, mwaka 1919 baada ya vita ya pili ya dunia Tanganyika ikawekwa chini ya udhamini wa Mwingereza ambaye alitawala mpaka Tanganyika ilipopata uhuru mwaka 1961. Muda wote wa utawala wa kikoloni Watanzania wakajikuta wanaingiliana na wageni kiasi cha kujikuta wanajinasibisha na tamaduni za kigeni hususani dini. Dini ilimtaka kila Mtanzania anayetaka kubatizwa au kusilimu kubadilisha jina, na kwa ambaye alizaliwa katika familia ya Kikristo au Kiislamu alimpa mtoto wake jina lililonasibishwa na dini yake.

Kutokana na idadi ya wageni kutoka mabara mengine kuzidi kuongezeka, Watanzania walijikuta wanazidi kujinasibisha na utamaduni wa kigeni. Aidha, maendeleo ya sayansi na teknolojia yameleta utandawazi uliorahisisha mawasiliano. Kutokana na utandawazi tamaduni za jamii mbalimbali zimesambaa duniani. Kusambaa kwa tamaduni hizo kumesababisha lugha za baadhi za jamii kuonekana ni dhaifu na nyingine kuonekana ni bora zaidi. Kutokana na athari ya mwingiliano huo, jamii zenye uchumi dhaifu zimejikuta zikiiga utamaduni wa jamii zenye uchumi imara. Tanzania ikiwa ni nchi ya dunia ya tatu imejikuta wananchi wake wanajinasibisha na jamii zenye uchumi imara kutoka Ulaya, Asia na Amerika. Lugha kama kipengele cha utamaduni, inaathiriwa sana kutokana na mwingiliano huo. Jamiilugha za Tanzania zimeachana na utaratibu wa kuwapa

watoto majina ya jamiilugha zao, badala yake wanawapa majina ya lugha za kigeni.

Mbinu na Upeo wa Mada

Tangu kuwepo kwa mwingiliano mkubwa baina ya Watanzania na wageni kutoka Ulaya, Amerika, Asia n.k., kumekuwa na tabia ya wazazi wa Kitanzania kuwapa majina ya lugha za kigeni watoto wao. Hali hii inazidi kujiimarisha kiasi kwamba imefikia hali ya jina la kwanza na la pili kuwa ya kigeni. Jina la tatu ambalo ni la ukoo, ndilo limeendelea kuwa lenye asili ya lugha za Kitanzania. Hali hii inatishia kupotea kabisa kwa majina ya jamiilugha za Kitanzania. Majina hayo yakipotea jamiilugha za Kitanzania zitakuwa zimepoteza utambulisho wake na kukili kuwa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu hazina hadhi kuliko lugha za kigeni. Hali hiyo ilimsukuma mtafiti kuchunguza majina ya lugha za kigeni wanayopewa watoto katika jamii za Tanzania. Utafiti ulifanyika mkoani Pwani katika halmashauri ya Bagamoyo. Data za msingi zilipatikana uwandani kwa watoa taarifa ambao ni wanachuo wa Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu. Mbinu zilizotumika kukusanyia data ni hojaji, mahojiano na majadiliano katika makundi. Hivyo, uwakilishi wao kwa jamiilugha za Tanzania si wa kutiliwa shaka. Makala hii inahitimisha kuwa kutowapa watoto majina ya lugha za jamiilugha zao kunashusha hadhi na kupotea kwa utambulisho wa jamiilugha zinazohusika.

Nadharia ya Makutano na Mwachano

Katika uchunguzi wa mada iliyoshughuliwa, mtafiti aliongozwa na nadharia ya Makutano na Mwachano iliyoasisiwa na Giles mwaka 1982. Nadharia hiyo, inapima mshikamano walionao wanajamiilugha kuhusu utamaduni wao na lugha yao kama mbinu ya kupima nguvu ya utambulisho wa jamiilugha. Inapofikia wanajamiilugha wa lugha fulani kukubali kuacha kutumia lugha yao na kuanza kutumia lugha ya jamiilugha nyingine, hapo kuna makutano kwa jamiilugha mbili. Hii ni kwa sababu jamiilugha mbili ambazo zimeingiliana kieneo zinaendelea kutumia lugha moja inayodumishwa na kutumiwa kwa utambulisho wa jamiilugha hiyo pana. Endapo inatokea jamiilugha mbili zimeingiliana kieneo, lakini kila moja ikaendelea kutumia na kudumisha lugha yake,

basi kuna mwachano wa jamiilugha hizo mbili. Mwachano huo unaashiria kuwa kila jamiilugha inathamini na inaendeleza utambulisho wake kwa kutumia lugha yake.

Mazingira ya makutano yanatokea kwa jamiilugha mbili zenye nguvu tofauti, yaani jamilugha dhaifu na jamiilugha bora; jamiilugha dhaifu inakubali kutumia lugha ya jamiilugha bora. Hali hiyo inaonesha kuwa yenyewe haithamini lugha yake na utamaduni wake kwa ujumla. Wanajamiilugha dhaifu huiga utamaduni wa jamiilugha bora ili wakubalike na jamiilugha bora wanalazimika kutumia lugha ya jamii hiyo bora na yenye nguvu. Kuendelea kutumia lugha za kigeni za nchi zilizoendelea katika mataifa yetu ya Afrika ni kudhoofisha utambulisho wa Mwafrika (Mulokozi, 2000). Mazingira ya mwachano yanatokea kwa jamiilugha mbili au zaidi zenye ubora na nguvu sawa. Katika hali hiyo, kila jamiilugha inajiona ni bora na yenye nguvu hivyo inathamini lugha yake na utamaduni wake. Utambulisho wa kila jamii unakuwa na nguvu kwa sababu amali za jamiilugha zinalindwa na kudumishwa na wanajamiilugha wenyewe kwa kila mmoja kutumia lugha yake ya asili.

Giles na Byrne (1982) wakifafanua zaidi nadharia hiyo, wanaeleza sababu mbalimbali zinazomfanya mzungumzaji wa jamiilugha fulani kuamua kutumia lugha ya jamiilugha nyingine katika kujitambulisha. Sababu hizo ni kama vile utambulisho wa jamiilugha ya mzungumzaji kuwa dhaifu na lugha ya jamii kuonekana haina umuhimu kwa watumiaji wake; mzungumzaji kutoamini kwamba mahusiano baina ya jamiilugha mbili zinazoingiliana yanaweza kuwa na manufaa kwa jamiilugha yake na mzungumzaji kuiona jamiilugha yake kuwa ni jamii dhaifu isiyokuwa na maendeleo kwa wanajamiilugha wake na mzungumzaji kuiona jamiilugha yake kuwa haina thamani kwa lolote. Mzungumzaji hulazimika kujitambulisha kwa jamiilugha yake kuhusu masuala ya ndani tu, lakini kwa masuala ya maendeleo, elimu na uchumi hujitambulisha kwa kutumia lugha ya jamiilugha nyingine yenye nguvu kwa lengo la kunufaika kijamii na kiuchumi. Misingi ya nadharia hii imetumika kufafanua mtazamo wa jamiilugha za Tanzania kuhusu lugha zao. Misingi hiyo imesaidia kuchambua na kuelezea

sababu zinazosababisha wanajamii kutokuwapa watoto majina ya lugha zao; na athari zake kwa jamii za Tanzania.

Sababu za Jamii za Kitanzania Kuwapa Watoto Majina ya Lugha za Kigeni

Kulingana na mila na desturi za jamii mbalimbali ni suala la kawaida mtoto anapozaliwa kupewa jina linalokuwa utambulisho wake na jamii yake. Kimsingi, jina analopewa mtoto linakuwa na maana kwa sababu ni sehemu ya lugha ingawa si wazazi wote wanaojua maana ya majina wanayowapa watoto wao. Rubanza (2000) anaeleza kuwa majina ya watu wa Kihaya yana maana kama ilivyo kwa majina ya lugha nyingine za Kiafrika. Kila familia inakuwa na sababu za kuchagua jina la kumpa mtoto anayezaliwa. Sababu mojawapo ni kuamini kuwa majina yana baraka. Imani yao ni kwamba kuna majina ambayo yana uhusiano wa moja kwa moja na baraka. Hii ina maana kwamba mtoto anayepewa jina linalosadikiwa kuwa na uhusiano na baraka, basi mtoto huyo atakuwa na baraka. Kutokana na imani hiyo, wanaona kuwa majina ya lugha za kigeni yana baraka tofauti na majina ya lugha za Kitanzania. Mfano wa majina yaliyotajwa na watoataarifa kuwa yana baraka ni Abillah, Glory, Hope, Jaqueline, Catheline, Irene, Bress, Nataria, Prisca, Brenda, Winner na Grace. Baraka hizo ni kama vile kumcha Mungu, kufanikiwa katika mambo mbalimbali, kuwa na akili nyingi, busara na hekima.

Dhana ya kuamini majina hayo kuwa na baraka ndiyo inayowafanya wasiwape watoto wao majina ya lugha za Kitanzania ambayo wanadai kuwa hayana baraka. Majina hayo yanafungamanishwa zaidi na imani za kidini, hasa za Kiislamu na Kikristo. Wanaamini kuwa majina ya Kizungu na Kiarabu yana uhusiano wa moja kwa moja na Mwenyezi Mungu. Pia, wanaamini kuwa watoto wakipewa majina hayo wanapata baraka moja kwa moja. Jambo hilo ni kasumba tu kwa sababu majina ya lugha za jamii zao yana maana sawa na majina ya lugha za kigeni. Pamoja na majina ya lugha zao kuwa na aana sawa na majina kutoka katika lugha za kigeni bado wanaona hayana thamani sawa. Jina la lugha ya kigeni linatazamwa kuwa na baraka zaidi likilinganishwa na jina la lugha ya Kitanzania. Maelezo haya yanadhihirika katika majina yafuatayo:

Majina Kutoka Lugha ya Kiingereza na Lugha za Jamiilugha za Tanzania

Jina la Lugha za Kigeni	Jina la Lugha za Jamiilugha za Tanzania						
Kiingereza	Kiswahili	Kinyakyusa	Kisukuma	Kihaya	Kinyamwezi	Kiha	Kipare
Bless	Bariki	Saja	Kudosha	Goshooka	Akujiwe	Hezagira	Lughenjo
Grace	Neema	Ipyana	Lubhango	Eneema	Lubango	Ikigongwe	Mbonea
Groly	Utukufu	Lwimiko	Bhukuji	Atugonza	Ndagatifuja	Ubwera	Ngazo
Winner	Mshindi	Ntoli	Bhutindi	Kusinga	Ntindi	Inchinzi	Kurota
Love	Upendo	Lugano	Bhutogwa	Kwangalanyo	Lwendo	Ulukundo	Lukundo
Peace	Amani	Lutengano	Mhola	Emile	Mhola	Amahoro	Mporer

				mbe			e
Happy	Furaha	*Lusekelo*	*Bhuyegi*	*Kushe melelw a*	*Lukelo*	*Ishimwe*	*Zihirwa*

Chanzo: Uwandani (Julai, 2019)

Mifano iliyotolewa hapa, inaonesha kuwa Watanzania wana majina yenye maana sawa na ya lugha za kigeni. Hata hivyo, watu hawawapi watoto wao majina ya kwao badala yake wanawapa majina ya lugha za kigeni wakidhani wakitumia majina ya lugha hizo, watoto wao watakuwa na baraka zaidi. Majina ya lugha za kigeni yanapewa uzito na yanaonwa kuwa yana uhusiano wa moja kwa moja na baraka kutoka kwa Mungu kama ilivyokwishaelezwa. Sababu hii ni kinyume na utaratibu uliotumika kuwapa majina watoto kabla ya ujio wa wageni kutoka nje ya Tanzania hususani Asia na Ulaya. Kabla ya ujio wa wageni, majina yalichaguliwa kwa kuzingatia hali ya wakati wa kuzaliwa mtoto, ugomvi na misuguano ya kifamilia (Rubanza, 2000). Watoto walipewa majina kwa kuzingatia mpangilio wa kuzaliwa, siku aliyozaliwa, msingi wa imani na shukurani kwa Mungu. Majina ya bibi au babu yanayoonesha uhusiano baina ya wazazi na jamii, majina ya vitu, matarajio ya wazazi kwa mtoto na mahali alipozaliwa (Buberwa, 2016).

Watanzania wanawapa watoto majina ya lugha za kigeni kwa kuamini kuwa majina ya watu wenye tabia nzuri na maarufu katika jamii yatasaidia watoto wao pia kuwa na tabia nzuri na kujipatia umaarufu. Sababu hii inatokana na imani kuwa kuna uhusiano wa moja kwa moja wa jina analopewa mtoto na tabia atakayokuwa nayo. Majina yanayohusishwa na tabia nzuri na umaarufu ni ya lugha za kigeni. Watoataarifa walitaja majina kama vile Jacqueline, Brian, Brenda, Clara, Beyonce, Nataria, Hellen na Matrider kuwa yana uhusiano na tabia nzuri na umaarufu. Majina mengi yanatoka katika lugha za Kiingereza, Kiarabu, Kireno, Kifaransa, Kihispaniola, Kilatini, na Kiebrania. Hali hii inaonesha dhahiri kuwa Watanzania wana mtazamo hasi kwa lugha zao pamoja na utu wao wenyewe. Kuendelea kuwapa watoto majina ya lugha za kigeni katika nchi za Afrika ni kudhoofisha utambulisho wa Mwafrika.

Watu wengine katika jamiilugha za Tanzania wanadai kuwa majina ya lugha za kigeni yanasikika na kutamkika vizuri ndiyo maana wanawapa watoto wao. Watu wenye mtazamo huu wanaona majina ya lugha za jamiilugha za Tanzania hayasikiki na kutamkika vizuri, hivyo

yanawakera masikioni wanapoyasikia na midomoni wanapoyatamka. Hiyo ni hali waliyojijengea kwenye akili zao kwamba kuna maneno hususani ya lugha za jamiilugha za Tanzania hayasikiki na kutamkika vizuri. Aidha, fikira hizo ni kasumba waliyoachiwa na wageni kutoka mabara mengine. Wengi wao wanaoona hivyo, hawajui hata maana ya majina yao na waliyowapa watoto wao. Watu, hususani vijana, hawajui maana ya majina yao na wazazi wengi wanawapa watoto wao majina ya lugha za kigeni bila hata kujua maana za majina hayo.

Sababu za Wazazi Kutowapa Watoto Majina ya Lugha za Jamiilugha za Tanzania

Watoto kutoka jamiilugha za Tanzania hawapewi majina ya jamii zao kwa sababu hayakubaliki katika dini za Kikristo au Kiislamu. Hali hii inatokea wakati mtoto anapobatizwa, viongozi wa dini wanayakataa majina ya Kiafrika na kuyakubali yale ya Kizungu au Kiarabu. Huu ni mwendelezo wa yaliyokuwa yanafanywa na Wamisionari wa mwanzo baada ya kuingia Tanzania ambao waliwalazimisha Watanzania kubadilisha jina au kupewa jina jingine. Kutokana na msimamo huo wa viongozi wa dini, watoto katika baadhi ya jamii za Tanzania wanapewa majina mawili. Jina moja ni la lugha ya kigeni ambalo linatumika kumtambulisha kanisani, shuleni na katika shughuli rasmi. Jina la pili ni la lugha ya jamiilugha ya Tanzania ambalo mawanda yake ya kutumika ni nyumbani na kwenye shughuli za kimila na kidesturi tu. Utaratibu huo unakubaliana na Giles na Byrne (1982) wanapoeleza sababu za mwanajamiilugha fulani kuamua kutumia utambulisho wa lugha ya jamii nyingine wanafafanua kuwa mzungumzaji hujitambulisha kwa jamiilugha yake kwa yale masuala ya ndani tu, lakini kwa masuala ya maendeleo, elimu na uchumi hujitambulisha kwa jamiilugha nyingine yenye nguvu ili kunufaika kijamii na kiuchumi.

Wazazi walio wengi hawawapi watoto wao majina ya lugha za Jamiilugha za Tanzania kutokana na kuamini kuwa majina hayo yanamweka mtoto mbali na Mungu. Hoja hii ni mwendelezo wa imani ambayo Watanzania wameaminishwa kuwa kuna baadhi ya majina yana uhusiano wa moja kwa moja na Mungu na mengine hayana

uhusiano huo. Katika mtazamo huu, majina ya Kitanzania yanatazamwa kama hayana uhusiano na Mungu, bali yanahusiana na miungu. Msimamo huuunashikiliwa na watu wenye imani kali za kidini. Vilevile, majina ambayo yana historia ya matukio mabaya au changamoto wakati mtoto anazaliwa au mama alipokuwa mjamzito yanaonwa kuwa hayafai kwa sababu kwa Mungu hakuna shida bali ni raha tu. Majina kama vile Chausiku, Majuto, Masumbuko, Mashaka, Matonya, Shida, Tabu, n.k., yamebeba historia ya matukio ya wakati mtoto alipozaliwa au kuonesha jinsi alivyopatikana. Watu wa mabara mengine wana utamaduni wao ambao unaambatana na majina hayo. Hivyo, kitendo cha Watanzania kuyakumbatia majina ya lugha za kigeni ni kukumbatia utamaduni wa kigeni na kutunza historia ya matukio yasiyowahusu.

Baadhi ya Watanzania wanaona majina ya lugha za jamiilugha za Tanzania hayana mvuto na hayaendi na usasa. Mtazamo huu unatetewa na watu wanaoona kutumia vitu na lugha za kigeni ndio usasa. Wengi wao, usasa wanaouona ni ule wa kutumia vitu vinavyotumiwa na watu kutoka katika mabara mengine, zikiwemo lugha za kigeni. Kwao kujiita jina analoitwa mwigizaji, mwimbaji, mchezaji wa mpira, mhubiri au raisi wa nchi za Ulaya, Amerika au Asia ndio usasa. Hivyo, wanaona kumpa mtoto jina ambalo halitumiwi na watu wenye sifa zilizotajwa hapa itakuwa sawa na kuukosa usasa na jina linakosa mvuto.

Athari za Watanzania Kutowapa Watoto Majina ya Lugha za Jamiilugha Zao

Jamii yoyote inapoacha kuwapa watoto majina ya lugha yao ni sawa na jamii hiyo kuacha kutumia lugha yake. Msanjila (2011) anaeleza kuwa lugha ni mojawapo ya amali za jamii na ndio msingi wa mtu au jamii kutetea na kusisitiza dhana ya sisi zaidi kuliko wao. Majina ni sehemu ya lugha na lugha ndiyo yenye kuitambulisha jamii, pamoja na amali zake. Kutowapa watoto majina ya jamiilugha za Tanzania kunasababisha kushuka hadhi kwa Watanzania. Hadhi inayozungumziwa hapa ni kwamba Watanzania hawatathamini lugha yao na utamaduni wao kwa ujumla. Giles na Byrne (1982) wanaeleza kuwa wanajamiilugha wa jamii dhaifu huiga utamaduni wa jamiilugha

bora; ili wakubalike na jamii bora wanalazimika kutumia lugha ya jamii bora na yenye nguvu. Hivyo, Watanzania kutowapa watoto majina ya lugha zao ni kukubali kuwa wao ni dhaifu na utamaduni wao haufai, kwa hiyo wanajikabidhi kwa jamii bora na yenye nguvu. Hali hii ikiendelea kushamiri, itasababisha wanajamii kukosa uzalendo kwa jamii yao, umoja na mshikamano na kujiamini kutatoweka. Msanjila (2011) anaeleza kuwa utambulisho ni ule mshikamano wa dhati wa jamiilugha ambao husaidia kujenga taifa lenye umoja.

Watanzania wakiendelea kutumia majina ya kigeni watapoteza utamaduni wao uliozoeleka kwa vile watajikuta ni wageni katika ardhi yao. Kwa kawaida, katika jamii za Tanzania kumpa mtoto jina ni tukio la kifamilia linaloambatana na mila na desturi. Siku hizi wazazi wanapompa mtoto jina hawazingatii taratibu za jamii za Tanzania, bali wanakimbilia kutafuta majina kwenye mitandao. Mtandaoni wanapata majina ya lugha za kigeni ambayo hayafungamani kwa vyovyote na utamaduni wa jamii yake, pamoja na mazingira yake. Hali hii ni sawa na kumtenga mtoto na jamii yake. Kuendelea kuwapa watoto wa Kitanzania majina ya lugha za kigeni kutazalisha kizazi ambacho hakitaweza kuthamini utamaduni wake. Mtoto atakuwa tayari kujinasibisha na watu wenye jina hilo ambao wako kwenye mazingira tofauti na anayoishi. Wajibu wa mwanajamii ni kuhamasika kukuza na kuitumia lugha yao ili iweze kuelezea amali za jamiilugha yao, mielekeo yao na makundi yao na jinsi lugha inavyotofautiana na lugha nyingine (Giles na Byrne, 1982). Haya hayawezi kutekelezeka kama watoto wataona majina yao hayahusiani na lugha yao; wataiona lugha yao haijitoshelezi, ni dhaifu na hakuna sababu ya kuitumia, kuitetea na kuikuza.

Majina ya watu ni sehemu ya lugha na kipengele muhimu sana katika utambulisho kwa sababu maneno yatumikayo kama majina hutokana na lugha husika. Tabouret-Keller na Le Page (1986) wanaeleza kuwa matamshi ya mzungumzaji yeyote ni matamshi ya utambulisho wake. Hii ina maana kuwa jamiilugha ambayo inawapa watoto wao majina ya lugha za kigeni watatamka majina hayo na matamshi yao yataitambulisha jamiilugha ambayo jina la mtoto ndio asili yake.

Majina kama sehemu ya utambulisho hayana budi kuendelezwa kwa kila jamii. Jamii ambayo inayojitambua, inapambana kuhakikisha utambulisho wake unaendelezwa. Endapo jamiilugha za Tanzania hazitaendeleza utamaduni wa kuwapa watoto majina ya lugha zake, utambulisho wa jamii hizo utafifia na hatimaye kutoweka kabisa. Hii ni kwa sababu jina linamtambulisha mtu kuwa ni mwanajamiilugha gani, anatoka wapi, utamaduni wake ni upi n.k. Msanjila (2011) anaeleza kuwa:

> *"Mzungumzaji anapofikia hatua ya kusema hadharani kwamba sisi huwa hatufanyi hivyo, sisi asili yetu ni mahali A, au anaposema lugha yetu sisi ni B, chakula chetu sisi ni C, kimsingi mzungumzaji huyo anadhihirisha mfungamano uliopo baina yake na jamiilugha yake na huo ndio utambulisho wake.Utambulisho ni kwa wanajamiilugha wenyewe kuthamini lugha yao pamoja na vibainishi vingine vya msingi vinavyowafanya wajione wako tofauti na jamiilugha nyingine".*

Kwa sasa nchini Tanzania kuna watoto wengi ambao jina la kwanza na jina la pili sio majina ya jamiilugha za Tanzania na wachache majina yote matatu si ya jamiilugha za Tanzania. Kwa mfano:

Majina ya Watoto wa Kitanzania

Na.	Lugha ya Kigeni	Lugha ya Kigeni	Lugha ya Kitanzania	Jamiilugha yake
i	*Mohamedi*	*Ally*	*Mtumbuka*	*Mmatumbi*
ii	*Glory*	*Derrick*	*Machange*	*Mchaga*
iii	*Catheline*	*Aloyce*	*Amlima*	*Mmakua*
iv	*Nataria*	*Richard*	*Mfungo*	*Mjita*
	Lugha ya Kigeni	*Lugha ya Kigeni*	*Lugha ya kigeni*	
v	*Jaqueline*	*Petro*	*Samwel*	*Msafwa*

Chanzo: Uwandani (Julai, 2019)

Katika data hii, majina ya watoto kuanzia i-iv, kila mmoja, jina la kwanza na la pili sio majina ya lugha za jamiilugha za Tanzania. Ukiyasikia majina hayo huwezi kutambua kuwa anayetajwa ni mtu wa jamiilugha za Tanzania. Watoto wenye majina hayo utawanasibisha na jamiilugha zao utakaposikia jina la tatu. Jina lililopo katika v hali ni mbaya zaidi kwa sababu majina yote ni zao la lugha za kigeni. Hivyo, ni vigumu kumtambua kama anatoka katika jamiilugha ya Kisafwa ambayo ni mojawapo ya jamiilugha za Tanzania. Kwa namna hali ilivyo, utambulisho wa jamii upo hatarini kupotea endapo hakuna juhudi za makusudi kudhibiti hali hii. Msanjila (2011) anaeleza kuwa kama wazungumzji wa jamiilugha fulani hawatakuwa tayari kudumisha utamaduni wao na lugha yao ya asili, iliyobeba amali za jamii yao, kuna kila dalili kuwa utambulisho wa jamillugha hiyo unaweza kupotea. Ili kulinda na kudumisha tamaduni zao, nchi nyingi zilizoendelea zina vyombo maalumu vya kisheria vinavyosimamia majina wanayopewa watoto kama ilivyo katika nchi za China, Japan, Finland, Denmark na Ujerumani. Vyombo hivyo huhakikisha jina analopewa mtoto linahusiana na lugha za nchi zinazohusika.

Kutowapa watoto wa Kitanzania majina ya jamiilugha za Tanzania kutasababisha Watanzania kupoteza uzalendo na umoja. Watoto wenye majina ambayo hayana unasaba na lugha za jamiilugha za Tanzania wanajiona wao ni tofauti na wale wenye majina ya lugha za jamiilugha za Tanzania. Mara nyingi wenye majina ya lugha za kigeni wanajiona kuwa wana majina mazuri na yenye mvuto kuliko wenye majina ya lugha za jamiilugha za Tanzania. Hali hiyo, huwafanya wenye majina ya lugha za kigeni kuwa sio Watanzania au hawastahili kuishi Tanzania, bali wanastahili kuwa katika nchi zinazozungumza lugha za majina yao. Kutokana na watoto kuwa na majina yenye asili tofauti, utani huzuka baina ya watu ambao wakati mwingine husababisha ugomvi. Kwa ujumla, kila kundi huona kundi lingine sio kama wao.

Hitimisho na Mapendekezo
Makala hii kwa ujumla imechunguza majina ya lugha za kigeni wanayopewa watoto katika jamiilugha za Tanzania. Makala imebainisha kuwa sababu zinazowafanya wanajamiilugha za Tanzania

kuwapa majina ya lugha za Kitanzania ni kuamini kuwa majina ya lugha za kigeni yana baraka, uhusiano na tabia nzuri, umaarufu na kusikika vizuri. Aidha, makala hii imebainisha sababu za kutowapa majina ya jamiilugha za Tanzania ni kutokubalika kidini, na kukosa mvuto. Mwisho, makala hii imebaini kuwa kutowapa watoto majina ya lugha za jamiilugha za Tanzania kunashusha hadhi ya Watanzania, kupotea kwa utamaduni, uzalendo na utambulisho wa jamiilugha zinazohusika.

Makala hii inapendekeza kuwa elimu itolewe kwa Watanzania kuhusu umuhimu wa kuendeleza na kuyatumia majina ya lugha za jamiilugha za Tanzania. Vilevile, serikali ianzishe chombo maalumu cha kusimamia majina wanayopewa watoto wa Tanzania. Mwisho, tafiti zaidi zifanyike kuhusu majina ya kigeni kutumika katika maduka, hoteli, vilabu vya michezo mbalimbali, nyumba za ibada, vyombo vya habari, shule, vinyozi, baa na vyama vya siasa. Maeneo hayo ni muhimu sana kufanyiwa uchunguzi kwa sababu Watanzania wengi watapata uelewa kuhusu majina wanayowapa watoto wao endapo maeneo hayo yatafanyiwa uchunguzi wa kina.

Marejeleo

Bibble Society of Tanzania, (1997). *Biblia Takatifu*. Dodoma: Bibble Society of Tanzania Publishers.

Buberwa, A. (2016). Kiswahili Personal Names Selection in Tanzania: A Social Analysis. *Journal for Studies in Humanities and Social Science*, 1(2), 111 - 120.

Giles, H. (1979). 'Ethnicity Markers in Speech'. In K. R. Scheres and H. Giles (eds.), *Social Markers in Speech*, 251- 289. London: Cambridge University Press.

Giles, H., & Byrne, J. L. (1982). 'An Intergroup Approach to Second Language Acquisition'. In *Journal of Multilingual and Multicultural Development*, 3, 17 - 40. No. 19.

Gumperz, J. (1972). 'Introduction'. In J.J. Gumperz and D. Hymes (eds.) Directions in Sociolinguistics: The Ethnography of Communication. New York: Holt, Rinchart and Wiston, Inc.

Hymes, D. (1972). 'Models of Interaction of Language and Social Life'. In J. J. Gumperz and G. Hymes (eds.) *Directions in Sociolinguistics: The Ethnography of Communication*. New York: Holt, Rinchart amd Wiston, inc.

Jilala, H. (2014). 'Athari za Kiutamaduni katika Tafsiri: Mifano kutoka Matini za Kitalii Makumbusho za Tanzania'. Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Labov, W. (1972). *Language in the Inner City*. Philadelphia: Pennsylvania University Press.

Lefevere, A. (1992). *Translating Literature: Practice and Theory in Comperative Literature Context.* 26 Broadway New York. The Modern Language Association of America.

Mekacha, R. D. K. (2000). *Isimujamii: Nadharia na Muktadha wa Kiswahili:* Osaka University of Foreign Studies.

Msanjila, Y. P., Kihore, Y. M., & Massamba, D. P. B. (2011). *Isimujamii: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam, TUKI.

Mwansoko, H. J. M. (1996). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu.* Dar es Salaam. TUKI.

Ordudary, M. (2007). Translation Procedures Strategies and Methods. Katika *Translation Journal*.

Ogot, B. A. (1995). 'Africa From the Twelfth to the Sixteenth Century', katika J. F. ADE AJAYI. Heinemann Educational Publishers, Halley Court Jordan Hill, Oxford OX2 8EJ.

Rubanza, Y. I. (2000). 'The Linguistic Creativity of Haya Personal Names'. *Jarida la Kiswahili*. 63, 11 - 22.

Tabouret-Keller, A., & Le Page R. B (1986). The Mother-Tongue Metaphor. In Grazer Linguistische Studien, 27: 249-259.

Methali za Kiswahili Hukwepa Ukiushi wa Kaida za Lugha?

Yangson Patrick Mgogo
Idara ya Usimamizi wa Elimu, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dodoma
Baruapepe: *tl20032007@gmail.com*

Ikisiri

Makala hii inalenga kuchunguza suala la ukiushi wa kaida za lugha katika methali za Kiswahili. Ili kuweka bayana wazo hili, zimeteuliwa baadhi ya methali na kuzifanyia uchunguzi. Mkazo umewekwa kwa kuangazia msamiati uliotumika katika methali bila kutumia tafsida au lugha fiche kulingana na kaida zilizozoeleka katika jamii za Tanzania na Afrika kwa ujumla. Aidha, methali kama chombo cha kimaadili na kiutamaduni kwa nini zinatumia lugha isiyoheshimu kaida za jamii? Data za makala hii zilipatikana katika kamusi ya Methali za Kiswahili iliyoandikwa na Mkota (2009). Mbinu ya uteuzi wa kimakusidi ilitumika ili kupata methali hizo. Msamiati wa vitenzi na nomino zisizotakiwa kutamkwa hadharani katika jamii ulituongoza kubaini methali hizo. Nadharia za Semiotiki na Usosholojia zilitumika katika uchambuzi, uhakiki na mjadala wa methali zilizolengwa. Kwa ujumla, makala hii inahitimisha kwamba methali zilizojadiliwa utunzi wake uliegemea zaidi katika kipengele cha maudhui na kusahau kuweka uwiano sawa katika kipengele cha fani ili kuendana na kaida za lugha.

Utangulizi

Methali ni kipengele cha fasihi katika utanzu wa semi ambacho huchunguzwa katika taaluma ya Paremiolojia. Kwa mujibu wa Gaichu (2016) akimnukuu Dabaghi (2012) anasema kuwa Archor Taylor ni miongoni mwa waanzilishi wa taaluma ya Paremiolojia ambayo imejikita katika uchunguzi na ufafanuzi wa kipengele cha methali. Methali inaweza kufafanuliwa kuwa ni msemo unaojitosheleza, wenye maana yenye nguvu, muundo au sifa za kishairi unaokusudiwa kuielimisha jamii (Wamitila, 2001). Methali zinaweza kutazamwa kama sanaa yenye sifa kibalagha au chuku inayotumika kama mbinu ya kuongeza sifa mahususi ya kitu (Mkota, 2009). Sifa hiyo inaweza kubeba dhana ya ubaya au uzuri.

Methali zina sifa nyingi, miongoni mwake ni sifa ya paradoksia ambayo huonesha hali ya ukinzani katika methali zinapotazamwa kimantiki ingawa zikichunguzwa kwa undani huleta maana fulani. Pia, zina uwezo wa kisitiari na kitashibiha ambao huonesha ulinganifu wa vitu kwa kutumia na kutotumia viunganishi. Kwa ujumla, methali ni semi zenye maelezo mafupi sana lakini zinapofafanuliwa hubeba ujumbe mzito kwa ajili ya mafundisho ya kijamii. Jamii za Kiafrika huzitazama methali kama taasisi muhimu inayobeba uwanja mpana wa maarifa ya binadamu wote bila kujali matabaka, umri na jinsi. Methali ni sanaa ya malezi kwa wanajamii katika nyanja zote za maisha kwa kuwa unahimiza ushirikiano, unaadilisha, unatia moyo na unaendeleza mila na desturi za jamii inayohusika.

Hapana shaka kuwa lugha ni mali ya binadamu na matumizi yake hutawaliwa na utamaduni wa wazungumzaji wa jamiilugha inayohusika. Jamiilugha hutambua neno gani litumike na kuepukwa katika muktadha fulani. Katika baadhi ya methali kuna matumizi ya maneno ambayo hurejelea viungo vya siri katika mwili wa binadamu. Isitoshe, methali zina vitenzi vinavyotaja matendo ya faragha yanayofanywa na wanadamu katika mazingira mahususi. Kwa mfano,'*Usiige kunya kwa tembo utapasuka mkundu'*. Umbo la nje la methali hiyo linaundwa na kitenzi 'kunya' pamoja na nomino 'mkundu'. Hoja yetu inajikita katika kuangazia uhalali wa kutamka maneno "kunya" na "mkundu". Je, maneno kama haya yanapotamkwa hadharani ni staha njema kwa wanajamiilugha, hasa ukirejelea muktadha mpana wa jamii za Afrika Mashariki?

Mwanaisimu Sapir na Whorf (1956) wanaeleza kuwa lugha huathiri na kudhibiti jinsi wazungumzaji na watumiaji wa lugha wa jamii fulani wanavyoufasili ulimwengu wao. Kulingana na wanaisimu hao, muundo wa maana katika lugha ndiyo msingi wa fikira za mwanadamu. Akieleza nafasi ya lugha katika jamii, King'ei (2010) anaeleza kuwa lugha ni zao la jamii na ni kipengele muhimu sana cha utamaduni wa jamii inayohusika. Hivyo, lugha hutumika kurithisha mila na desturi za jamii ikiwa ni pamoja na kutolea elimu. Binadamu huweza kufunzwa na kupewa maadili mbalimbali kwa kutumia lugha ili aweze

kujitambua. Mbali ya kuwa lugha hutumiwa katika kuleta mawasiliano baina yao pia ni nyenzo ya ujenzi na uhifadhi wa maadili kwa jamii.

Suala la lugha lina nafasi kubwa katika kujenga na kuimarisha utamaduni wa jamii. Kipengele cha utamaduni kina upana wake kwa kuwa hubeba vitu vingi ndani yake ambavyo hutokana na shughuli wanazozifanya wanadamu kila siku. Utamaduni hujidhihirisha vema katika lugha, matendo na katika vipengele mbalimbali vinavyogusa maisha ya kila siku ya binadamu kama vile nyimbo, ngoma, mavazi, fasihi, mila, semi na desturi. Uwasilishwaji na uhifadhi wa vipengele hivyo, msingi wake ni lugha. Kwa hiyo, lugha inayotumika ni lazima izingatie kanuni na taratibu za watumiaji ili kuepuka upotoshaji wa maadili. Vivyo hivyo, methali ni kipengele kimojawapo katika utanzu wa semi ambacho hakiwezi kukwepa kuingizwa katika mkululu huo. Kwa hiyo, makala hii imechunguza methali za Kiswahili zinazokwepa uzingativu wa kaida za lugha katika jamii.

Mbinu na Mawanda ya Uchunguzi
Katika taaluma ya fasihi na lugha, wataalamu wengi kama vile Othman (1997), Hoja (2004), Mbonde (2005), Mahenge (2009), Hassan (2010) na Mturo (2011) wamefanya uchunguzi katika methali za Kiswahili kwa misukumo na mitazamo mbalimbali. Licha ya kuwapo kwa jitihada za kiuchunguzi zilizokwishafanywa na wanazuoni hao, kwa kadiri ya ufahamu wetu, hakuna uchunguziulioshughulikia kipengele cha matumizi ya methali zinazokiuka kaida zilizozoeleka katika jamii ya Waswahili na sababu zake. Hivyo, makala hii imeshughulikia suala hilo kwa kuchunguza methali zinazokiuka kaida za lugha zilizozoeleka katika jamii za Tanzania. Mbinu ya uchunguzi wa kimaktaba ilitumika kupata data zilizotumika katika makala hii. Data zilipatikana katika kamusi ya Methali za Kiswahili ya Mkota (2009). Data za upili zilikusanywa kwa mbinu ya kinyaraka ili kurejelea na kujaziliza data za msingi zilizolengwa. Mbinu ya kimakusudi ilitumika kupata methali zilizolengwa. Uchambuzi na mjadala wa data uliongozwa na nadharia za Simiotiki na Usosholojia.

Nadharia Zilizotumika katika Uchunguzi

Nadharia ya Usosholojia iliasisiwa na Hippolyte Taine (Mfaransa). Kihistoria, nadharia hii ilianza kujitokeza katikati ya karne ya 19 na kushamiri katika karne ya 20 barani Ulaya (Taine, 1863). Nadharia hii ilizitazama kazi za kifasihi kama nakala ya tabia na kiwakilishi halisi cha jamii fulani (Shorter, 1969 &Njogu na Chimerah, 1999). Pia, huyatazama mazingira ya asili ya jamii kuwa ndio huamua namna kazi ya kifasihi inavyotakiwa kuwa. Fasihi ni usawiri mkamilifu ambao hayasawiri maisha kwa undani na huyachunguza kwa mtazamo mpana (Silbermann, 1963; Scott, 1974; Narizvi, 1982 & Sarup, 1989). Kwa hiyo, methali zilitazamwa kama zao mahususi la jamii ya Waswahili iliyochunguzwa kwa kuzingatia vipengele vya kitamaduni vinavyoibuka kupitia katika historia yao, falsafa yao, mila na desturi zao, uchumi wao na siasa zao.

Nadharia ya Semiotiki iliasisiwa na mwanaisimu wa Ki-Swizi, Ferdinand de Saussure, pamoja Charles Pierce mwanafalsafa wa Ki-Marekani (Nazarova, 1996). Semiotiki ni taaluma ya kisayansi inayojishughulisha na uchunguzi wa ishara kwa kuzingatia zaidi kiwakilishi na kiwakilishwa (Massamba, 2004). Hadhira hutengeneza maana mbalimbali kupitia ubunifu na tafsiri zao kuhusu alama hizo. Binadamu ndiye mtengenezaji na mnyambulishaji wa ishara zinazotumika katika kazi za kifasihi (Culler, 1981; Chandler, 1992 & Barthes, 1994). Watunzi wa kazi za fasihi hutumia lugha ya picha na ishara kurejelea matendo na tabia za mwanadamu ili kuwafunza wanajamii masuala mbalimbali kulingana na mahitaji ya jamii yao.

Msimbo wa kirejelezi ulituongoza kwani msingi wake hujengwa na viashiria vya kiutamaduni vinavyorejelewa katika kazi inayohusika. Msingi wa jambo hilo ni kwamba wasanii wa kazi za fasihi huchota dhamira zao kulingana na matakwa, ada na tajiriba za mazingira yaliyowalea na kuwakuza (Macherey, 1978; Solomon, 1988 & Wamitila, 2002). Urejelezi huo ndio unaounda uhalisi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka kwa hadhira. Msimbo huo umetumika kwa msingi wa kuwapo kwa maneno mengi ya kiutamaduni katika methali za Waswahili. Maneno hayo hutumika kurejelea masuala

ambayo yanahitaji ufafanuzi na uchambuzi wa kina. Maneno ya kiutamaduni yaliyotumiwa na wasanii katika methali zao tuliyatafakari kwa undani katika makala hii. Ufafanuzi wa kina wa maneno ya kiutamaduni yaliyotumika ulifanyika ili kubaini dhamira zilizomo na manufaa yake kwa jamii iliyochunguzwa.

Kaida za Lugha, Ukiushi na Mawasiliano

Katika taaluma ya fasihi, wasanii huitumia lugha kama nyenzo muhimu na ya pekee katika ujenzi wa sanaa hiyo. Wasanii hufanyakazi kubwa ya kufinyanga na kuipamba lugha ili ilete mvuto kwa hadhira. Lugha hutumika kama mbeleko inayobeba ujumbe uliomo katika fikra zao. Mohammed (1981) anaeleza kuwa lugha hubadilika na kufuata tabia, kanuni na kaida fulani kutegemea muktadha wa matumizi. Kwa hali hii, lugha ya maelezo ya kisayansi itatofautiana na lugha ya kifasihi kwa sababu malengo na madhumuni ya mawasiliano, fikira na matumizi ya lugha katika kuwasilisha fikra hizo hutofautiana.Kazi ya fasihi haiwezi kuvutia, kufikisha ujumbe, kuburudisha wala kuonya kama lugha haikutumika vizuri. Kuna ufundi mkubwa wa matumizi ya kipengele cha lugha ambayo inajumuisha sarufi, muundo na vionjo muhimu katika lugha, hasa tamathali za semi. Vipengele hivyo husaidia kuongeza msisitizo, ladha, ushawishi na kuonesha usahihi wa kile kilichokusudiwa pasipokuwa na mlolongo wa maneno mengi wala kuikwaza jamii yake.

Lugha ya methali inahitaji tafakuri ya kina itakayowezesha kupata dhana halisi inayokusudiwa na mzungumzaji, agharabu msamiati wa methali huwa na mafumbo ndani yake. Mulokozi (1996) anaweka msisitizo kuwa, mara nyingi mawazo na falsafa katika methali huelezwa kwa kutumia tamathali za usemi, hasa sitiari na mafumbo. Kauli hiyo inaungwa mkono na Ngole na Honera (2004) kwamba baadhi ya tamathali hizo ni tashibiha, sitiari, kejeli na chuku. Mara nyingi viashiria (picha) mbalimbali kama vile wanyama, ndege, vitu na mimea ambavyo kwa dhana na maana humwakilisha binadamu. Msisitizo wa wanafasihi hao ni kwamba matumizi ya methali yanahitaji ujuzi mkubwa katika kipengele cha lugha, zikiwemo tamathali za semi.

Aidha, kaida ni neno ambalo linatumika sana katika taaluma ya isimujamii likiwa na maana ya kanuni na taratibu za matumizi ya lugha kulingana na misingi ya mila na desturi zilizopo katika jamii inayohusika. Kaida ni ada au taratibu zilizozoeleka katika jamii ambazo huwa kama kanuni au desturi (BAKITA, 2017). Katika makala hii, neno kaida limetazamwa kama matumizi ya lugha kwa kuzingatia taratibu na makubaliano ya jamii yenye utamaduni wa aina moja. Hii ina maana kwamba kila jamii imetenga maneno ambayo ni mwiko kutamkwa mbele za watu na msingi wa utaratibu huo umo katika itikadi za jadi zinazorithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine kwa manufaa ya kizazi kilichopo na kijacho.

Lugha na utamaduni wa watu ni vitu viwili changamano mno ambavyo wala havipashwi kutenganishwa. Utamaduni hutuwezesha kufahamu ni kwa kiasi gani kaida, maadili na kanuni zinaelekeza namna lugha inapaswa kutumiwa na kusarifiwa katika jamii bila kuathiri umilisi wa kimawasiliano.Utamaduni hubeba miongozo yake na kuwaasa wanajamii wasitumie baadhi ya maneno au msamiati ambao unachukuliwa kuwa ni mwiko. Mathalani, katika jamii nyingi za Kiafrika, kuna msemo wa adabu/staha unaopaswa kutumiwa kwa lengo la kueleza kitendo cha mama mjamzito kujikopoa mwana. Waswahili husema kuwa '*fulani amejifungua mtoto*' na wala '*siyo fulani amezaa*'. Kwa hiyo, tunapovuruga lugha ya watu, husababisha kuvurugwa kwa utamaduni wa watu hao.

Ukiushi ni istilahi inayopewa nafasi katika taaluma zote za lugha yaani isimu na fasihi. Istilahi hiyo inatokana na neno 'ukiukaji' lenye maana ya hali ya kufanya kinyume na makubaliano au taratibu zilizowekwa (BAKITA, 2017). Miongoni mwa waasisi wa dhana hii ni Huddleston (1976) kama anavyoeleza kuwa binadamu hukiuka maana dhamiriwa anapotumia neno kinyume na kaida za kijamii. Kutokana na maelezo hayo, tunaweza kusema kuwa ukiushi hutokana na kitenzi 'kiuka' neno lenye maana fanya kinyume na matarajio au makubaliano yaliyopo kisheria. Hii ina maana kwamba ukiushi ni utumiaji wa maneno kinyume na ilivyozoeleka katika jamii ya wanajamiilugha.

Akichangia kuhusu ukiushi katika fasihi, Newmark (1981) anasema kuwa ukiushi katika kazi za kifasihi hutokana na mambo mawili. Kwanza, ukiushi humwezesha msanii kuboresha mawasiliano kati yake na hadhira yake. Pili, humwezesha msanii kutoa ufafanuzi katika kiwango cha urejelezi ili kuwasiliana na hadhira yake kwa njia muafaka na kuhakikisha kuwa maana ya ujumbe unaowasilishwa imeeleweka katika kiwango cha kutosha. Makala hii imelitumia neno 'ukiushi' kwa kuweka msisitizo kuwa ni hali ya kutumia neno kinyume na utaratibu wa kaida za kijamii. Hivyo, lugha inapokiuka kaida za kijamii, lazima pawepo na athari zinazojikita katika ukiukaji wa mila na desturi za wanajamiilugha. Matokeo ya ukiushi yanaweza kuzorotesha mwenendo mzima wa ukuaji na matumizi ya lugha yenyewe.

Methali za Kiswahili Hukwepa Ukiushi wa Kaida za Lugha?

Kama tulivyodokeza awali, makala hii inalenga kuchunguza ukiushi wa kaida za lugha katika methali za Kiswahili. Hivyo, katika sehemu hii tumewasilisha uchambuzi wa methali zinazoshadidia kiini cha makala. Msingi wa uchunguzi huu umo ndani ya msamiati unaojenga methali hizo. Ili kurahisisha urejelezi na ufuatiliaji wa mjadala, methali hizo zimegawanywa katika makundi matatu ambayo ni: matumizi ya lugha katika methali zinazohusu viungo vya mwili wa binadamu, matumizi ya lugha katika methali zinazotaja takataka katika mwili wa binadamu na matumizi ya lugha katika methali zinazotaja matendo yanayofanywa na binadamu.

Matumizi ya Lugha katika Methali Zinazohusu Viungo vya Mwili wa Binadamu

Mwili wa binadamu umeumbwa kwa mchanganyiko wa viungo vingi vyenye sifa, ukubwa na kazi tofauti. Tangu jadi kila jamii imejiwekea utaratibu wa kugawa viungo vya mwili katika makundi mawili. Kundi la kwanza lina viungo vya kawaida vinavyoruhusiwa kuonekana na kutajwa hadharani na mtu yeyote, mathalani kichwa, kiganja, mguu, shingo n.k. Kundi la pili ni viungo ambavyo havistahili kutajwa wala kuoneshwa hadharani, mathalani makalio, sehemu ya haja ndogo na kubwa na viungo vya uzazi kwa jinsi zote. Viungo hivyo husitiriwa

kwa kitu chochote, hasa kipande cha nguo. Msingi wa mambo hayo huongozwa na taratibu za kimapokeo kama vile hali ya mazoea, miiko, dini, mila na desturi.

Wagah, O. M., Agak, J. O., & Indoshi, F. C. (2009). Factors that Determine Students' and Teachers' Attitudes Towards Art and Design Curriculum. Masemo.*International Journal of Vocational and Technical Education, 2(1),* 9 - 17. Retrived from http://www.academicjournals.org/ijvte.

Walker, K., Alloway, N., & Dalley-Trim, L. (2008). Secondary School Students' Perceptions of and the Factors Influencing their Decision-Making in Relation to, VET in Schools.*The Australian Educational Researcher, 35 (2),* 55-69. Retrived from http://doi.org/10.1007/bf03216883.

Wollschlager, N. & Guggenhein, E. F (Eds.). (2004). A History of VET in Europe from Divergence to Convergence. *European Journal Vocational Training*, *32*, 1 - 100. Retrived from https://www.cedefop.euopa.eu/files/32-en-pdf.

Ziderman, A. (1997). National Programmes in Technical and Vocational Education: Economic And Education Relationships. *Journal of Vocational Education And Training, 3,* 351 – 366.

Sura ya Mwanamke Inavyoakisiwa katika Nyimbo za Kijamii Nchini Tanzania

Gerephace Mwangosi
Idara ya Lugha, Chuo Kikuu cha Kikatoliki Ruaha
Baruapepe: *mwangosigerephace@yahoo.com*

Zacharia Mwakatobe & Amani W. Mwangosi
Idara ya Lugha na Fasihi, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
Baruapepe: *mwakatobezk@gmail.com*

Ikisiri

Kwa kawaida, fasihi hutegemewa kusawiri hali halisi iliyopo katika jamii kwa kuzingatia muktadha wa jamii inayohusika. Kwa kawaida, fasihi hubadilika kutegemeana na wakati na hufungamana na mifumo mahsusi iliyopo katika jamii. Makala hii imechunguza namna mwanamke anavyojadiliwa katika shughuli mbalimbali za kijamii kupitia utanzu wa nyimbo za kijamii nchini Tanzania. Kipekee, inalenga kuchochea mwamko thabiti wa fikira za mwanamke ili kunyanyua nafasi, hadhi na thamani ya kiutu anayostahiki katika ngazi na asasi mbalimbali za kijamii. Data za msingi za makala hii zilikusanywa katika nyimbo za Magosi za jamii ya Wanyakyusa nchini Tanzania kwa mbinu za majadiliano na uchunguzi-shiriki. Mapitio ya nyaraka zilizotumika kushadadia na kujaziliza data za msingi zilipatikana kwa mbinu za usomaji wa nyaraka. Nadharia ya Ufeministi imetumika katika uchambuzi, uwasilishaji na mjadala wa data. Makala hii inahitimisha kuwa mwanamke hapaswi kutazamwa katika hali ya kupuuzwa na kukandamizwa badala ya kumtazama kama mhimili thabiti katika mifumo ya malezi, uzalishaji mali na uchumi katika ngazi zote za jamii na taifa.

Maneno Msingi: Sura ya Mwanamke, Nyimbo za Magosi na Jamii ya Wanyakyusa.

Utangulizi

Jamii ya Wanyakyusa kama ilivyo katika jamii nyingine hapa nchini inao utamaduni wake ambao umejikita katika fasihi simulizi, zikiwamo

nyimbo za ngoma tangu zama za maisha ya mwanadamu (Tew, 1950). Nyimbo za Magosi ni utanzu uliotamalaki katika jamii zote zinazoishi nchini Malawi na Tanzania katika ukanda wa ziwa Nyasa. Uimbaji wake hufungamana na matumizi ya ngoma yanayoambatana na uchezaji ambao huleta athari za haraka katika kuwasilisha ujumbe (Campbell, 1983). Kwa kawaida, nyimbo za Magosi huchezwa na vijana wanaokuwa katika vikundi vinavyokuwa na waimbaji kati ya 8 hadi 15. Uimbaji wa kawaida hufanyika muda wa jioni baada ya shughuli za uzalishaji mali na uchumi.

Nyimbo za Magosi zimejengwa katika uwanja mpana unaohakiki hali na harakati za maisha ya kila siku ya jamii ya Wanyakyusa. Kupitia utanzu huo, suala la maisha ya binadamu limejadiliwa kwa mitazamo na misukumo mbalimbali. Maisha ya binadamu yanatazamwa katika ngazi zote za maisha yake tangu uzazi, malezi, ndoa, uzee hadi kifo (Mwangosi, 2019). Kila ngazi katika maisha ya binadamu ina harakati zake. Hii ni kwa sababu kila jamii ina vikwazo vyake, miiko yake na masharti yake yanayomwongoza binadamu. Kimsingi, kanuni za jamii humfunga binadamu na kuingilia matakwa na shughuli zake za kujiendeleza kimaisha na kimtazamo. Katika harakati hizo binadamu wana matatizo yao, matakwa yao na maslahi yao.

Katika makala hii, utanzu huu umeonesha kuwa ukandamizwaji, kuonewa na kupuuzwa kwa mwanamke kumeambatana na mkabala wa mwanamke kutumiwa kama chombo duni cha uzalishaji mali na kuendeleza kizazi katika jamii ya mwanadamu. Hali hii inatokana na sababu za utamaduni wa kibepari unaogeuza kila kitu kuwa bidhaa ya kuuzwa sokoni (Siranchi, 1992). Utatuzi wa mgogoro huo una mikabala mingi kufuatana na mitazamo ya jamii. Suala la usawa na ukombozi wa mwanamke halina misingi imara ya kiuchumi na kisiasa; na uduni wake unajitokeza wazi wazi katika asasi mbalimbali za kijamii. Wanaume wanaendelea kuwasilisha nguvu za kiuchumi na kimadaraka katika asasi mbalimbali za kijamii na kitaifa (Khatibu, 2011). Huu ndio msingi wa makala hii iliyolenga kuchunguza sura ya mwanamke katika nyimbo za Magosi za Wanyakyusa nchini Tanzania.

Mbinu na Upeo wa Mada

Wapo wataalamu na wahakiki wengi walioshughulikia suala la mwanamke katika sura tofauti katika kazi za fasihi, ikiwamo fasihi ya Kiswahili. Baadhi yao ni Bader (1974), Mshana (1996), Bond (2000), Momanyi (2001), Chaligha (2011) na Maganga (2015). Wataalamu hawa wote, kama wawakilishi wa wengine, wameonesha mitazamo mbalimbali kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii. Kazi hizo bado zinaibua maswali mengi kila uchao kuhusu mwanamke katika jamii za nchini Tanzania. Makala hii imeshughulikia pengo hilo kupitia utanzu wa nyimbo za Magosi za jamii ya Wanyakyusa nchini Tanzania. Data za msingi zilipatikana kwa mbinu za majadiliano na uchunguzi-shiriki. Nyimbo hizo ziliteuliwa kwa kuwa zina mawanda mapana yaliyotosha kuwakilisha na kushughulikia mada iliyochunguzwa. Mapitio ya nyaraka zilizotumika kufafanua na kujaziliza data za msingi zilipatikana kwa mbinu za usomaji wa nyaraka.

Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Iliyochunguzwa

Suala la ujinsia halijashughulikiwa vya kutosha katika uhakiki wa kifasihi, hasa katika fasihi za Kiafrika, ikiwamo fasihi ya Kiswahili. Wahakiki wengi wa fasihi za Kiafrika wanakumbana na wanawake katika miktadha mbalimbali, lakini wanakwepa kuchunguza na kuhakiki uhusika wao katika fasihi ya Kiswahili kutokana na kuwapo kwa sababu mbalimbali (Senkoro, 1982). Hata hivyo, wasanii wengi wanamchora mwanamke katika sura mbalimbali kulingana na misukumo na mitazamo mbalimbali katika fasihi ya Kiswahili. Baadhi ya wataalamu wamemtazama mwanamke kama mfungwa anayewekwa ndani muda wote pasipo kupewa ruhusa ya kutoka nje (Shafi, 1978). Hali hiyo inamfanya mwanamke kunyimwa haki zake za msingi. Mtazamo huu ulimfanya King'ei (1997) kuwatazama wanawake kama kundi lililokandamizwa na kutengwa kwa muda mrefu bila kushiriki kikamilifu katika harakati mbalimbali za jamii.

Kezilahabi (1975) anaeleza kuwa mgawanyiko kati ya jinsi ya kike na ile ya kiume uligeuka kuwa mgawanyiko kati ya matabaka mara jamii ilipogawanyika baina ya wale waliomiliki nyenzo na njia zote za uzalishaji mali na uchumi ambao walikuwa wanaume dhidi ya wale

ambao hawakuwa na chochote. Wengi wao katika kundi hilo walikuwa ni wanawake. Kuanzia wakati huo, mwanaume amekuwa akiwakilisha nguvu na mwanamke alilazimika kumtegemea mwanaume kwa kila jambo. Jambo hilo lilimfanya Kajeza (2016) kuzishambulia na kuzikosoa baadhi ya asasi zinazoendelea kuchangia kumdhalilisha na kumdunisha mwanamke katika jamii. Suala la kudhalilishwa na kudunishwa kwa mwanamke linapatilizwa na Adeola (1990) anapoeleza kuwa, kuna mtazamo potofu ulioanzishwa na asasi za kijamii za kumwona mwanamke kama chanzo cha uovu katika jamii bila kuchunguza kwa kina mchango wa mwanaume katika kumfanya mwanamke aoneshe tabia zisizofaa. Hali hii inasababishwa na kutamalaki kwa mfumo wa utamaduni unaomtaka mwanamke awe mnyenyekevu na mtiifu kwa mumewe kwa kila jambo. Suala hilo linamfanya mwanamke atazamwe kama kiumbe aliyeumbwa ili kumuondolea upweke mwanaume na kumzalia watoto.

Wapo waandishi (Robert, 1968; El Saadawi, 1983 & Aidoo, 1991) wanaosisitiza kuwapo kwa usawa kati ya mwanaume na mwanamke katika jamii. Hali hiyo huwafanya wanawake wengi kupata nguvu na sauti katika maeneo mengi jambo linalosababisha kujengwa kwa jamii inayoanza kuweka misingi ya usawa na haki katika jamii nyingi hapa nchini na kwingineko barani Afrika. Hali hiyo ilimfanya Mshana (1996) kueleza kwamba wanawake lazima wasimame kidete kwa nguvu zao ili wapambane kwa dhati kwa sauti zao wenyewe na kuacha kuwategemea wanaume ambao kimsingi ndiyo wanaodhulumu haki wanazopigania. Aidha, wanawake hawana budi kupigania haki zao ili kuhakikisha kuwa elimu, kazi, afya na huduma za kiuchumi zinatolewa kwa usawa. Kupigania haki zao ni pamoja na kuhakikisha kuwa wanawake wanashiriki katika nafasi mbalimbali za uongozi katika maeneo ya ngazi za maamuzi pasipo kubaguliwa.

Wahakiki na watafiti wengi wamejaribu kwa kiasi fulani kushughulikia suala la mwanamke kwa namna mbalimbali. Wengi wanaelekea kuafiki kuwa mitindo na miundo ya kijamii pamoja na asasi zake inashirikiana kumkandamiza mwanamke. Suala la utamaduni linatazamwa kama mhimiri mkuu unaosababisha kumdunisha mwanamke katika jamii

(Millet, 1992). Mifumo ya kiutamaduni iliyopo katika jamii imechangia kwa kiasi kikubwa kumchora mwanamke katika mitazamo chanya na hasi. Huu ndio msingi wa makala hii kuchunguza sura ya mwanamke namna inavyoakisiwa katika nyimbo za Magosi za jamii ya Wanyakyusa nchini Tanzania.

Nadharia ya Ufeministi katika Uhakiki wa Kifasihi
Mtazamo wa Ufeministi una historia ndefu duniani kwa kuwa uliibua vuguvugu la kutaka kufuta kabisa suala la uonevu dhidi ya mwanamke. Chimbuko la ukandamizaji wa mwanamke linatokana na uroho wa tamaa ya mwanaume ya kutaka kumdhibiti na kumtawala mwanamke (Shule, 2004). Agenda ya Ufeministi inalenga kumaliza utawala wa mwanaume dhidi ya mwanamke. Ili kufanikiwa, wanawake wanahitaji kubomoa kabisa miundo ya mihimili ya utamaduni wa jamii iliojengeka katika sanaa, dini, sheria na kaya zinazodhibitiwa na mfumo wa kibaba na taswira zote za asasi zinazomwona mwanamke kama mtu dhaifu.

Kwa kurejelea misingi ya nadharia hii, mtafiti alichunguza nguvu za kijamii zinavyohusiana na nguvu za kisanaa. Hii ni kwa sababu kazi ya fasihi inadhibitiwa na miundo iliyopo katika jamii kwa kuzingatia uhusiano wa wanajamii katika mienendo yao ya maisha yao ya kila siku. Kimsingi, fasihi hutazamwa kama usawiri mkamilifu ambao huyasawiri maisha kwa undani na huyachunguza kwa mtazamo mpana (Booker, 1996). Nyimbo teule zilichunguza namna sura ya mwanamke inavyoaminika na kukubalika katika jamii ya wakati wake. Nafasi ya mwanamke ilihakikiwa kulingana na uhusiano wa moja kwa moja uliopo kati ya jamii na hali halisi iliyopo katika jamii za Tanzania. Kwa kawaida, wanawake wanakabiliwa na kuathiriwa na masuala mbalimbali yaliyopo katika jamii zao, hasa njaa na maradhi, pamoja na kuimarika kwa taasubi za kiume na silka za tamaduni kandamizi (Sanga, 2013). Nadharia hii imetumika kuchunguza jinsi mwanamke anavyoakisiwa katika nyimbo za Magosi za jamii ya Wanyakyusa nchini Tanzania.

Sura ya Mwanamke Inavyoakisiwa katika Nyimbo Teule

Historia ya kudunishwa kwa mwanamke katika jamii za ulimwengu ni ndefu kwani inarudi nyuma hadi enzi zile jamii ya watu ilipoanza kugawanyika katika matabaka. Katika baadhi ya jamii kulikuwa na vipindi vya kihistoria ambamo wanawake walitawala kiuchumi na kisiasa (Mugane, 2000). Hali hii ilitokea jamii ilipoanza kugawanyika na kutokea wale waliomiliki njia za uzalishaji mali na uchumi; ndipo mwanaume alipoanza kuwakilisha nguvu za uchumi na kuzitumia nguvu hizo kufanya lolote dhidi ya mwanamke. Uhusiano huo ulizidi kukuzwa na taasisi mbalimbali za kijamii, hasa za kidini na kindoa zilizoambatana na utoaji wa mahari. Suala la mahari linatazamwa katika misingi ya kumnunua mwanamke hali inayoendelea kumpa mwanaume wigo mpana wa kumtumia mwanamke kwa namna anavyotaka.

Suala la harakati za wanawake linaangukia katika mikabala mbalimbali iliyopo katika jamii. Chodorow (1991) anaeleza kuwa upo mkabala unaolitazama suala la harakati za wanawake kutetea haki zao kama sehemu tu ya fujo za dunia. Mtazamo huo hauwezi kutupatia uzito unaopaswa kwa kuwa hautupeleki mbali kulingana na hali halisi ya maisha ya jamii. Pia, upo ule unaoeleza kuwa suala la ukombozi wa mwanamke ni ule uhuru wa kuweza kurudi nyumbani kutoka kazini, kukaa na kusoma gazeti, pamoja na kushiriki katika mijadala mizito na mwanaume. Kwa kawaida, mtazamo huu unataka kutumia mbinu ya kuheshimiana kama kisingizio cha kuhalalisha kuonewa kwa mwanamke. Suala hili linatazamwa kwa wepesi bila kupewa mtazamo sahihi wa namna ya kulishugulikia kwa kurejelea misingi ya ukweli wa kihistoria. Katika nyimbo za Magosi suala la mwanamke limechunguzwa katika sura mbalimbali kama ilivyoelezwa katika sehemu inayofuata.

Kutothaminiwa kwa Mwanamke

Katika jamii nyingi, mwanamke hutazamwa kama kiumbe asiye na uwezo wa kushiriki kwa dhati katika shughuli za kijamii, hasa za kiutawala na kiuchumi. Suala hili huwafanya wanawake wabaguliwe kutokana na kuwapo kwa mgawanyo usio sawa wa kimamlaka kati ya

wanaume na wanawake katika nyanja za kijamii kama vile katika siasa, uchumi, jeshi na dini (Barbara, 1999). Wanawake huonekana kuwa ni watu wa kuongozwa tu. Aidha, uwezo wa wanawake kiuongozi umenyamazishwa bila sababu za msingi. Jambo hili linatokana na mfumo wa jamii unaoamini kuwa mwanamke hawezi kuwa kiongozi imara kama wanaume walivyo. Wanawake wameendelea kuachwa nyuma katika masuala ya msingi ya kimaendeleo pamoja na yale yanayohusu suala la siasa, uzalishaji mali na uchumi (Khatibu, 2014). Wasanii katika wimbo wa *Abhakhikhulu* (Wanawake) wanaeleza:

> *Abakikulu,*Wanawake,
> *Akajapo ugwakubaketa,*Hawashirikishwi,
> *Batikubaligwa mbulongosi,* Hashirikishwi katika uongozi,
> *Kumbombo syosa,*Katika kila jambo,
> *Bikubilamwa!*Hawathaminiwi!

Nukuu hii inaonesha namna wanawake wanavyopewa nafasi ndogo katika nyanja mbalimbali za kijamii. Hakuna asiyefahamu kuwa mwanamke ni nguzo kuu katika uzalishaji mali na kukuza uchumi wa familia, jamii na taifa (Abdun, 2000). Wapo wanawake mwenye taaluma ya masuala ya uchumi wanaosaidia kwa kiasi kikubwa harakati za kukuza uchumi wa jamii na nchi. Kajeza (2016) anaeleza kuwa wakati fulani akiwa anasikiliza wimbo ulioimbwa na hayati Luck Dube, maudhui yake yalimvutia sana kwa kuwa una maneno yanayoeleza namna wanawake wanavyopambana na maisha kwa kujituma ili kuhakikisha kuwa familia zao zinakuwa na ustawi mzuri, pamoja na kuepuka hali ya kumtegemea mwanaume. Luck Dube anaulaumu ulimwengu kwa kumsahau kumtangaza mwanamke kama shujaa na kutompa msaada wa kumuimarisha kama mojawapo ya nguzo maalumu katika malezi ya familia na ukuaji wa uchumi wa taifa. Anaeleza:

> *Kila siku tunawasifu mashujaa, hasa wanaume ambao wanaainishwa katika fani zote za kijamii, lakini wapo tunaowasahau, nao ni wanawake wa ulimwengu huu wanaowajibika na kusimama imara katika majukumu*

> *yao ya kila siku. Mungu wabariki wanawake* (Kajeza, 2016: 31).

Wanawake wengi wameendelea kunyanyaswa na wanaume kwa kukosa nguvu za kiuchumi ili kujisaidia wenyewe. Mlacha (1996) anasisitiza kuwa katika uwanja wa elimu, masomo yanayofundishwa kwa wanawake wengi, bado ni yale yanayowahimiza kuwa manesi, wakunga na makarani kazi ambazo zina kipato kidogo. Jambo hili linawafanya wanawake mara zote kuonekana kama wanawategemea wanaume wanaojiona kuwa ni mabwana walio na mamlaka makubwa juu yao. Kuwapo kwa wanawake wachache katika vyombo vya maamuzi husababisha wanawake kutokuwa na watetezi, hasa yanapotolewa maamuzi yanayowakandamiza. Hali hii haina budi kuwa mojawapo ya changamoto za msingi katika kufanya jitihada za kukabiliana na matatizo yanayowasibu wanawake.

Mwanamke katika Shughuli za Biashara na Uchumi
Katika mfumo wa biashara nchini, wanawake hawapati mikopo kwa urahisi ili kukidhi na kumudu harakati zao za kibiashara. Wengi wao hawana uwezo wa kuendesha biashara zao katika kiwango kinachofaa kutokana na kukosekana kwa mitaji inayokidhi harakati zao za msingi (Freeman, 2008). Wanawake hawakopesheki na hawaaminiki katika taasisi zinazojihusisha na masuala ya fedha kutokana na kuwapo kwa sababu mbalimbali. Wengi hawafanyi biashara zao kisasa kutokana na ukosefu wa mitaji yenye tija. Pengo linalobainishwa huwafanya wanawake walio wengi kutokuwa na sauti katika maeneo mengi. Wasanii katika wimbo wa*Abhakhikhulu* (Wanawake) wanaeleza:

> *Abakikulu,* Wanawake,
> *Akajapo ugwakubaketa,* Hawashirikishwi,
> *Nkumendamenda,* Katika biashara,
> *Bakaja nu twa kubombela,* Hawana mitaji,
> *Bikulima ulutasi,* Hawalimi kisasa,
> *Kumbombo syosa,* Katika kila jambo,
> *Bikubilamwa!* Hawathaminiwi!

Data hii inaonesha namna mwanamke anavyonyimwa na kukosa fursa pana ya kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii kutokana na kutoshirikishwa kikamilifu katika shughuli za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Matokeo yake ni kushindwa kusimama imara katika kila fani ya maendeleo katika jamii. Kushindwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kibiashara na uzalishaji mali na uchumi kunachangia kuporomoka kwa uchumi katika ngazi za familia na taifa (Barwany, 1992). Suala hilo linatokana na sababu zinazomtazama mwanamke kama nguzo imara katika uzalishaji mali na uchumi katika jamii nyingi za Kiafrika na kwingineko barani Afrika. Mshana (1996: 23) anaeleza:

> *Wanawake lazima wasimame kidete kwa nguvu zao ili wajitetee na kupambana kwa dhati kwa sauti zao wenyewe na kuacha kuwategemea wanaume ambao kimsingi ndiyo wanaodhulumu haki wanazopigania. Wanawake hawana budi kupigania haki zao katika taifa lao ili kuhakikisha kuwa elimu, kazi, afya na huduma za kiuchumi zinatolewa kwa usawa. Kupigania haki zao ni pamoja na kuhakikisha kuwa wanawake wanashiriki katika nafasi mbalimbali za uongozi katika maeneo ya ngazi za maamuzi pasipo kubaguliwa.*

Barani Afrika, karibu wanawake wote hujishughulisha na kilimo ili kulea na kutunza familia zao. Licha ya majukumu hayo, wanawake wana nafasi ndogo ya kuwa na maamuzi na kupata nyenzo za kuzalishia mazao, hasa pembejeo na teknolojia (Momanyi, 1998). Kuna fikira potofu inayoshikiliwa kuwa mchango wa wanawake katika kuinua uchumi unatambuliwa na mahitaji yao yanatoshelezwa kwa kiwango cha kutosha; na kwamba wanawake wanapata manufaa yanatokana na miradi fulani ya maendeleo ya jamii (Seleman, 2008). Kwa namna hali ilivyo, ukweli ni kwamba wanawake wanakosa mikopo na mafunzo yanayofaa hali inayoendelea kupunguza mapato wanayoweza kupatikana kutokana na shughuli zao za kujikwamua kimaisha na kiuchumi.

Mwanamke katika Sekta ya Maendeleo

Umoja ni fimbo ya mnyonge katika jamii na taifa lolote. Uzoefu huu unaonesha kuwapo kwa haja ya kuwashirikisha wanawake kikamilifu katika shughuli zote za maendeleo na kupewa nafasi na wapanga sera, hasa katika utekeelezaji wake (Okeke, 1996). Serikali ya Tanzania, kwa kutambua hali na ushiriki wa wanawake katika jamii, na kwa kuzingatia Tangazo la Kimataifa la Haki za Binadamu na lile la Azimio la Beijing la mwaka 1995, imefanya jitihada kubwa zinazolenga kuitikia hali ya mahitaji ya wanawake nchini kisheria. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limetunga sheria ili kuwawezesha wanawake kumiliki mali na ardhi, ingawa bado imekuwa vigumu katika utekelezaji wake. Namna pekee ya kufikia lengo hili imeelezwa katika mapendekezo yaliyopitishwa na Mikutano ya Umoja wa Mataifa iliyofanywa mwaka 1976, 1980 na 1985 huko Mexico City, Copenhagen na Nairobi, ambako haja ya kutambua haki ya ushirikishwaji wa watu wote inapaswa kutiliwa mkazo na kuinuliwa kwa hadhi ya wanawake kimaisha, kiuchumi na kimaendeleo ya jamii (Sozigwa, 1993). Maendeleo ya wanawake hayana budi kuunganishwa kwa ukamilifu ndani ya sera za maendeleo ya taifa. Wasanii katika wimbo wa *Abhakhikhulu* (Wanawake) wanaeleza:

> *Abakikulu,* Wanawake,
> *Abhukikulu ne njila,* Wanawake na kazi,
> *Ikumbhulu jo mbombo,* Jembe ni kazi,
> *Abalimi bho bhakikulu,* Wakulima ni wanawake,
> *Abakukulu bho bha mboto,* Wazalishaji wakuu,
> *Bikubilamwa!* Hawathaminiwi!

Maelezo hayo yanaonesha kuwa mwanawake ni mhimiri wa maendeleo, hasa katika shughuli za kilimo. Kipekee, wanahitaji kuunganishwa moja kwa moja ndani ya sera zinazotekelezeka zinazolenga kuwawezesha kiteknolojia na kimitaji (Grosz, 1994). Suala la sera ya kulinda na kuhimiza uwezo wa wanawake wa kushiriki kuinua mchango wao katika sekta zote za uchumi na kuimarisha jinsi ya kujitegemea, ushirikishwaji wa umma, pamoja na kulinda mazingira linapaswa kuchunguzwa upya kwa manufaa endelevu ya jamii na taifa.

Ingefaa taratibu na sheria zilizopo sasa zirekebishwe ili kusaidia wanawake kuingizwa katika mkondo mzima wa uchumi. Oyeronke (2005: 14) anaeleza:

> *Ipo haja ya kujenga vyombo na taratibu zitakazojali nafasi za maumbile katika shughuli za maendeleo. Miundo ya mikakati, mitazamo ya ushirikishaji wa kiwakati na kisera, mafunzo ya mawakala wa maendeleo na marekebisho ya taratibu za uendeshaji na za sheria, lazima vyote vioneshe jukumu muhimu walilonalo wanawake katika kujenga uchumi wa jamii na taifa, hasa katika shughuli za uzalishaji mali na uchumi katika ngazi zote za kijamii.*

Data hii inaonesha kuwa maendeleo yanayowafikiria wanawake si jambo linalowahusu wanasiasa pekee, bali ushirikishwaji katika kila ngazi ya maendeleo ni sharti la msingi kwa ufanisi endelevu kwa uchumi na kwa ustawi wa jamii. Fikira hizo zinahitajika kubadilika katika jamii zote, hasa katika jamii ambazo hisia za mwanamke hutazamwa kuwa duni kuliko mwanaume zinaendelea kutamalaki, na ambako hirizi ya utamaduni mbovu unaoendelea kutumiwa kuhalalisha kubaguliwa kwa wanawake (Muindi, 1996). Kwa kutambua majukumu ya maendeleo ya taifa, lazima wanawake washirikishwe na kuwezeshwa kikamilifu katika shughuli zote za maendeleo ya jamii na taifa.

Mwanamke Kutoshiriki katika Maamuzi

Nafasi ya mwanamke katika kufanya maamuzi na uwakilishi wake ni mdogo katika ngazi za kijamii na kiserikali, ingawa katiba ya mwaka 1977 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 1984 inatoa haki sawa baina ya mwanawake na mwanaume, hasa katika kupiga kura na kuutumikia umma. Mtandao wa Jinsia Tanzania (2001) wanaeleza kwamba ipo tofauti kubwa kati ya wanawake na wanaume katika masuala yanayojitokeza serikalini katika ngazi za uongozi na ufanyaji wa maamuzi. Pia, utaratibu wa ufanyaji wa maamuzi katika ngazi za kaya si wa kidemokrasia kwa kuwa wanawake hawahusishwi kikamilifu ili kujenga misingi imara ya mahusiano ya kijamii katika ngazi zote

(Mbelle, 1990). Hali hii ikiendelea, ni dhahiri kuwa jamii itaendelea kupata viongozi ambao ni zao la ushabiki usiozingatia sifa mahsusi za kiongozi bora. Katika wimbo wa *Haki Sawa* wasanii wanaeleza:

> *Mabadiliko,*
> *Haki sawa,*
> *Acha vitisho vya talaka kutoa,*
> *Kumchagua umtakaye,*
> *Waache wanawake,*
> *Kulazimisha waje mliko,*
> *Katika vyama vyenu,*
> *Wasilazimishwe!*

Katika nukuu hii, wasanii wanaonesha namna mwanamke anavyolazimishwa kuishi na kufanya shughuli za kijamii kwa mujibu wa misingi iliyopo katika kaya zao. Katika masuala ya siasa, mwanamke analazimishwa kumchagua kiongozi wa chama cha siasa kwa mujibu wa chaguo la mumewe. Kwa kufanya hiyo, mwanamke ataendelea kupoteza haki yake ya msingi ya kidemokrasia kutokana na kuwapo kwa utamaduni ambao unatakiwa kuchunguzwa upya katika kipindi hiki cha mfumo wa vyama vingi vya siasa hapa nchini. Jambo hilo si sahihi kwa ustawi wa demokrasia na maendeleo yake hapa nchini. Kihistoria, umoja wa wafanyabiashara wanawake ndio uliokuwa na haki ya kufanya kazi katika sekta za umma na kupata haki ya kupiga kura (Pullen, 2006). Katika kipindi hiki cha mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini, si sahihi kwa mwanamke kuendelea kumchagua kiongozi wa serikali na chama bila kuzingatia uzito wa ilani ya uchaguzi na hoja zinazofafanua namna bora ya utekelezaji wa sera, katiba na uwajibikaji wenye tija kwa maslahi ya jamii na taifa. Katika kuthibitisha kuwapo kwa hali hiyo (Mwangosi, 2019: 172) anaeleza kwamba:

> *Mfumo dume ni itikadi ya kawaida inayotumika*
> *ulimwenguni kote kuunda mahusiano ya kijamii*
> *yanayobainisha dhima duni ya wanawake, pamoja na*
> *jinsi wanavyonyanyaswa, wanavyonyonywa na*

> *kushindwa kushiriki kikamilifu katika maamuzi ya msingi katika ngazi zote za kijamii. Itikadi hiyo inaathiri sana uchaguzi kwa kuwa wanawake hawawezi kushindana na wanaume katika baadhi ya mambo, yakiwamo ya kuchagua na kuchaguliwa.*

> *Kutokana na mabadiliko makubwa yanayojitokeza katika sekta za uchumi, utamaduni na siasa ni jambo la busara kuutazama upya mfumo huu kwa madhumuni ya kujenga misingi inayochochea umoja na mshikamano kati ya mwanamke na mwanamke katika eneo la kusimamia mipango na maendeleo ya jamii na taifa. Kuendelea kuufuata ni kuzidi kudhoofisha jitihada za umoja na mshikamamo wa kitaifa zinazolenga kuchochea maendeleo ya watu wake.*

Maelezo haya yanaitazama Tume ya Uchaguzi ya Taifa nchini kama chombo kilichoshindwa kufika maeneo yote, hasa kutoa elimu kuhusu haki ya mpiga kura kwa kila raia. Pengo hilo limesababisha baadhi ya wananchi kufanya vyovyote wanavyoweza kwa sababu hawana elimu ya kutosha kuhusu haki na taratibu za kupiga kura na uchaguzi. Mwanamke anahitaji kupata elimu sahihi ya kupiga kura na kuchagua viongozi awatakao bila shinikizo. Kwa muda mrefu, wanawake waliwekwa katika daraja la chini na hawakuhusishwa katika michakato ya kuendeleza masuala ya kidemokrasia katika mataifa yao kutokana na kukosekana kwa elimu na utashi wa siasa za mataifa ya dunia (Guethel, 1981). Kidemokrasia, mwanamke hapaswi kulazimishwa wala kutishiwa kwa kuwa ni kiumbe aliye na utashi na haki ya kufanya maamuzi kwa kuzingatia sheria. Wasanii katika wimbo huo huo wa *Haki Sawa* wanaeleza:

> *Mabadiliko,*
> *Haki sawa,*
> *Katika kipindi cha nyuma,*
> *Haki haikutendeka,*
> *Kwa upande wa mwanamke,*

> *Hawakupewa haki,*
> *Katika siasa na elimu,*
> *Ilikuwa kwanza wa kiume,*
> *Sasa wa kike kwanza,*
> *Wasilazimishwe!*

Kwa namna hali ilivyo, upo umuhimu wa kufanyika mabadiliko makubwa katika mfumo wa siasa, hasa namna bora ya kumfanya mwanamke ashiriki kikamilifu katika shughuli zote za ujenzi na maendeleo ya taifa lake kulingana na sheria za taifa zilizopo, hasa misingi ya haki na usawa katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Jambo hilo likifanyika kwa usahihi litaiepusha jamii katika mivutano ya kitabaka isiyokuwa ya lazima hapa nchini (Kiango, 1992). Kwa upande mwingine, kuimarika kwa misingi ya umoja na mshikamano katika jamii ni nyenzo imara katika ujenzi wa jamii, taifa na maendeleo yake.

Kudunishwa na Kudhalilishwa kwa Mwanamke

Licha ya kuwapo kwa miongozo sahihi ya serikali inayolenga kumtetea mwanamke, kwa kiasi kikubwa, haitekelezeki kwa kuwa wanawake hawana taarifa za kutosha kuhusu namna bora ya kupambana na mila na desturi zinazowadhulumu. Wanawake walio wengi hawana habari hiyo kama inavyoelezwa katika katiba kifungu namba 13 cha ya ndoa cha mwaka 1971 kama kilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2000. Matokeo yake, wanawake wengi wanaishia kukandamizwa na baadhi ya mila na desturi zilizoshamiri katika jamii zao. Wasanii wanaeleza katika wimbo wa *Ulumilisyo* (Kulazimisha):

> *Unyambala,* Mwanaume,
> *Nu kubweja kwa lugano*, Kwa bashasha za mapenzi,
> *Ne kinyonyo kya bhulogwe,* Kwa tamaa za kingono,
> *Pakumilisya ukwegigwa ubhana*, Kulazimisha vitoto kuolewa,
> *Ukunyasya nu konanga,* Kuvinajisi, uharibifu,
> *Ukujujubika utwana,* Unyanyasaji watoto,
> *Bubuti kubana*, Udhalimu kwa watoto,
> *Ingomelesyo sikanamino!* Sheria kibogoyo!

145

Fungu hili linaonesha kuwapo kwa utamaduni unazomkandamiza mwanamke na kumnyima haki ya kuamua na kuchagua mtindo wa maisha anayotaka bila kuvunja sheria za nchi, pamoja na kaida bora zilizozoeleka katika jamii. Matokeo yake, mwanamke amejikuta akiogelea katika bahari kuu ya kupuuzwa na kuonewa, kunyanyaswa, kukandamizwa na kulazimishwa kuolewa kabla ya kukomaa kikamilifu kwa mujibu wa sheria za nchi na uhalali wa mila na desturi za kijamii. Kuwapo kwa hali ya utamaduni unaomtaka mwanamke awe mnyenyekevu na mtiifu kwa mumewe, kumemfanya mwanamke aendelea kunyanyasika na kudhalilishwa katika jamii nyingi hapa nchini. Bond (2000: 17) anaeleza:

> *Utamaduni ndio unaoweka alama na kanuni zilizozoeleka na kutumiwa na jamii, na baadaye huota mizizi na kutumika kama sheria rasmi za jamii inayohusika; na zinaendelea kuonesha nafasi na majukumu ya mwanamke na mwanaume. Kipengele cha utamaduni kinatengeneza mazingira ya kumkandamiza mwanamke asifikie ngazi za juu za uongozi kwani wanaume hawaamini kama wanawake wanaweza kuongoza vizuri na kuyatimiza maamuzi ya wanaume na wanawake kwa usawa. Kwa hiyo, matokeo ya mtazamo huu, wanawake wanaishia kuwekwa pembeni na kuendelea kuwa watazamaji wa kila kinachotokea katika jamii zao.*

Kwa kawaida, wanawake katika baadhi ya jamii hawana mamlaka katika masuala mbalimbali ya kijamii. Hali hii inawafanya wanawake waelemewe na majukumu kemkem na hawawezi kulalamika kwa kuwa utamaduni unamtaka asiwe mdadisi, bali awe mtiifu kwa mumewe (Momanyi, 2001). Baadhi ya wanaume wanatumia uwezo wao wa kiuchumi na kifedha kuwarubuni wanawake, hasa mabinti wadogo. Hali hiyo huwatumbukiza katika hali mbaya ya maisha, kutumbukia katika maradhi ya kuambukizwa (UKIMWI), magonjwa ya zinaa, kukatishwa masomo na hata kupata mimba katika umri mdogo. Sheria

kali za kisheria hazina budi kuchukuliwa ili kupambana na hali hiyo. Wasanii katika wimbo huo huo wa*Kilingo* (Urithi) wanaeleza:

> *Unyambala,* Mwanaume,
> *Bhikulongosya indalama,* Kutumia vishilingi,
> *Ukonanga abhalindwana,* Kuvitafuta vibinti,
> *Isyaba kulumba bikubhomba,* Ya wakubwa kuvitendea,
> *Isyo sya vinyamana,* Hakika ni uhayawani,
> *Ingomelesyo sikanamino ,*Sheria kibogoyo.

Khamis (1982) anaeleza kuwa mapambano ya ukombozi wa wanawake yawe huru na ya kujitegemea; na yasifanye kazi ndani ya matakwa ya wanaume. Wanaume wasiwepo kabisa katika jitihada za ukombozi wa mwanamke. Mapambano yanashindikana kwa sababu mfumo wa kibaba uliasisiwa na wanaume ili kuwatawala wanawake. Kwa namna hali ilivyo sasa, wanaume hawana budi kuwekwa kando katika harakati za ukombozi dhidi ya mwanamke ili kuepuka hujumu na kukwamisha jitihada za wanawake. Jambo hili linashadidiwa na Kalugula (1991: 28) anaeleza:

> *Utawala wa kibaba katika jamii nyinginezo hapa nchini na kwingineko barani Afrika, na mtazamo mkuu wa ustaarabu wao unaotawaliwa na kuongozwa na wanaume, ndiyo umewafanya wanawake kuwa wasaidizi wa wanaume katika nyanja zote za kijamii kama katika utamaduni, dini, familia, siasa, uchumi, sheria na sanaa. Kwa bahati mbaya, mfumo huu unatazamwa kwa jicho la kawaida na jumuiya ya wanawake, hasa wale waishio vijijini ambako mwamko wa kupata elimu inayotetea haki zao, bado ni mdogo sana ikilinganishwa na harakati zilizopo katika miji na vijiji-miji vya nchi hii. Kwa msingi huo, jitihada za wanawake kutaka kujikomboa hazitafua dafu kama mti wa utawala wa kibaba hautavunjwa na kung'oa mizizi yake yote.*

147

Kwa upande wa elimu, bado mwanamke anaendelea kuwekwa nyuma kutokana na sababu za kimila, zikiwamo za kuolewa. Kimsingi, elimu ni haki ya lazima kwa kila mtu, bila kujali jinsia. Hata hivyo, sera ya elimu kwa wote na ile ya elimu ya watu wazima za mwaka 1974 zimesaidia angalau kwa kiasi wanawake na wanaume kupata elimu japo ya msingi. Kutokana na sababu hizo, kusoma na kusomeshwa lilikuwa jambo la hiari, ingawa miaka hii ya 2000 limeanza kupungua kwa kasi kutokana na kuwapo kwa mwamko mkubwa wa kielimu.

Wanawake wanahamasishwa kusoma kwa bidii hadi elimu ya juu. Suala la wanawake kufika elimu ya juu halipo kwa kuwa hufikiri kwamba haiwahusu (Pullen, 2006). Fikira hizo hazina budi kuvunjwa kwa kuwa wanawake wanastahili kupata elimu ya juu kama ilivyo kwa wanaume. Hata hivyo, baadhi ya wazazi wamekosa mwamko wa kuwasomesha watoto wa kike kwa sababu ya kuwapo kwa fikira potofu, pamoja na msukumo mdogo wa uchumi. Kwa namna hali halisi ilivyo sasa, ni wakati sahihi wa kuunda sheria zinazotekelezeka zikiwa na lengo la kupambana na kuondoa mianya inayomdhulumu mwanamke katika sekta zote za kijamii, vinginevyo, nafasi yake itaendelea kuwa duni katika maamuzi na majukumu ya kijamii na kitaifa.

Hitimisho na Mapendekezo
Katika makala hii, sura ya mwanamke imeelezwa kwa namna mbalimbali katika nyimbo za Magosi za jamii ya Wanyakyusa nchini Tanzania. Jambo la kuzingatia ni kwamba jamii haina budi kupinga mambo yote yanayonuia kumdunisha mwanamke katika hali mbalimbali. Aidha, itakuwa vizuri kama watafiti wengine watachunguza kuhusu mwanamke, desturi na miiko katika tanzu nyingine za fasihi ya Kiswahili, hasa katika tanzu za hadithi, nyimbo na semi za kijamii. Jambo hili linategemea sana utamaduni wa jamii unajidhihirisha wazi wazi katika tanzu hizo. Utamaduni ni asasi mojawapo ya kijamii iliyosheheni taarifa mahususi kuhusu nafasi ya mwanamke na maisha ya binadamu katika jamii za ulimwengu.

Jamii haina budi kubadilika kulingana na mahitaji ya wakati kwani suala la umoja na mshikamano kati ya mwanamke na mwanaume ni la msingi katika ujenzi wa jamii na taifa. Kutokana na mwamko wa elimu, harakati za serikali na taasisi zisizo za kiserikali kuendelea kupinga na kukemea hali yoyote inayonuia kumtazama mwanamke katika mtazamo hasi zitawasaidia wanawake kufanikisha wajibu wao katika jamii. Kimsingi, umoja ni fimbo ya mnyonge katika jamii na taifa lolote duniani. Mwanamke hana budi kutazamwa kama mhimiri imara katika ujenzi na harakati za maendeleo ya jamii na taifa.

Marejeleo

Adeola, J. (1990). *In their Own Voices: African Women Writters Talk*. London: James Currey Limited.

Aidoo, A. A. (1991). *Changes: A Love Story.* City University of New York: The New York Feminist Press.

Abdun, N. H. (2000). *Ukombozi wa Mwanamke*. Morogoro: Mzumbe Book Project.

Bader, Z. (1974).'Social Condition of the Peasant Women in Zambia and Pemba'. Paper No, 18 Iliyowasilishwa katika Semina ya Wanawake Brulap. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Barbara, A. (1999). *Politics and Feminist*. UK: Blackwell Publishers.

Barwany, N. J. (1992). *How Marriage Customs and Traditions Effect Woman Progress in Zanzibar.* Unpublished Article.

Bond, S. (2000). 'Culture and Feminine Leadership', In *Women Power and the Academic From Rhetoric to Reality*. New York: Berghahn Books.

Booker, M. K. (1996). *A Practical Introduction of Literary Theory and Criticism*. New York: Longman USA Publishers.

Campbell, C. A. (1983). Nyimbo za Kiswahili: A Sociol Ethnomusicological Study of the Swahili Poetic Form. A Thesis for Doctor of Philosophy. University of Washington.

Challigha, N. E. (2011). Usawiri wa Mwanamke na Mgawanyo wa Majukumu Kijinsia katika Fasihi Picha ya Katuni Mnato za Kiswahili. Tasinifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Chodorow, N. J. (1991). *Feminism and Psychonalytic Theory*. London: Yale University Press.

El Saadawi, N. (1983). *Women at Point Zero London*. London: Zed Books Ltd.

Freeman, M. (2008). *Women: A Feminist Perspective.* Califonia: Ufield Publishing Campany.

Guethel, A. (1981). *Sociology of Housework*. New York: Pantheon Books.

Grosz, E. (1994). *Bodies and Knowledge Feminism and Crises of Reason*. In Feminist Epistermologies.

Hino, S. (1968). The Custome Culture of the Swahili People katika Kyoto University African Studies 2: 109 – 149, Kyoto University.

Kajeza, R. T. (2016). Usawiri wa Mwanamke katika Fasihi Andishi: Mifano Kutoka katika riwaya ya *Machozi na Damu* ya E. Shigongo (2005). Tasinifu ya Shahada ya Kwanza. Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

Kalugula, C. (1991). *The Policy Implications of Sex-Role Stereotyping in Text Books for Girls in Tanzania: Seminar on Women and Education in Tanzania*. Dar es Salaam.

Kezilahabi, E. (1975). *Dunia Uwanja wa Fujo*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kiango, S. D. (1992). Taswira ya Mwanamke katika Tamthiliya za Kiswahili za Kenya 'Baragumu', CKM, 102: 84 - 91.

King'ei, K. (1997). *Mwongozo wa Amezidi*. Nairobi: East African Publishers.

Khatibu, M. S. (2011). *Chanjo, Matakwa ya Mwanaume Katika Mwili wa Mwanamke: Ulinganisho wa Ushairi wa Muyaka na Shaaban Robert.* Taaluma ya Taasisi za Kiswahili.

Maganga, M. (2015). Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya *Pesa Zako Zinanuka*. Tasinifu ya Shahada ya kwanza. Chuo Kikuu cha Tumain Makumira.

Mbelle, M. B. (1990). Women in Classical Swahili Poetry. (Unpublished Article) University of Dar es Salaam.

Millet, P. (1969). *Sexual Politics*. London: Manchester Univesity Press.

Mlacha, S. A. (1996). *Women's Images in Kiswahili Poetry and Taarab Songs in Gender Relations and Women in the Media*. University of Dar es Salaam.

Momanyi, C. (1998). Usanii wa Mwanamke wa Kiislamu katika Jamii ya Waswahili kama Ilivyobainika katika Ushairi wa Kiswahili. Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Momanyi, C. (2001). 'Nafasi ya Mwanamke katika Ushairi wa Shaaban Robert' katika *Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI, Uk. 53 - 65.

Mshana, R. (1996). 'Nafasi ya Wanawake katika Mageuzi ya Kisiasa na Uchumi' katika*Jarida la Kichungaji*. Juzuu 3, Na 1. Uk. 28 - 36.

Mtandao wa Jinsia Tanzania (2001). 'Kuelekea Kwenye Usawa: Taswira ya Mwanamke Tanzania'. Dar es Salaam: SARDC.

Mugane, D. (2012). Nafasi ya Mwanamke katika Jamii. U. S. A: Harvard Univesity Press.

Muindi, A. (1996). Usawiri wa Wahusika Makahaba katika Vitabu vya Said Ahmed Mohamed. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mwangosi, G. (2019). Kuchunguza Dhamira na Fani katika Nyimbo za Magosi za Jamii ya Wanyakyusa. Shahada ya Uzamivu. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Okeke, P. (1996). 'Post-Modern Ferminist and Knowledge Productions; The African Context in Africa Today'. Vol. 43, No, 3. July – September, 1996. Boulder: Lynne Rienner Publishers.

Oyeronke, O. (2005). *African Gender Studies*. New York: Palgrave MacMillan.

Pullen, C. (2006). *Marxist Against Feminists on Education*. London: Routledge.

Robert, S. (1968). *Kufikirika.* Nairobi: Nelson.

Sanga, A. (2013). *Wanawake na Injili katika Ujasiriamali.* Dar es Salaam: Ujuzi Education Publishers Limited.

Seleman, H. J. (2008). Ujamiishaji wa Kijinsia katika Nyimbo za Harusi za Kihaya. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Dodoma.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Shafi, A. S. (1999). *Vuta N'kuvute*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Shule, V. (2004).'Effective Video Film Reducing Young Womens Gender Violence and Other.HIV Risk Behaviours'. A Research for Master Degree. University of Dar es Salaam.

Siranchi, B. M. (1992). Hadhi na Hali ya Mwanamke katika Riwaya za S. A. Mohamed. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sozigwa P. (1993). *Majukumu ya Nchi za Kusini: Ripoti ya Tume ya Kusini*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Tew, M. (1950). *People of the Lake Nyasa Region*. London: SAGE Publications.

Taswira ya Uhusika wa Mhusika Nguli katika Tamthiliya ya Kiswahili

Ndimyake Mwakanjuki
Idara ya Lugha, Chuo Kikuu cha Kikatoliki Ruaha
Baruapepe: *ndimmyake@gmail.com*

Gerephace Mwangosi
Idara ya Lugha, Chuo Kikuu cha Kikatoliki Ruaha
Baruapepe: *mwangosigerephace@yahoo.com*

Ikisiri

Tamthiliya ya Kiswahili ni miongoni mwa kazi za kisanaa zenye wajibu mkubwa wa kuijenga jamii katika hali mbalimbali za kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni kupitia wahusika wake. Kwa kawaida, wahusika hudhibitiwa na kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na hisia za muktadha wa mtunzi, kwani mawazo yao hutokana na falsafa zao, mazingira yao, utamaduni wao, hali ya maisha na harakati zilizopo katika jamii inayohusika. Makala hii imechunguza uhusika wa mhusika nguli katika tamthiliya ya Kiswahili. Imefanya hivyo kwa kurejelea tamthiliya teule za Emanuel Mbogo, *Fumo Liongo* (2009) na *Sundiata* (2011). Data za msingi zilikusanywa kwa mbinu ya usomaji wa matini teule. Data za upili kwa ajili ya kufafanua na kujaziliza katika data za msingi zilikusanywa maktabani kwa mbinu ya usomaji wa nyaraka. Uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa uliongozwa na nadharia ya Semiotiki. Makala hii inatoa wito kwa wanajamii wote kuwa na moyo wa uzalendo, mshikamano kwa kuepuka usaliti, uchu wa mali na madaraka, visasi na ukatili ili kujenga jamii yenye ustawi imara katika fani zote za kimaisha.

Utangulizi

Tamthiliya ni miongoni mwa tanzu za fasihi ya Kiswahili zinazoshughulikia masuala yanayomhusu binadamu, mazingira yake, itikadi, mitindo na mifumo ya maisha kwa mawanda tofauti tofauti (Shule, 2010). Matukio huelezwa kwa mtindo wa igizaji wa jambo lolote lililoshuhudiwa au kusikika. Hali hiyo, huupa utanzu huo fursa pana ya kuyashughulikia masuala ya kijamii kwa mawanda mapana.

Mtunzi husawiri mawazo kwa maongezi ya wahusika kwa kujenga migongano na mijadala baina yao (Daniel, 2012). Wahusika huteuliwa ili kuwasilisha hali, tabia, hisia, mawazo na matendo ya wahusika wanaowamithilisha. Kwa msingi huo, tamthiliya ni miongoni mwa tanzu kubwa na muhimu za kifasihi (Wafula, 1999). Mtazamo wa Wafula unaweza kudhihirisha kuwapo kwa uwezekano mkubwa wa tanzu kuingiliana ili kukamilishana na kutegemeana.

Kabla ya kuwapo kwa taaluma ya uchapishaji katika jamii za Kiafrika, sanaa za maonesho zilitazamwa kama chombo thabiti kilichofungamana na mitindo ya maisha iliyoakisi ujumi wa utamaduni; na kutazamwa kama ghala la rasilimali na amali za Uafrika (Wafula, 1999). Maarifa yanayopatikana katika tamthiliya ni mojawapo ya shahada ya pekee kwa wanajamii kuweza kuitumia katika harakati zao za kuyamudu maisha na mazingira yao. Maendeleo ya utanzu huu yamechukua mikondo tofauti kutegemeana na historia na utamaduni wa jamii inayohusika. Katika karne ya 20 imeingia katika mikondo mingi ya kimajaribio na kiuasi (Ali, 2017). Wakati mwingine, si rahisi kubaini tofauti zilizopo kati yake na tanzu nyingine kutokana kuwapo kwa mwingiliano mkubwa kimuundo. Kitu kinachoweza kuzitofautisha fani hizo ni malengo na maumbo yake.

Kwa namna hali ilivyo sasa, utanzu huu hutazamwa kama chombo kinachoihakiki jamii namna ilivyo na inavyoweza kujieleza. Pia, hutumiwa kuukuza na kuuendeleza ufahamu mpana kuhusu masuala mengi yanayohusu falsafa, mazingira na hali halisi iliyopo katika jamii inayohusika (Gichamba, 2005). Kwa upande mwingine, hutazamwa kama kipimajoto cha maendeleo na hali halisi iliyopo katika jamii kwa kuchambua na kuhakiki masuala yote yanayohusu harakati na fani zote za mwanadamu kama vile maarifa, falsafa, siasa, utamaduni, uchumi, historia, mazingira na maendeleo yake. Kwa msingi huo, makala hii imeshugulikia jukumu hilo kwa kuchunguza taswira ya mhusika nguli katika tamthiliya teule za Emanuel Mbogo, *Fumo Liongo* (2009) na *Sundiata* (2011).

Dhana ya Mhusika Nguli

Kulingana na Campbell (1968), mhusika nguli ni mtu anayeikomboa jamii yake katika mambo ambayo wengine hawawezi kuyatafuta. Anaendelea kueleza kwamba nguli hana budi kuwa na nguvu za kisihiri, ushajaa, urijali, kuungana na watu wake ili kupambana kwa ajili ya kuwakomboa. Ushindi atakaoupata si wake peke yake, bali ni wa jamii nzima. Nguli anaweza kuondoka na kurudi baadaye ili kuleta na kutetea haki kwa watu wake. Mulokozi (1996) anamuona mhusika mkuu ndiye nguli katika kazi ya fasihi. Kwa hiyo, nguli wa tamthiliya ni yule ambaye matendo mengi yanahusu maisha na majaliwa yake, akitolea mfano wa Kinjekitile katika tamthiliya ya *Kinjekitile* (1978). Pia, anaongeza kwamba katika tanzia ya kijadi, nguli huwa anatoka katika tabaka la juu, ambapo huwa anaangamia kutokana na ila fulani katika tabia yake, maamuzi yake ama kusakamwa na mazingira yaliyomzidi uwezo. Maelezo haya yanatupa msingi wa kumchunguza nguli na tajriba anazokumbana na katika ulimwengu anamoishi.

Wamitila (2003) ameeleza kuwa shujaa ni dhana inayotumiwa kuelezea mhusika mkuu ambaye anaweza kuwa wa kike au wa kiume. Mhusika mkuu anaweza kuwa mbaya au mwema kama mhusika Dakta Matoga anavyoelezwa katika *Vipuli vya Figo* (2014). Pia, kuna shujaa kinzani, dhana inayorejelea mhusika ambaye haelekei kutangamana na jamii yake; ni dhaifu na huishia kuonesha sifa za ushinde. Mara nyingi wahusika katika kundi hili huusishwa na ubwege na huwa na wahusika wasimulizi ambao hawana sifa za kishujaa kama Kazimoto katika *Kichwa Maji* (1974).

Raymond (1966) katika kuelezea aina za tanzia, ndipo anaainisha sifa za mhusika mkuu kama shujaa. Humwangalia shujaa kuwab lazima awe mtu bora ambaye kuaminika kwake kunakotokana na uhuru alionao binadamu katika kufuata ushauri wake; na anapatikana katika tabaka tawala ambalo, kwa kawaida, ndio chanzo cha uovu na harakati mbalimbali. Kundi hili huzingatia sana dhamira ambapo shujaa aliweza kutatanishwa na dhamiri yake mwenyewe. Pia, shujaa anayepatikana katika tanzia ya kisasa ambayo inatokana na mabadiliko ya fikira za maisha ya watu huko Ulaya karne ya 18 kipindi ambacho ubepari

ulikuwa umeshamiri pamoja na unyonyaji. Shujaa katika kundi hili alionekana ni yule aliyetoka katika ngazi yoyote ya jamii. Hata hivyo, katika kipindi hicho, msisitizo mkuu ulikuwa kuhamasisha watu kutumia sayansi katika masuala ya jamii kutafuta chanzo cha matatizo na kudhibiti matokeo yake.

Mwisho, ni tanzia ya uhalisia wa Kijamaa iliyotokana na Ukomunisti ili kuleta jamii isiyo na matabaka duniani. Shujaa katika kundi hili ni mhusika anayejengwa kipropaganda kwa manufaa ya siasa ya kikomunisti. Shujaa alitakiwa awe amefikia kiwango cha juu cha ubinadamu, awe na moyo wa ushupavu na uzalendo, akili, aheshimu watu na awe na msimamo mmoja tu kuhusu misingi ya Ujamaa na maendeleo yake. Upungufu wa tanzia hii ni kumtaka mhusika asiwe na makosa. Jambo hili lina ugumu wake kutokana na kuwapo kwa mambo yanayochochewa na mazingira anamoishi katika jamii (Senkoro, 1987). Katika makala hii, tumemchunguza mhusika nguli anayesawiriwa katika mazingira mbalimbali katika tamthiliya teule.

Mbinu na Mipaka ya Makala

Emanuel Mbogo ni miongoni mwa waandishi nguli wa tamthiliya ya Kiswahili katika jamii za Afrika Mashariki. Kazi zake zimejengwa kwa kuzingatia vigezo vya kihistoria, kiutamaduni, kifalsafa na kimaendeleo kwa kuzingatia muktadha wa utunzi wake unaodhihirisha mfungamano mahsusi uliopo baina ya wakati na jamii yake. Hali hii huwafanya wanataaluma wengi (Fadhili, 2014; Clemence, 2015; Mningo, 2015 & Shemweta, 2015) kuzishughulikia kazi zake kwa mitazamo na misukumo mbalimbali. Hata hivyo, kipengele kinachohusu taswira ya mhusika nguli katika kazi zake, hakijapewa uzito unaostahiki katika uhakiki wa kazi zilizoshughulikiwa. Pengo hili limechochea ari ya kutaka kukichunguza kipengele hicho ili kubaini taswira ya mhusika nguli katika maandishi yake. Ukusanyaji wa taarifa za msingi uliendeshwa kwa mbinu za usomaji wa matini teule kwa kurejelea tamthiliya za *Fumo Liongo* (2009) na *Sundiata* (2011). Data za upili zilikusanywa kwa mbinu ya kinyaraka ili kufafanua data za msingi zilizokuwa zimelengwa.

Mwega wa Uhakiki Kinadharia

Semiotiki ni taaluma ya mfumo wa alama katika mawasiliano ya kutumia lugha (Eco, 1976). Miongoni mwa waasisi wake ni Ferddinand de Saussure (Kimarekani). Nadharia hii inashughulika na ishara pamoja na uashiriaji katika kazi za kifasihi. Ishara zinazojitokeza katika fasihi huundwa na mtunzi kwa kuzingatia muktadha wa jamii na binadamu ndiye mtengenezaji wa alama zinazotumika katika mawasiliano yake ya kila siku (Mwangosi, 2019). Hadhira inayolengwa hutengeneza maana mbalimbali kupitia ubunifu na tafsiri zao juu ya alama na ishara inazokutana nazo katika kazi za kifasihi.

Nadharia hii ilitumika kuichunguza fasihi namna inavyohusiana na mazingira ya jamii. Aidha, fasihi ni usawiri mkamilifu ambao hayasawiri maisha kwa undani na huyachunguza kwa mtazamo mpana (Msokile, 1993). Hivyo, mtafiti aliichunguza jamii kuwa ni malighafi ya fasihina kwamba fasihi ina athari kubwa katika jamii inayohusika. Mwandishi wa vitabu teule aliwekwa katika muktadha wake wa kawaida, kweli na halisi ili kujua mwenendo na shughuli zake kwa kuwa kazi zake ni kiungo chake. Aidha, jamii iliyoandikiwa iliwekwa katika ulimwengu wake wa kawaida, kweli na halisi ili kufanya uhakiki wa kina kuhusu taswira zilizotumika na kupata yaliyomo. Pia, imetumika kuchunguza uhusiano uliopo baina ya fasihi na jamii kwa kurejelea vitabu teule vya *Fumo Liongo* (2009) na *Sundiata* (2011) vilivyolengwa katika makala hii.

Taswira ya Uhusika wa Mhusika Nguli katika Tamthiliya Teule

Taswira ni sehemu mojawapo tu ya vipengele vya fani katika kazi ya fasihi. Taswira ni uwasilishaji wa jambo, mawazo, dhana na hoja kwa njia ya vielelezo vinavyojengwa kwa maneno (Semzaba, 1997). Taswira ni mkusanyiko wa picha mbalimbali zinazoundwa na maelezo ya wasanii katika kazi za fasihi. Pia, ni picha zinazojitokeza baada ya matumizi mbalimbali ya semi na ishara. Picha hizo hujengwa kutokana na maelezo au tamathali za usemi alizotumia mwandishi (Wamitila, 2006). Taswira hujengwa kutokana na tajiriba za kila siku za jamii inayohusika kulingana na usawiri wa wahusika alioufanya mwandishi. Matumizi mazuri ya taswira hutegemea ufundi wa mtunzi wa kuweza kuchota mambo yanayomzunguka katika jamii yake.

Taswira hutazamwa kama maneno yanayotumiwa na wasanii wa kazi za fasihi ili kuchora picha kamili ya kitu, hali, wazo au uzoefu fulani wa jamii (Mapunjo, 2014). Pia, wanaainisha aina tatu za taswira. Kwanza, kuna taswira zinazoonekana ambazo hujengwa kwa kutumia vielelezo vinavyojulikana katika maisha ya kila siku ya jamii inayohusika. Pili, kuna taswira za hisi ambazo zina nguvu ya kuganda akilini na kunasisha ujumbe wa msanii kwa wasikilizaji au wasomaji. Tatu, kuna taswira za kufikirika zinazotokana na mawazo yanayohusu mambo yasiyoweza kuthibitishwa (Senkoro, 1987). Kwa hiyo, ulinganisho wa taswira zilizopo katika jamii husaidia kupata jibu la fumbo lililojengwa katika mazingira halisi.

Kuhusu uhusika wa mhusika, Wamitila (2010) anaeleza kwamba mhusika ni nyezo kuu ya fasihi kwa kuwa ndiye anayehusika kuyafanya matukio na matendo yanayopatikana katika kazi ya kifasihi. Matendo ya wahusika hao ndio nguzo kuu ya kuibua maudhui yanayoendelezwa katika kazi inayohusika. Uhusika wake unajidhihirisha kwa tabia na wasifu wake, sura yake, hisia zake na namna anavyofungamana na tajriba za wahusika wengine katika kazi ya kifasihi (Mhando, 2015). Wahusika hao lazima wafungamane na tajriba za jamii zao na mojawapo ya jukumu lao ni kuleta mabadiliko. Makala hii imechunguza taswira ya uhusika wa mhusika nguli katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo za *Sundiata* (2011) na *Fumo Liongo* (2009). Taswira za uhusika wa mhusika nguli zimejidhihirisha kwa namna mbalimbali katika tamthiliya teule kama ilivyoelezwa katika kipengele kinachofuata.

Taswira ya Shetani

Shetani ni malaika anayesadikiwa kuwa amelaaniwa kwa kukataa kufuata amri za Mwenyezi Mungu (TUKI, 2004). Pia, ni mtu mwenye vitendo vibaya. Taswira ya shetani inatazamwa kwa sura tofauti tofauti. Senkoro (2011) anaiweka taswira hii katika kundi la taswira ya viumbe visivyokuwa na mwili. Dhana ya shetani katika mfumo wa kaida za kijamii hutazamwa kuwa ni dhana dhahania. Hii hutokana na kuwa watu hufikiria tu juu ya kuwapo kwake, lakini hajawahi kuonekana dhahiri kwa wanajamii (Wamitila, 2008). Hata hivyo, ingawa shetani

hajawahi kujidhihirisha dhahiri, bado anatazamwa kama wakala wa maovu yote yanayoendelea katika jamii kama vile ajali, vifo, uasi, uadui, majanga na maradhi.

Katika tamthiliya ya *Sundiata* shetani amejengwa kitaswira kwa kuonesha hali na chanzo cha maovu mbalimbali katika jamii. Kutumika kwake kumezingatia misingi ya nadharia ya Semiotiki kuwa lugha anayoipata mtu huwa ni matokeo ya mwingiliano wa jamii. Wanajamii wengi wanamhusisha shetani na matendo maovu kwa mujibu wa imani zao. Kulingana na Furguson (1990), shetani kwa jina lingine ni pepo ambao daima hawana heri wala jema. Katika tamthiliya hiyomwandishi anamchora shetani kupitia katika matendo maovu yanayofanywa na mhusika Sumanguru kwa watu. Mwandishi anaeleza:

> *Hakuna awezaye kumuua Sumanguru. Huyu si mtu ni jini…kupigana na Sumanguru ni sawa na kupambana na Maimuna toka Uajemi. Hakuna binadamu awezaye kupigana na shetani* (Mbogo, 2011: 66 - 67).

Nukuu hii inaonesha ushetani wa Sumanguru unaotokana na matendo yake maovu kwa raia wake. Pia, inaashiria picha ya kutokuwepo kwa ushirikiano mzuri baina ya viongozi na raia wao kutokana na ukatili kwa watu wanaowaongoza. Raia huwaogopa viongozi kwa udhalimu uliokithiri na vitendo vya ukatili wanavyotendewa (Barthod, 1964). Vitisho hivyo, huleta ukimya kwa raia wasiweze kuongea kuhusu uongozi mbaya wakihofia usalama wa maisha yao. Massoud (2018) anaifananisha hali hii na namna Ukoloni ulivyokuwa umekithiri katika nchi za Kiafrika kwa ukandamizaji, ubadhilifu, wizi wa mali ya umma na unyonyaji, kuwa huo ndio ushetani wenyewe. Aidha, Sumanguru alidhihirisha ushetani wake alipomjibu waziri wake kuhusu ujumbe uliotoka kwa Dankarani aliposema:

> *Mwambie: Sumanguru, yule avaae viatu vya ngozi ya binadamu aiponda mikono yake ya suluhu. Sumanguru, yule mchawi wa wachawi akivisagasaga kwa guu lake la shaba, videvu vya hao mbwa wakapiga magoti ili kuibusu*

> *miguu yangu kwa suluhu… Sumanguru, yule Mfalme*
> *mfuga bundi, majoka na majini, ataipasua na*
> *kuichanachana kwa shoka…* (Mbogo, 2011: 27).

Sumanguru anatazamwa kama mchawi wa uchawi aliyekosa ubinadamu kutokana na udhalimu wake dhidi ya raia wake. Hata hivyo, Wafula (1999) anaitazama taswira ya shetani kwa kuinasibisha na itikadi za jamii nyingi za makabila ambazo humuonashetani kuwa ni kiumbe anayeogofya na hawezi kutawalika na binadamu. Taswira hii huashiria hofu ambayo huathiri utendaji kutokana na kutanda kwa ukimya kwa kuhofia kupata matatizo pindi mtu akiongea. Viongozi hawana budi kuepuka mitindo ya kuongoza jamii zao kwa udhalimu unaosababisha hofu kwa wananchi. Hali hii husababisha jamii kushindwa kujiamini na katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku kwani hufanya shughuli zao wakiwa ni wenye hofu kubwa.

Pia, taswira ya shetani imetumika kuashiria matendo ya udharirishaji wa kijinsia. Mwandishi anamtumia Sumanguru kama kiongozi aliyekithiri kwa vitendo vya udharirishaji kwa wanawake, hasa wake za watu. Sumanguru anapowatuma wanajeshi wake kwenda vitani, huku nyuma anaendeleza uovu wa kufanya mapenzi na wake wa maaskari waliopo vitani (Mbogo, 2011). Jambo hili limejitokeza pia katika *Biblia Takatifu* ambapo mfalme Daudi aliamuru jemadari wake (Huria) awekwe mbele kwenye mapigano makali ili auawe, kisha amuoe mkewe (*Mwanzo*, 4: 1-12). Huu ni ushetani uliokithiri, hasa unapofanywa na viongozi dhidi ya wananchi wake. Jambo hili halina budi kupingwa kwa nguvu zote.

Mfalme Sumanguru alidharirisha wanawake kwa kufanya nao mapenzi ya lazima bila idhini yao. Aidha, alifanya mapenzi na mke wa mpwa wake aliyemtuma vitani kuwakabili maadui wake. Malalamiko ya Keleye (msichana) ndiyo yanaijenga taswira ya ushetani wa Sumanguru na namna anavyofananishwa na uchu na tamaa ya fisi. Mwandishi anaonesha ulafi na tamaa ya kutamani kila kitu kinachoonekana mbele yake kwani alidiriki hata kuvuna mazao katika shamba lisilo lake. Taswira ya mnyama imetumika kudhihirisha tabia

ya ukatili inayotokana na kufanya mambo nje ya ufahamu wa akili na maisha ya binadamu. Kufanya hivyo kunachangia kuvunja heshima, migogoro na kuvunja mahusiano ya kidugu na kiutu katika jamii. Wananchi wanapoteza imani kwa viongozi wa nchi. Viongozi hawana budi kutenda mema kulingana na misingi ya haki na demokrasia (Dukore, 1974). Jambo la msingi kwa kiongozi ni kufuata misingi ya maadili, utu, haki na demokrasia.

Katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*, taswira ya shetani imesawiriwa kupitia kwa mfalme Mringwari, hasa anapokosolewa kuhusu uongozi wake mbaya. Mringwari alidiriki kutoa uhai kwa mtu yeyote aliyethubutu kumkosoa kwa kumwambia ukweli. Hali hii inatokana na viongozi wengi kulinda madaraka waliyopewa kikatiba ama kujinyakulia kwa nguvu kubwa, huku wakikiuka maadili ya uongozi na miongozo ya katiba ya nchi zao. Viongozi hawataki kukosolewa kama njia majawapo ya kujijenga na kuuimarisha uongozi wao. Mwandishi kupitia kwa Msheki anaeleza:

> *Waziri kiongozi… nyimbo za kukosoa viongozi lilikuwa jambo la jadi. Sasa vipi leo Liongo kufanya geni lisiloeleweka? Waziri kiongozi kwa nini tusiyapime yote haya kwa urazini wa fikira zetu badala ya kuruhusu hukumu na maamuzi yetu yatawaliwe na mihemuko ya damu na hisia zetu? Mimi msimamo wangu ni huo; hata mbele ya Daudi Mringwari ni huo, Liongo silioni kosa lake.* MRINGWARI alimjibu:*Mjinga mkubwa we! Punde si punde nitakuonesha kwa kuwa katika nchi hii ya Pate ni mimi tu ninayeweza kuchezea uhai na kupituapitua solo za ufu na uhai wa Wabajuni…. Huku utaka uhisani wa afadhari yangu, basi utaambulia ufidhuli wa ole ya nyongo yangu…* (Mazabania wanaingia, mavazi yao yakionesha kuwa ni wauaji). *Huyo! Mtalimbo toka utosini! Kisha mtoseni baharini* (Mbogo, 2009: 5 - 7).

Nukuu inaonesha matukio yanayoambatana na matendo ya maovu yanayofanywa na baadhi ya viongozi. Mfalme Mringwari

anapokosolewa aliona kama anadharauliwa, hivyo, alitoa adhabu ya kuuawa kwa Msheki kwa kuchomwa utosini kwa mtalimbo. Viongozi wasiojiamini na kutofuata sheria za uongozi wa kidemokrasia, hutumia mamlaka ya utawala, kupoteza maisha ya watu wanaowakosoa au kuwatosa vifungoni kama suluhu ya amani katika nafasi zao za uongozi (Mhando,1981). Kwa kawaida, amri zinazoambatana na matendo maovu ya viongozi kwa raia wao, hukwamisha na kutokomeza juhudi za kusimamia haki na maendeleo ya jamii.

Taswira hii imedhihirika kutokana na mfululizo wa matukio yanayosawiriwa na msanii katika kitabu chake. Mfalme Mringwari anaendeleza mauaji kwa kuweka mipango ya kuandaa sumu ya nyongo ya mamba itakayomuua Liongo kwa kuwa alikuwa mpinzani na tishio kwa manufaa ya cheo na utawala wake. Hulka ya viongozi wasiojiamini hutumia muda mwingi kulinda vyeo vyao kuliko kuweka mikakati thabiti ya uongozi bora unaozingatia haki, sheria na uwajibikaji (Fadhiri, 2014). Katika mazingira hayo, wanaharakati wengi wamekuwa wakitiwa nguvuni pindi wanapofichua uovu, ukiwamo ubadhilifu wa mali ya umma, uhujumu uchumi, ukosefu wa maadili ya viongozi na kuonesha mianya ya ukwapuaji wa fedha za umma kwa baadhi ya viongozi wasio wadilifu. Mwandishi anasema:

> MRINGWARI: *Wapi atakaa fisimaji yule?*
> W. KIONGOZI: *Hapa kwenye meza hii.*
> MRINGWARI: *Basi tia na koroga barabara.*
> W. KIONGOZI: *Anatia sumu ya nyongo ya mamba na kukoroga. Tayari.*
> MRINGWARI: *Basi na iwe hivyo. Tumelifuga joka hili tukutu katika tundu la ufalme wangu kwa muda mrefu. Ila sasa tutaliteketeza kwa moto, tuligeuze majivu baridi badala ya kulizika kiwiliwili* (Mbogo, 2009:20).

Data hii inaonesha kukithiri kwa utawala wa mabavu na uonevu katika jamii ya msanii. Hili ni tatizo kubwa tena lipokatika ngazi mbalimbali za kiutawala. Maelezo haya yanapewa nguvu zaidi na Omary, (2011)

kuwa watawala wa nchi za Kiafrika hawana budi kusimamia maendeleo ya maitafa yao, likiwamo suala la uongozi bora kwa kupambana na Ukoloni mamboleo, kutenda haki, kusimamia sheria na katiba, kuwajibika ili kuchochea ustawi wa jamii isiyo na mazonge yanayokwamisha maendeleo pia hawana budi kusimamia haki kwa kuzingatia uzalendo wa kuijenga nchi kulingana na mahitaji ya taifa. Viongozi wanapowakandamiza wananchi kwa kuwanyima haki zao za msingi husababisha matatizo makubwa katika jamii, mthalani kuishi kwa hofu, kukosa matumaini, imani na uzalendo mwisho wa yote ni huangukia katika uwanja wa chuki, uasi na visasi, mambo ambayo ni hatari kwa ustawi wa taifa.

Taswira ya Pazia la Pate
Pazia ni kitambaa chenye ukubwa fulani ambacho hufungwa dirishani, mlangoni au jukwaani kufanya sehemu ya ndani isionekane (BAKITA, 2017). Pazia hutazamwa kuwa ni kitu kinachokinga ama kusitiri kitu kingine kisiharibike au kisiharibiwe. Katika kitabu cha *Fumo Liongo*, Fumo Liongo anatazamwa kama pazia la Pate kutokana na nguvu aliyokuwa nayo katika jamii yake. Aidha, alitazamwa kama mlinzi wa jamii yake dhidi ya maadui kutoka katika jamii jirani zilizokuwa zikihasimiana ziogope kuivamia ovyo Pate. Kwa hiyo, kifo cha Liongo kilionesha hali ya kuanguka na kupotea kwa ulinzi wa jamii hiyo. Kuanguka ni kupotea kwa matumaini ya ustawi wa jamii yao.

Taswira ya pazia la Pate inaonesha kuwapo kwa hali ya uzalendo na ujasiri wa Liongo katika kupambana na maadui wa jamii yake. Kifo cha Liongo kinaleta hali ya kupotea kwa matumaini kwa jamii ya Pate kwa kuwa ulinzi wao ulikuwa umeondolewa, nchi ilibaki tupu, hawakuwa na tegemeo tena bali walijawa huzuni na hofu ya kuvamiwa na kushindwa kwa urahisi dhidi ya maadui zao. Katika sintofahamu hiyo, mfalme anaonesha hali ya kukithiri kwa viongozi dhalimu waliojaa ubinafsi, uchu wa madaraka na kutanguliza maslahi yao mbele badala ya mataifa yao wanayoyaongoza (Chuachua, 2011). Kifo kwa Liongo kilisababisha kutanda kwa hofu miongoni mwa jamii ya Pate kwani waliona kama wametelekezwa katika himaya ya Mringwari

iliyokuwa imetanda giza la kila udhalimu. Mwandishi akionesha hofu hizo anasema:

> *Lakini huku nyuma, baba yetu Liongo umetutelekeza sisi wanao. Tumebakia wakiwa, yatima. Hekima uliyotuunganisha nayo imezimika. Wabajuni sasa tunatapatapa gizani. Tunatweta mkabala na lango la kinywa cha mamba wa Ikulu* (Mbogo, 2009: 49).

Katika nukuu hii, hofu imetanda kwa wananchi wakihofia kurudi kwenye mateso ya mfalme Mringwari ambaye hulinganishwa na hali ya kukikabili kinywa cha mamba, yaani maangamizi kutokana na ukatili wake. Hali hiyo ndiyo hutazamwa kama kuwarudisha raia katika hali ya ukandamizwaji wa Kikoloni, hasa Ukoloni mamboleo. Pia, kuanguka kwa pazia linalinganishwa na vifo vya viongozi maarufu, wakiwamo waasisi wa mataifa mengi ya Kiafrika waliopigania uhuru kutoka katika mikono ya utawala dhalimu wa Kikoloni (Beja, 1988). Mwandishi akionesha kuanguka kwa tegemeo la Wapate, anasema, 'Fundo hili, sasa wadhalimu hawa wamelikata. Oh! Tazameni Wabajuni. Pazia la taifa la Pate sasa limeanguka chini; na Pate imebaki utupu' (Mbogo, 2009: 45).

Matumaini yaliyotarajiwa na raia katika mapambano dhidi ya uongozi dhalimu yalizima ghafla kama mshumaa unavyoweza kuzima ukimwagiwa kopo lililojaa maji. Hali ya kuanguka kwa pazia ndiko kumesababisha jamii kujiona kama imebaki bila ulinzi kwamba hakuna tena kitu kitakachoweza kuwasitiri katika ustawi wa maisha yao. Hali hii inalinganishwa na tangazo la kifo cha aliyekuwa raisi wa Zimbabwe, Robert Gabriel Mugabe lililotolewa na raisi Mnangagwa kwamba Robert Mugabe, atakumbukwa na kutazamwa kama Baba wa Taifa na Mwanga wa Mapinduzi, Mwana Umajumui wa Afrika ambaye aliyatoa maisha yake yote kuipigania na kuikomboa Zimbabwe ili kuleta maendeleo, utulivu na ustawi kwa raia wake (Mgogo, 2012).

Kifo cha Mugabe kilitazamwa kama anguko la pazia la Wazimbabwe wote kwa kuwa alikuwa nguzo kubwa katika kupigania na kuilinda

Zimbabwe. Mugabe hakupenda kuona Afrika ikinyonywa na kutumikishwa kwa namna yoyote na Mabeberu. Hivyo, kifo chake kiliacha pengo kubwa kwani uzalendo, ushujaa na uzoefu wake ulitegemewa katika kutoa miongozo ya namna ya kuiongoza na kuisimamia nchi ili kuleta maendeleo na ustawi katika misingi ya haki na demokrasia ya kweli. Mbonde (2002) anazungumzia suala la utupu kuwa ni dhana inayoashiria uduni wa maisha. Uduni huo huweza kusababishwa na teknolojia na uvumbuzi duni kuhusu maendeleo na ustawi wa jamii, hayo ni miongoni mwa mambo yaliyopiganiwa na Liongo. Taswira hii ni fundisho kwa kizazi kilichopo na vijavyo kuwa na tabia ya uzalendothabiti kwa ajili ya ujenzi wa taifa.

Taswira ya Simba
Taswira ya simba katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* imetumika kumaanisha kiongozi shupavu wa kijadi. Pia, humaanisha mwanamume mwenye nguvu za aina yake ambaye hupata ushindi katika kila tukio inalohusisha matumizi ya nguvu. Taswira hii inaonesha kuwa ukali wa simba ndio unaosababisha aogopwe na wanyama wengine. Aidha, katika tamthiliya hii imetumika kuonesha namna Liongo alivyokuwa shupavu, hakuogopa wala kutetemeshwa na adui yeyote. Mama yake alimtahadharisha kuwa aache kukinzana na kupambana na mfalme Mringwari kwa kuwa anaweza kumuua kutokana na ukatili aliokuwa nao dhidi ya raia wake. Liongo hakujali na alimtazama mfalme Mringwari mjinga aliyemudu kuwatetemesha mabanati. Hivyo, Fumo Liongo alitazamwa kama Simba wa Pate (Mbogo, 2009: 14).

Suala la Liongo kuogopwa na maadui wa Wabajuni lilitokana na tabia ya msimamo wake wa kukemea matendo maovu katika jamii yake. Pia, aliogopwa kutokana na uwezo wa nguvu zake za ajabu alizokuwa nazo za kuwakabili maadui na kuwashinda. Hata hivyo, mfalme Mringwari, pamoja na vitisho vyake kwa raia, alionesha wazi kumwogopa Liongo na kuhofia kunyang'anywa madaraka yake kama anavyobainisha mwandishi "Mbwa huyu, licha ya kuwa ananilindia nyumba na mali yangu dhidi ya wanyang'anyi, lakini nahofia meno yake yanayozidi kuchongoka kila uchapo" (Mbogo, 2009: 8). Liongo alikuwa na uwezo wa kuwatokomeza maadui wote wanaotaka kumchezea.

Pia, katika tamthiliya ya *Sundiata*, taswira ya simba imetumika kudhihirisha ujemadari wa Sundiata katika vita. Katika mapigano yote ya kivita, Sundiata alionesha uhodari wa kupigana bila kukata tamaa; hatimaye, alishinda kwa kuwaangamiza maadui na kuwachukua mateka. Mwandishi anaonesha jinsi mfalme Tunkara alivyofurahia ushindi kwa:

> *Sote tumefurahia ushindi huu, mateka na ngawira tumechukua. Yote haya ni sababu ya jemadari wetu Sundiata, Simba wa vita." Vita vilikuwa vigumu…lakini …moto uliwaka! Sundiata, farasi na upanga vilielea hewani, vichwa vya mahasidi vikitemwa na kuachana na miili yao… na wakati wote Sundiata alitutia moyo tusonge mbele* (Mbogo, 2011: 36).

Aidha, data imeonesha uwezo wa jeshi kuwa na nguvu na kumfanya adui akimbilie msituni akajifiche kutafuta hifadhi ili kuyanusuru maisha yake. Mfalme Sumanguru anaonekana kuukimbia mkono wa Simba wa Mali – Sundiata ambaye anamsaka ili amwangamize. Hivyo, majeshi ya Sundiata yaliweza kupigana vikali na kuwashinda maadui wao.

Taswira ya Kisu na Sindano

Kisu ni kifaa kinachotumika kuingizia dawa kwenye mwili wa binadamu. Kisu huweza kuleta ustawi, utengamano, maangamizi na uharibifu. Katika tamthiliya ya *Sundiata*, kisu kimetumika kama siraha ya maangamizi kwa nyakati hizo, ikilinganishwa na bunduki ambayo ni siraha kali ya katika maisha ya leo. Kisu alichopelekewa mfalme Tunkara kama malipo ya ardhi, kimesawiri maangamizi atakayofanya Sundiata kwa Tunkara ili kulipa kisasi. Kisu kimetumika kuimarisha tabia ya ubinafsi wa tamaa ya madaraka. Mwandishi anamwonesha Sassuma anavyojitoa mhanga kufanya maandalizi ya kupata kisu ili amuue Sundiata kwa kusudi la kuhakikisha mwanae Dankarani anakalia kiti cha ufalme. Mwandishi anaeleza:

> *Nahitaji kisu. Kisu kifupi, imara, chenye ncha kali… kwa ajili ya mwananngu Dankarani, …alivyovaa hatambuliki. Anamsogelea Sundiata; Sassuma anamvika taji kwa mkono wa kushoto na kumchoma kisu mara tatu kwa mkono wa kulia… (anampiga kisu binti yake) na wewe mbegu haramu, kufa, umfuate kiwete kuzimu. Nana anaanguka anakufa; na Sundiata anayumba kwa uchungu anakufa* (Sundiata, 2011: 74).

Kisu kutumiwa kama siraha ya kupigania madaraka kwa maslahi binafsi. Suala la kupigania madaraka kwa kutumia silaha limekuwa ni janga sugu katika bara la Afrika. Mwitikio wa mahitaji ya kutumia silaha kali za kisasa ni mkumbwa kama ilivyo mvutano baina ya Marekani na Korea Kaskazini, ambako kumekuwa na migongano ya kisiasa na kiuchumi. Kwa ujumla, taswira zilizorejelewa katika vitabu hivi ni matukio na matendo ya msingi katika jamii iliyochunguzwa. Suala matumizi ya silaha limekuwa likileta madhara makubwa ya ukiukwaji wa haki za binadamu yakiwamo mauaji, uharibifu wa mali ya umma na raia, kuongezeka kwa wakimbizi, ubakaji na ukatili wa kingono kwa raia. Pia, wananchi wamekuwa wakiporwa na kupoza mali zao kama nyumba, mashamba na mifugo.

Taswira ya sindano ya shaba katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* ilitumikakuashiria ulinzi wa nguvu za kisihiri za Fumo Liongo katika harakati zote za mapambano dhidi ya maadui zake. Mbijima (2011) anasisitiza kuwa shujaa lazima awe na kinga inayomlinda dhidi ya maadui. Kinga hiyo huambatana na nguvu za sihiri ambazo zina uwezo wa kugeuza mikuki, pinde na mishale ya adui kuwa kichuguu ili kuepuka kupata madhara yaliyoelekezwa kwake. Liongo hakuweza kunaswa kwa mtego wa aina yoyote ule kutoka kwa adui zake kutokana na nguvu za sihiri alizokuwa amesheheni. Wena kiongozi kutoka ikulu anathibitisha:

> *Huyu mtu si mtu,…ukimnasa kwa ulimbo, atajinasua kwa fimbo tu. Ukimng'ata kwa meno, yeye atajinga'atua kwa maneno tu….mara ngapi*

> *tumeviamuru vipapasio vyetu vya nchi viende kumfanyia mitego?... Lakini siku zote Liongo mitego ameitegua. Lazima tuibukue siri inayozilinda nyota za uhai wake* (Mbogo, 2009: 4).

Liongo kama shujaa katika tamthiliya hii anamthibitishia mwanae Zahidi kuwa hawezi kuuawa kirahisi kama mawaziri wanavyomtafuta. Liongo alimwambia mwanae kwamba Zahidi mwanangu, mimi ni Fumo Liongo. Mimi ni Simba wa Pate. Hakuna mwingine yeyote ajuaye siri ya ufu wangu ila mimi na Muumba wangu. Mimi mkuki hauniui, shoka haliniui, mshale hauniui na kisu hakiniui. Kitu chochote hakiniui. Ila ukitaka kuniua fanya bidii utafute sindano ya shaba (Mbogo, 2009). Kwa kawaida, shujaa lazima awe na maadui ambao hawafurahishwi na utendaji harakati za shujaa.

Hapana shaka matokeo ya madaraka yenye kuendekeza usaliti na uovu yamekuwa chanzo cha kukwamisha maendeleo na ustawi wa jamii. Taswira ya sindano ya shaba imetumika kama silaha ya kumwangamiza Liongo ambaye alikuwa akitafutwa kwa muda mrefu bila mafanikio. Mwandishi anamwonesha mwanae Zahidi anamnyemelea na kumchoma Liongo sindano ya kitovuni na kukimbia. Ubinafsi wa viongozi umewafanya kutumia madaraka na nguvu za kisiasa na kiuchumi vibaya kwa kufikiri kuwa wao ni bora zaidi kuliko wananchi (Wafula, 1999). Hali hii ndiyo inayojenga tabia ya baadhi ya viongozi kukataa na kutopenda kushauriwa ama kupokea maoni ili kulinda maslahi binafsi kwa kupuuza mtazamo mpana wa mahitaji ya taifa.

Taswira ya Taji
Taji katika tamthiliya ya *Sundiata* limetumika kuashiria madaraka ama mamlaka aliyonayo mtu. Taji ni vazi linalovaliwa kichwani au shingoni analovishwa mshindi, vazi linalovaliwa kichwani aghalabu na mfalme au malkia (BAKITA, 2017). Taji huwa linashindaniwa. Taswira ya taji katika tamthiliya ya *Sundiata* imesawiri mapambano makali ya motifu ya msako wa madaraka kati ya Sundiata na Dankarani. Gichamba (2005) anaeleza kwamba ingawa shujaa hutoka katika ukoo bora, mara nyingi hakipati cheo cha ufalme hivi hivi tu. Shujaa sharti akitetee au

akipiganie cheo chake kadiri anavyoweza kwa kuzingatia taaratibu na misingi ya uongozi, haki na wajibu katika jamii (Omar, 2011).

Pia, taswira ya kugombaniwa kwa taji baada ya kifo cha baba yao imeonesha visa vingi vya kisihiri na kutishiana kuuana hadharani. Sundiata anaona kuwa, yeye ndiye mrithi halali wa kurithi taji kwa misingi ya kiutamaduni. Dankarani kwa kuliona hilo, wanaungana na mama yake Sassuma kunyakua madaraka kwa nguvu. Mambo kadhaa yaliyofanywa na Sassuma ili kuhakikisha wanapata taji na kumiliki kiti cha ufalme. Kwanza, Dankarani anaungana na Sassuma mama yake kutumia sihiri kwa kuweka uwete kwa Sundiata tangu akiwa mdogo ili asije kupata taji hilo. Pili, Sundiata anapoonekana amepona, walifanya uchawi wa kutambika njia panda ili akipita auawe kwa kafara waliyoifanya njia panda. Tatu, kumuua Sundiata kwa kumchoma kisu tumboni. Haya yote ni mahangaiko ya kupigania taji la ufalme.Sassuma aliona hakuna mtu yeyote anayeweza kuvaa taji la ufalme ila mwanae Dankarani. Aliamua kupambana kwa mbinu zote kama vile rushwa, uchawi na kuua ili apate nafasi kwa ajili ya mwanae Dankarani. Kwa kufanya hivyo, hali hiyo iliibua mizozo iliyochangia kurudisha nyuma maendeleo ya jamii.

Taswira ya Ndoto
Ndoto ni mfuatano wa picha, mawazo, hisia zinazotokea bila hiyari kwenye akili za mtu usingizini . Barrett (2007) anaeleza kuwa ndoto ni mbinu mojawapo ya kutatua matatizo kwani kupitia kwazo mtu anaweza kudokezwa jambo fulani linalohusiana na suala alilonalo na huweza kumpatia mbinu za kutoka katika tatizo hilo. Mtu huweza kupewa maono ya namna atakavyolishughulikia jambo fulani. Katika *Bibilia Takatifu*, Yusufu aliyetafsiri ndoto za Farao ambazo zilihusu janga la njaa litakalotokea katika nchi ya Misri kwa miaka saba. Yusufu alitoa ushauri kwa Farao kuhusu umuhimu wa kuhifadhi chakula ili kulikabili na janga hilo. Farao, akatii wakaweka akiba ya chakula cha kutosha. Ndoto ni mbinu ya kimtindo ambayo hutumika kumtoa msomaji katika ulimwengu halisi uliozoeleka na kumpeleka katika ulimwengu wa kinjozi baina ya ujenzi wa jamii mpya na

vikwazo vyake (Massoud, 2018). Mwandishi anaonesha mlolongo wa ndoto ya Liongo akimsimulia Zahidi akisema:

> *Usiku wa jana haukuwa usiku mzuri kwangu. Nilifadhaishwa na ndoto iliyojirudia mara kwa mara kila nilipoamka na kurudi tena usingizini. Katika ndoto, kilikuja kivuli cha sura ya nusu ya mtu, nusu mnyama, kikazikwapua silaha zangu, na sikuwa na nguvu za kukizuia wala kukifukuza kivuli hicho. Lakini nilipozinduka kwa taharuki nikazikuta silaha zangu zi salama* (Mbogo, 2009: 42).

Ndoto hii inaashiria kuwa Liongo alikuwa anapokonywa uhai na nguvu za kisihiri alizokuwa nazo. Kupokonywa silaha zake kulionesha kupokonywa madaraka yake na nafasi yake ya kupigania haki za Wapate. Maana kamili inajidhihirisha pale Liongo anapouawa kwa kuchomwa sindano kitovuni kupitia kwa mwanae aliyemtembelea msituni. Zahidi alimvizia baba yake akiwa amelala na kumchoma sindano ya kitovu na kukimbia. Mwandishi anahimiza umuhimu wa kuzitafsiri ndoto ili kuepuka changamoto zinazoweza kuepukika. Liongo angeweza kuitafsiri vizuri ndoto yake angechukua tahadhari na kuepuka mauti yake. Pia, imeelezwa (*Mwanzo*, 41: 32) kwamba ndoto ya Farao kwa vile ilivyokuja mara mbili, ni kwa sababu neno hilo Mungu amelithibitisha na atalitimiza upesi. Nyutu (2016) anaeleza kwamba ndoto huwa na maana kwa mwanadamu. Hivyo, haipaswi kupuuzwa.

Taswira ya Damu

Katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*, taswira ya damu imetumika kudhihirisha mapisi ya kurithisha amali za jamii kwa kizazi kilichopo baada ya Liongo kufariki. Katika imani za kidini, damu huelezwa kuwa ina uwezo wa kunena na inakisiwa kwa kuwa kuna damu inayonena mema na mabaya. Damu ya Habiri iliweza kulaani muuaji Kaini (*2 Samwel* 11: 1- 17). Pia, damu hutumika kuwa ukumbusho wa jambo muhimu kama Wakristo wanavyotumia Sakramenti Takatifu wakiamini kuwa wanafanya ukumbusho wa matendo mema ya Yesu Kristo na

kukumbuka ukombozi wake kwao kwa kujitoa mhanga kufa kwa ajili ya mwanadamu mwenye dhambi. Mwandishi ameonesha uzito wa kuithamini damu ya Liongo kama urithi wa uzalendo, hekima na ujasiri kwa wananchi na vizazivitakavyofuata. Anaeleza:

> *Tazameni hata sasa bado ninayo damu ile ya thamani iliyomwagika pale pangoni alipochomwa sindano ya shaba kitovuni. Ichukueni muione! Ibusuni. Jipakazeni mwilini. Ichukueni mkaifanye mbolea mashambani na makondeni mwenu. Gawaneni, muihifadhi ili vizazi vijavyo vije viishuhudie na kusujudia ushujaa wa pekee wa Fumo Liongo* (Liongo, 2009: 46).

Data hii inaonesha kuwa kifo cha Liongo aliyesheheni matendo ya kizalendo na kijasiri yanayosisitizwa na kuhimizwa huchukuliwa kuwa ni ni mfano mzuri wa kuigwa kwa vizazi vilivyopo na vijavyo katika jamii zetu. Maisha ya Liongo hayana budi kurithishana ili kujenga hali ya kuwa na ujasiri na uzalendo katika shuguli zitakazoleta maendeleo na ustawi wa jamii na taifa kwa kutenda haki na kupinga uongozi usiozingatia sheria na haki. Jamii haina budi kujenga misingi imara ya kuendeleza maadili na uzalendo ili kuimarisha jamii yenye utu, maadili, uzalendo na ujasiri. Makala hii inatoa wito kwa jamii kuwa na moyo wa uzalendo, mshikamano kwa kuepuka usaliti, uchu wa mali na madaraka, visasi na ukatili ili kujenga jamii yenye ustawi katika fani zote za maisha.

Hitimisho

Kwa ujumla, makala hii imebaini kuwapo kwa taswira ya uhusika wa mhusika nguli katika tamthiliya teule. Matukio na matendo ya kishujaa ya kila nguli yamewekwa wazi kupitia taswira zilizomo. Mjadala wa data zilizowasilishwa umeonesha nafasi ya taswira ya uhusika wa mhusika nguli inavyojidhihirisha kupitia matendo yao ya kishujaa yanayofanywa katika harakati zao za kiutawala, kimaisha na kiwakati. Uhusika wao, kwa namna tofauti tofauti, unatazamwa kama maktaba mahsusi ya urejelezi wa masuala ya kijamii; na kiungo thabiti cha kiasili kinachojenga mfumo wa kuifunza, kuiimarisha na kuiweka

jamii pamoja katika misingi ya utamaduni na falsafa nzima ya maisha tangu kale mpaka sasa. Kipekee, suala la uzalendo limepewa nafasi kubwa katika harakati za usimamizi na ujenzi wa jamii yenye ustawi katika fani zake zote za kiutawala, kimaisha na kimaendeleo.

Marejeleo

Ali, S. K. (2017). Kuchunguza Matumizi ya Lugha na Dhamira Katika Tamthiliya Teule za Mwandishi Emmanuel Mbogo. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Barthod, O. (1964). *History of the World Theatre*. New York: Frederick Ungar Publishing Co.

Beja, S. K. (1988). Maudhui ya Ujamaa katika Riwaya za Tanzania. Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Campbell, J. (1968). *The Hero with a Thousand Faces*. New York: Princeton.

Chama cha Biblia Tanzania. (1997). *Biblia Takatifu*. Dodoma: Chama cha Biblia Tanzania.

Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Clemence, S. M. (2015). Kuchunguza Mbinu za Kitanzia za Ki-Aristotle Katika Tamthiliya za Fumo Liongo na Sundiata. Tasinifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Daniel, Z. L. (2012). Nadharia ya Ubaada-Ukoloni Katika Tamthiliya ya *Amezidi* (1995) ya Mohamed Said. Kioo cha Lugha, Juz.10. Dar es Salaam: TUKI.

Dukore, B. F. (1974) . *Dramatic Theory and Critisim*. New York: Holt, Rinehart, And Winston, Inc.

Eco, U. (1976). *A Theory of Semiotics*. Bloomington: Indiana University Press.

Fadhiri, F. E. (2014). Kuchunguza dhima ya mtindo katika Tamthiliya za Kihistoria: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya za *Morani* na *Kinjekitile*. Tasinifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Gichamba, J. M. (2005). Sifa za Mashujaa na Umuhimu Wao kwa Jamii Zao: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu. Tasinifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Isakwisa, C. (2003). Nyimbo za Harusi za Wanyakyusa na Mabadiliko ya Jamii. Tasinifu ya Shahada ya Kwanza. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Lighola, M. (2004). Athari za Sayansi na Teknolojia Katika Vitendawili vya Kigogo (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mapunjo, G.C. (2014). Usawiri wa Mwanamke Kama Kiongozi Katika Tamthiliya: Uchunguzi wa Kivuli Kinaishi na Nguzo Mama. Tasinifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Massoud, H. S. (2018). Kutathimini Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya Mfadhili. Tasinifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Mbijima, R. J. (2011). Dhima ya Visasili katika Kabila la Wagogo. Tasinifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mbogo, E. (2009). *Fumo Liyongo*. Dar es Salaam: Dar esSalaam University Press.

Mbogo, E. (2011). *Sundiata*. Dar es Salaam: TUKI.

Mbonde, J. P. (2002). 'Uchambuzi na Uhakiki' katika 'Janga Sugu la Wazawa'. Swahili Forum 12 (2005): 81 – 93.

Mgogo, Y. P. (2017). Kuchunguza Hadithi za Wanyiha katika Kurithisha Elimu ya Jadi. Tasinifu ya Uzamivu. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mgogo, Y. P. (2017). Kuchunguza Hadithi za Wanyiha katika Kurithisha Elimu ya Jadi. Tasinifu ya Uzamivu. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mhando, R. E. (2015). Kuchunguza Dhamira za Kijamii Katika Tamthiliya ya Kiswahili: Mfano wa Tamthiliya ya Hatia ya Penina Mlama. Tasinifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mligo, E. S. (2015). *Utandawazi katika Mazingira ya Kanisa la Tanzania* (Hakijachapishwa). Mbeya: Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

Mnigo, R. A. (2015). Tathimini ya Mwingiliano Matini katika Utunzi wa Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya ya Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo. Tasinifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili*. Dar es salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mwangosi, G. (2019). Kuchunguza Dhamira na Fani Katika Nyimbo za Magosi za Jamii ya Wanyakyusa. Tasinifu ya Uzamivu. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Msokile, M. (1991). *Uchambuzi na Uhakiki: Lina Ubani*. Dar es Salaam: Dar es Salaam Publishers Press.

Muhando, P. (1981). *Sanaa za Maonesho katika Jamii za Kijadi katika Urithi wa Utamaduni Wetu*. Dar Es Salaam: TPH.

Raymond, W. (1966). *Modern Tragedy*. London: Chatto & Windus.

Semzaba, E. (1997). *Tamthiliya ya Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Senkoro, F. E. M. K. (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publication Centre.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.

Shemweta, G. (2015). Itikadi katika Tamthiliya za Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo. Tasinifu ya Uzamivu. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Shule, V. (2010). Beyond Sociolism: Tanzanian Theatre, Neoliberalism and Foreign Aid Complex. A Thesis of Doctor of Philosophy (Unpublished). Mainz: Johannes Gutenberg Universitat.

Wafula, R. M. (1999). *Tamthiliya, Historia na Maendeleo Yake*. Nairobi: JKF.

Wamitila, K. W. (2006). *Uhakiki wa Fasihi*. Mombasa: Phoenix Publishers Limited.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide - Muwa Publishers Limited.

Wamitila, K. W. (2010). *Kichocheo cha Fasihi: Fasihi simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Publications.

The Contributions of University Students in Poverty Alleviation: A Case of Iringa Municipality in Iringa Region

Danny Mdage
Department of Humanities, Ruaha Catholic University
Email: *mdagedanny@gmail.com*

Abstract
This paper aimed at examining the contributions of university students within Iringa Municipality in poverty alleviation. It is based on the survey conducted in January 2020 in three universities found in Iringa Municipality namely Ruaha Catholic University, University of Iringa and Mkwawa College of Education (Constituent College of University of Dar Es Salaam). The objective of the study is to examine the linkages between university students and poverty alleviation within Iringa Municipality. The paper employed a case study research where a qualitative research was used to gather in-depth information on the contributions of university students in poverty alleviation. A purposive sampling was used to obtain twenty where fifteen members were selected from universities and five members from service providers from the list of 150 who were involved in the study. Simple random sampling and stratified sampling was involved to obtain the respondents for focus group discussion (FGDS). In-depth interview were conducted to collect the information. The three universities have approximately above thirteen thousand students. The findings of the study indicated that, university students contribute for poverty alleviation in Iringa Municipality through expansion of settlements or urbanization, per capita income, acquisition of physical properties, education for their children and remittances to the areas of origins to some migrants. Therefore, Universities students should not be treated as merely students but as important stakeholders for poverty alleviation in Iringa Municipality.

Key Words: University, Students and Poverty Alleviation.

Introduction

Jaspers (1965) states that, the university is a place for search of truth. Truth requires systematic methods of research which a foremost concern of a university. The second purpose of university is teaching, the research truth must be transmitted through teaching. The third, function that is culture or reflection of the community. In short, teaching, research and consultancy are key functions of any University in the World. The presences of universities in any part of the World, Iringa Municipality in particular, play significant contributions for the individual and national development through identified roles. For example, in Africa, the university is suppose to perform a developmental functions as centre for knowledge (pursuit, promotion and disseminations), research, provisions of intellectual leadership, manpower development, promotion of social and economic modernization and intercontinental unity (Ndlovu - Gatshen, 2017).

Iringa Municipality in Iringa region is blessed to have three predominant universities namely; Ruaha Catholic University (RUCU), Iringa University and Mkwawa College of Education (MUCE). The presence of these institutions within Iringa Municipality have changed development tremendously and hence, alleviation of poverty among the dwellers. The areas in which the University students contribute for poverty alleviation to dwellers of Iringa Municipality are restaurants, hotels and other areas in which are specialized in food issues. The communities around these universities have established and specialized in provision of food services to students. Most service providers are specialized in chips snacks which are the loveliest food for most students. Therefore, in return they earn reasonable income necessary for poverty alleviation.

Shops, through involvement in selling clothes, shoes, phones and other accessories. The university students contribute very much through buying the identified goods and others. Income from the activity contribute very much for the individual development within Iringa Municipality, and hence, poverty alleviation. Saloons, most of the university students are key users of saloons which are within Iringa

Municipality. Female students contribute very much compared to male students. No doubts dwellers with these facilities benefit much out of the university students.

Stationeries, where the communities around the universities are involved in providing services to students' pertained to printing and photocopying the academic materials such as books, pamphlets, class lecture notes and hand outs. This is second major enterprise after restaurants and hotels where the majority of the dwellers are doing into small scale. On the other hand, transportation, mostly daladala, tricycles and motorcycles are important forms of transport within Iringa Municipality. Youth are employed in providing services to universities students; in return they earn income necessary for alleviation of poverty. Most idle and restless youths have been employed particularly in tricycles and motorcycles operations. This has reduced to some extent crimes in the streets of Iringa Municipality.

Financial institutions and communication companies, within Iringa Municipality there are several financial institutions operating such as Banks namely; National Microfinance Bank (NMB), CRDB, National Bank of Commerce (NBC), Mkombozi Commercial Bank, Tanzania Postal Bank (TPB), Exim and Diamond Trust Bank. However, important transactions are carried out through mobile companies such as Tigo (Tigo - Pesa), Vodacom (M - Pesa), Airtel (Airtel-Money), Halotel (Halopesa) and very little carried out through Tanzania Telecommication Company Limited (T-Money). Also, the university students buy airtime for communication for social media such as twitter, facebook and whatsapp. All these contribute for individuals and Iringa Municipality in general in poverty alleviation.

House renters and agents, the universities within Iringa Municipality have inadequate accommodation facilities due to increase number of enrolment. Most of the students fall in the trap of looking houses for accommodation. The classes of house agents have been created to facilitate the smooth house renting processes. Therefore, university,

students have   contributed to creation of employment and income in general.

Statement of the Problem

Most of research on poverty alleviation don't recognize the contributions of the university students in poverty alleviations, it only focus on the role of university as development functions particularly, centre for knowledge (pursuit, promotion and disseminations) research, provision of intellectual leadership, manpower development, promotion of social and economic modernization (Ndlove, 2017). Therefore, the paper focus on the contributions of university students in poverty alleviation particularly in Iringa Municipality.

The Study Area

The study was carried out in Iringa Municipality in Iringa District which is one of the four Districts of Iringa Region, others are Kilolo, Mufindi and Iringa rural District. The selection of Iringa Municipality in Iringa District was based on the fact that it the only district with all universities. Iringa Municipality administratively is divided into 18 wards namely; Gangilonga,Igumbiro, Ipogolo, Kitwilu, Ilala, Isakalilo, Kahesa, Kitanzini, Kwakilosa, Makorongoni, Mvinjeni, Mkwawa, Mlandege, Mshindo, Mtwivila, Nduli, Ruaha and Mwangata. However, the study was carried out in three wards with Universities. Mkwawa ward with Mkwawa College of Education (Constituent College of the University of Dar es Salaam), Gangilonga ward with Ruaha Catholic University (RUCU) and Kihesa ward with University of Iringa.

The study is a case study research where qualitative research approach was used to provide a detail information about the contributions of university students in poverty alleviation in Iringa Municipality. Content analysis was employed to provide a general knowledge of the quantified content of the text (Denscombe, 2010). The purposive sampling was used because it relies on the judgment who to ask in selecting people who were likely have necessary information. Therefore, the sample size of twenty respondents out of 150 involved in

the study were used which is twenty percent as above minimum suggested by Kothari (2014).

The stratified sampling was used to obtain respondents for the focus group discussion. Two focus group discussion were conducted involved 6 to 8 respondents. The selection of the members were based on age, sex and education, marriage and how they involve in the study problem. In-depth interviews covering one hour was used to 20 consisting of university students and service providers involved. Finally, the analysis process was involved. Primary and Secondary data were involved in the study. Primary data were collected from the field through in-depth interview and focal group discussion. Secondary data were obtained from the documentary sources such as books and journals.

Findings and Discussion: Demographic Characteristic of the Respondents
Makala hii inalenga kuchambua maumbo yanayobeba dhana ya jinsia katika lugha ya Kimalila inayozungumzwa mkoani Mbeya katika wilaya ya Mbeya Vijijini. Kwa mujibu wa Guthrie (1967 - 1971) lugha ya Kimalila imewekwa katika kundi (M24). Suala la uhusiano uliopo kati ya lugha na jinsia limewavutia wataalamu wengi kufanya tafiti zao kuhusu jinsia (Corbett, 1991; Southerland na Katamba, 2011; Mastropavlou na Tsimpli, 2011; Jakiela na Ozier, 2019 kwa kutaja baadhi). Neno jinsia linaweza kufafanuliwa kwa namna tatu (Yule, 2006). Kwanza, huzingatia msingi wa kibaiolojia ambapo kunakuwa na tofauti kati ya mwanamke na mwanaume. Tofauti hizi zinapatikana karibu katika lugha zote. Pili, ni jinsia ya kisarufi inayohusu uwepo wa tofauti za hali ya kiume au kike. Aina hii inatajwa kuwa ni ya kufikirika zaidi kwa vile iko akilini mwa watumiaji wa lugha. Tatu, ni msingi wa jinsia ya kijamii ambapo mwanamke anatazamwa kutokana na nafasi yake katika kushiriki kwenye masuala ya kijamii. Kwa mfano, haki zake, utawala, kazi, mavazi na ndoa. Tofauti za kijamii zinachagizwa na muingiliano uliopo kati ya lugha na utamaduni, yakiwemo masuala ya kijinsia (Southerland na Katamba, 2011). Makala hii inajikita zaidi katika mtazamo wa tatu unaonesha jinsi lugha inavyoathiriwa na masuala ya jinsia katika jamii.

Corbett (1991) amependekeza namna tatu za kuielezea dhana ya jinsia. Kwanza, kama mfumo wa kisemantiki unaojikita zaidi katika maana ya jinsia kwenye nomino. Kwa mfano, uwepo wa sifa za viumbe hai dhidi ya visivyo hai, ubinadamu dhidi ya usibinadamu na mwanaume dhidi ya mwanamke. Tofauti hizi zimejengeka katika msingi wa maana zaidi. Pili, ni mfumo wa kisemantiki wenye uvulivuli. Kwa mujibu wa Corbett, tofauti na ilivyo katika mfumo wa kisemantiki, mfumo huu unakuwa na vighairi vingi vinavyoruhusu matumizi ya baadhi ya sheria za kimaumbo. Suala hili lilimsukuma Lakelo (2018) kueleza kuwa ukamilifu wa sheria za kimaumbo unategemea uwepo wa baadhi ya sheria za kisemantiki.

Tatu, kuna mfumo wa kimaumbo unaojikita katika kuchambua maumbo kwa lengo la kubaini mofu za jinsia badala ya kutumia sheria

za kimaana tu. Mfumo huu unajengeka katika fonolojia na mofolojia. Pia, ni mfumo ambao sheria za kifonolojia zinafanya kazi katika kiwango cha neno kama vile nomino kutofautishwa kutokana na kuwepo au kutokuwepo kwa sauti fulani au kutofautishwa kwa matamshi yake pamoja na majina mahususi ya jinsia. Sheria za kimofolojia zinahusu mawanda mapana zaidi kwa kuhusisha maana, fonolojia na mofolojia (Corbett, 1991).

Maumbo ya ngeli za majina yamekuwa yakitajwa kwa jina la jinsia na baadhi ya wachambuzi wa lugha, zikiwemo lugha za Kibantu (Corbett na Schadeberg, 2003b). Baadhi ya wachambuzi hutumia istilahi ya jinsia za kisarufi kurejelea dhana ya maumbo ya ngeli. Baadhi ya lugha zina maumbo mahsusi yanayodokeza juu ya dhana ya jinsia (Corbett, 1991 na Southerland na Katamba, 2011). Dhana za jinsia ya kibailojia na jinsia inayorejelea masuala ya kijamii zinaingiliana kimatumizi na kusababisha istilahi moja inapotumika kubeba baadhi ya sifa za istilahi nyingine (Litosseliti, 2006). Hata hivyo, jinsia inayofungamana na masuala ya kijamii inakuwa na uwanja mpana zaidi kimatumizi kuliko jinsia ya kibaiolojia.

Tafiti mbalimbali zilizofanyika kuhusu muundo wa nomino katika lugha za Kibantu zinaonesha kuwepo kwa umbo ngeli mwanzoni mwa shina la nomino (Maho, 1999; Schadeberg, 2003a; Katamba, 2003; Kusch-Lojenga, 2007; Hyman na wenzie, 2017 na Mark, 2019). Umbo ngeli linaweza kutokea peke yake au linaweza kutanguliwa na kiambishi awali tangulizi kwa baadhi ya lugha. Hata hivyo, kuna baadhi ya lugha za Kibantu zinazoruhusu maumbo mawili ya ngeli za majina kutokea katika nomino moja (Maho, 1999). Maumbo ngeli huitwa jinsia za kisarufi (Katamba na Stonham, 2006). Lugha ya Kimalila, kama ilivyo kwa lugha nyingine zikiwemo za Kibantu, haiwezi kujitenga na athari za jinsia katika lugha, pamoja na utumiaji wa maumbo ya ngeli katika nomino. Kisichojulikana hapa ni ikiwa, kuna maumbo yanayohusiana na dhana ya jinsia ya kibaiolojia katika nomino za Kimalila. Suala la utokeaji wa maumbo haya katika nomino linahitaji kuangaziwa pia. Kwa mantiki hii, makala hii inajikita katika

uchambuzi wa maumbo yanayotumika kubeba dhana ya jinsia katika lugha ya Kimalila nchini Tanzania.

Uhusiano Kati ya Lugha na Jinsia

Uhusiano kati ya lugha na jinsia ni suala lisiloepukika katika jamii. Southerland na Katamba (2011) wanauelezea uhusiano huu katika jamii kwa namna mbili. Uhusiano wa kwanza unahusu tofauti za kijinsia zinazotokea katika lugha ambazo zinasababishwa na namna jamii inavyofanya kazi. Hivyo, kuna shughuli zinazofanywa na wanawake na nyingine hufanywa na wanaume, jambo linalofanya tofauti hizi kujipambanua katika lugha (Eckert na McConnel-Ginet, 2003). Uhusiano wa pili unaeleza kwamba tofauti za utumiaji lugha kati ya mwanamke na mwanaume zinatokana na tabia ya lugha kuhusika kama njia muhimu ya kubeba mawazo yanayojenga na kuiendeleza jamii. Hii ina maana kwamba mambo yanayotokea katika lugha yanaakisi kinachotendeka katika jamii.

Kwa mujibu wa Eckert na McConnel-Ginet (2003) wanawake na wanaume wanatofautiana katika matumizi ya lugha kwa namna mbalimbali. Tofauti hizi, kama anavyofafanua Coates (2004), zinaathiriwa na mabadiliko yanayotokea katika jamii ambayo husababisha namna ya kutumia lugha kubadilika. Kwa kuwa lugha zinatofautiana kutokana na tofauti ya mazingira zinamotumika, ni rahisi tofauti hizi kujitokeza pia katika kuelezea masuala ya kijinsia kati ya lugha na lugha.

Methodolojia

Mbinu za mahojiano na ushuhudiaji zilitumika katika ukusanyaji wa data za msingi. Mbinu ya mahojiano ilihusisha watoataarifa watano wamilisi wa lugha ya Kimalila. Mbinu hii ilimakinikia katika kukusanya data kuhusu ujinsia unaojitokeza katika majina yanayotumika kutaja watu pamoja na mahusiano yao katika jamii. Aidha, mbinu ya ushuhudiaji ilitumika kuchunguza mazungumzo ya watumiaji wa lugha ya Kimalila katika mazingira mbalimbali. Lengo kuu lilikuwa kuchunguza, kubaini na kukusanya majina yanayotumika kuwataja watu yanavyoakisi masuala ya kijinsia, katika mahusiano

mbalimbali kwenye viwango vya familia, mtu na mtu hadi ukoo. Mtafiti, kwa kuwa ni mzawa na mmilisi wa lugha ya Kimalila, aliweza kung'amua kwa urahisi majina mbalimbali.

Maumbo Yanayobeba Dhana ya Jinsia katika Nomino

Sautherland na Katamba (2011) wanabainisha kuwa masuala ya lugha na jinsia yanaweza kusababisha tofauti katika utumizi wa lugha yakiathiriwa na: (i) Jinsia ya mzungumzaji au msikilizaji na (ii) Jinsia ya mtu anayezungumziwa. Dondoo hizi zina maana kwamba suala la utumizi wa lugha linaathiriwa na sifa za kijinsia za wahusika wanaotumia lugha. Lugha ya Kimalila ina tabia ya kuambisha maumbo maalumu katika majina yanayotaja watu na kuyapa maana tofauti na maana ya awali. Kitendo hiki kinachukuliwa kuwa ni unyambulishaji kwa kuwa jina jipya linapata maana mpya ambayo ni tofauti na iliyo katika jina la kwanza. Sehemu ifuatayo inajikita katika kuchambua utokeaji wa maumbo yanayohusiana na dhana ya jinsia katika lugha ya Kimalila.

Umbo {*na-*}

Mofu {na-} ikiambishwa katika majina yenye asili ya Kimalila, yanayotaja watu, inasababisha dhana ya jinsia kutokea katika neno unde. Jina jipya linalotokea linakuwa na maana ya mama mzazi wa mtu fulani. Hii ina maana kwamba umbo hili linatumika kuonesha uhusiano wa kiwima unaotokea kati ya mama na mtoto wake wa kike. Hata hivyo, inaonesha kuwa umbo hili linatumika kwa mtoto wa kumzaa tu kama inavyooneshwa katika data hii:

(1)*(a) Nt←←ta*"Ntuta" *Nant←←ta* "Mama Ntuta"
  (b) Y⚐sambi"Yisambi" *Nay⚐samb⚐* "Mama Yisambi"
  (c) Nsyani "Nsyani" *Nansyani* "Mama Nsyani"
  (d) *Sinde*"Sinde" *Nasinde* "Mama Sinde"
  (e) *Mb←sh⚐*"Mbushi" *Na⊒mb←sh⚐* "Mama Mbushi"

Aidha, inaonesha kwamba lugha ya Kimalila hairuhusu matumizi ya kinyambulishi {na-} katika kuunda majina yoyote ya watu. Mathalani, umbo hili halitumiki katika kuunda majina ya mkopo katika lugha ya

Kimalila. Hivyo, majina katika (2) hayatakubalika kwa kuwa ni mageni katika lugha ya Kimalila. Kwa mfano:

(2)(a) *Juma* "Juma"**Najuma*
  (b) *Hamisi* "Hamisi"**Nahamisi*
  (c) *Nehema* "Neema"**Naneema*
  (d) *Gelesi* "Grace"**Nagelesi*
  (e) *Peteli* "Petro"**Napeteli*
  (f) *Pa☝←lo* "Paulo"**Napa☝←lo*

Vilevile, kinominishi {na-} hakiruhusiwi kutumika kwa majina yanayorejelea koo za watu katika jamii ya Kimalila (3). Hii inatokana na uhusiano unaokuwepo kati ya mama na mtoto wa kike ambapo katika muktadha huu inaonesha kwamba mama hawezi kumiliki ukoo ambao ni dhana dhahania tofauti na ilivyo katika (1) ambapo kuna mtu dhahiri anayeweza kumilikiwa na mama. Chunguza mfano huu:

(3)(a) *Sote**Nasote
  (b) *-gwale**Nagwale
  (c) *-⟲gaga**Na⟲gaga
  (d) *-senga**Nasenga
  (e) *-pepu**Napepu
  (f) *-njoka**Nanjoka
  (g) *–☝eza**Na☝eza

Data yetu hapo juu ina maana kwamba umbo {na-} linatumika katika majina yenye asili ya Kimalila, lakini yasiyokuwa ya koo. Data inamaanisha kuwa, umbo {na-} linakusudiwa kutumika kwa mwanamke ambaye ana mtoto. Hata hivyo, jina lenye kinyambulishi {na-} linaweza kutumika kwa mtu ambaye hana mtoto, likiwa kama jina la urithi la bibi yake ambaye ana sifa ya msingi ya kuwa na mtoto, ingawa linaishia kutumika katika utani tu kwa vile linakosa mashiko.

Umbo {sa-}
Uchunguzi unaonesha kwamba umbo {sa-} linatumika katika majina kwa lengo la kubeba dhana ya jinsia ya kike katika lugha ya Kimalila kama inavyofafanuliwa katika sehemu ifuatayo:

Umbo {sa-} Linalorejelea Dhana ya Ukoo
Umbo {sa-} linaambishwa mwanzoni mwa majina yanayorejelea dhana ya koo katika jamii ya Kimalila na kusababisha majina yanayoundwa kubeba dhana ya mtu wa jinsia ya kike katika ukoo fulani. Tazama data hii:

      (4)(a) *-yↃgaga>*"SayↃgaga"
         (b) *-sote>*"Sasote"
         (b) *-gwale>*"Sagwale"
         (d) *-njoka>*"Sanjoka"
         (g) *-mpamba>*"Sampamba"
         (h) *-Senga>*"Sasenga"

Katika muktadha huu (4) inaonesha kwamba umbo {sa-} linaambishwa mwanzoni mwa majina yanayohusiana na koo kwa kuwa majina yote katika data yanarejelea koo. Maelezo haya yana maana kwamba kinyambulishi {sa-} hakitumiki katika majina mengine ya watu yasiyohusiana na koo kama ilivyobainishwa katika (5):

      (5)(a) *Yisambi**sa-yisambi "Yisambi"
         (b) *Nt←←ta**Sa-nt←←ta "Ntuta"
         (c) *Shiizya**Sa-shizya "Shizya"
         (d) *Mwinga**sa-mwinga "Mwinga"
         (e) *Sinde**sa-sinde "Sinde"
         (f) *Yilosi**sa-yilosi "Yilosi"

Data yetu hapo juu ina maana kwamba majina ya koo yanapomrejelea mtu wa jinsia ya kike hutumia umbo {sa-}, lakini majina yasiyokuwa ya koo hayapokei umbo hili. Inawezekana hali hii inatokana na kuwepo kwa majina ya watu ambayo ni mahsusi kwa watu wa jinsia ya kike au kiume kama vile jina *Mwinga* (5d) linarejea jinsia ya kike. Hivyo,

kutumia umbo {sa} itakuwa ni sawa na kurudia dhana ya jinsia mara mbili katika jina moja jambo ambalo litakuwa ni kinyume na dhana ya uwekevu katika matumizi ya lugha.

Umbo {sa-} Linalomrejelea Baba Mkwe
Lugha ya Kimalila inatumia umbo {sa-} kurejelea dhana ya jinsia. Katika data hiyo, neno linaloundwa linakuwa na maana ya baba mkwe au ndugu wa kiume wa mume wa mwanamke. Hivyo, matumizi ya umbo hili yanategemea kukamilika kwa tukio la ndoa. Ndugu wa kiume anayezungumziwa hapa lazima awe na uhusiano wa kiulalo wa ukaka au ubinamu na baba mkwe. Umbo hili halizalishi nomino inayomrejelea mwanamke kama ilivyoshuhudiwa katika (4), bali hubeba dhana ya mahusiano zaidi. Kwa mfano:

> (6) *Savwala* "Baba mkwe au mzazi wa kiume (baba) wa mume fulani".

Jambo la kuvutia ni kuwa jina hili (6) linatumika kwa masharti maalumu. Uchunguzi unaonesha kuwa mwanamke hawezi kumtaja baba wa mume wake kwa kutumia jina *savwala*, badala yake atatumia jina la *tayivwala* lenye maana ya mzazi au ndugu wa kiume (baba) wa mume kama ilivyofafanuliwa katika (10). Jina *savwala* hutumiwa na watu wengine katika kumtaja mzazi wa kiume wa mume wa mtu mwingine. Kwa mfano, ←*savwala wa Nsanya* "Baba mzazi au ndugu wa kiume (kaka au binamu) wa mume wa Nsanya". Katika muktadha huu, *Nsanya* hazuiwi kutumia jina *savwala* kumtaja baba mkwe wake. Hata hivyo, kipragmatiki haikubaliki kwa wazungumzaji wa lugha ya Kimalila. Wingi wa neno *savwala* utakuwa *a🖋asavwala* "Akina baba mkwe". Kimuundo, inaonesha kwamba mofu {sa-} hubeba dhana ya jinsia pamoja na idadi ya umoja; inapokuwa katika wingi hutokea pamoja na mofu ya ngeli ya 2 {🖋a-} inayobeba dhima ya wingi.

Umbo {mwa-}
Lugha ya Kimalila inatumia umbo {mwa-} katika majina yanayorejelea koo na kuunda nomino mpya, ikiwa na maana mtu wa kiume wa ukoo fulani. Mofu hii hutumika kubeba dhana ya mtu wa jinsia ya kiume

katika jamii ya Kimalila kwa kuwa wazungumzaji hutumia kumtaja mwanaume tu na sio kinyume chake. Chunguza data inayofuata:

(7) (a) - *Ɂgaga>Mwa-yƁgaga* Mwaigaga
(b) –*sile>Mwa-sile* Mwasile
(c) –*mbwiga>Mwa-mbwiga* Mwambwiga
(d) -*senga>Mwa-senga* Mwasenga
(e) -*pepu>Mwa-pepu* Mwapepu
(f) -*mpamba>Mwa-mpamba* Mwampamba
(g) - *ɓeza>Mwa- ɓeza* Mwabheza
(h) -*sote>Mwa-sote* Mwasote
(i) -*nsiha>Mwa-nsiha* Mwansiha

Hata hivyo, inaonesha kwamba katika mazingira yaliyo rasmi kama maeneo yanayohitaji kuhifadhi kumbukumbu katika maandishi jina lenye umbo {mwa-} hutumika kwa jinsia ya kike pia. Ndiyo kusema kwamba jina lenye kupokea mofu {mwa-} linatumika katika mazingira ya namna mbili. Kwanza, wazawa wa lugha ya Kimalila wanapowasiliana hutumia mofu {mwa-} kumrejelea mwanaume tu. Pili, mofu {mwa-} inatumika kumrejelea mtu wa jinsia ya kike au kiume katika mazingira yasiyohusisha wazawa wa lugha ya Kimalila. Hii ina maana kwamba wazawa wa lugha ya Kimalila ndiyo wanaoweza kuzibaini tofauti za matumizi ya umbo hili. Wageni wanachanganya dhima za mofu {mwa-}. Wingi wa jina linalopokea umbo {mwa-} unaanza na umbo la ngeli ya pili {ɓa-}, ambapo {mwa-} linabaki katika nafasi yake ya kuwa jirani na shina. Data katika (7b-c) itakuwa *a ɓamwasile* na *a ɓamwambwiga* kwa maana ya "wa ukoo wa Mwasile na Mwambwiga".

Umbo {*Samwa-*}
Lugha ya Kimalila inatumia pia maumbo mawili ya {sa-} na {mwa-} kuunda umbo moja la {samwa-} jina linaloundwa kwa kuambishwa umbo hili {samwa-} linakuwa na maana mtu wa kike katika ukoo fulani kama ilivyooneshwa katika sehemu hii:

(8) *(a) -ndeleSamwa-ndele* "Samwandele"

(b) -sile   Samwa-sile "Samwasile"
(c) -l←☝andaSamwa-l←☝anda"Samwal←☝anda"
(d) -nsihaSamwa-nsiha "Samwansiha".

Data inaonesha kwamba mofu {samwa-} inatumika kutaja mtu wa jinsia ya kike katika ukoo kama ilivyojadiliwa katika (4). Lugha ya Kimalila inatumia umbo {sa-} peke yake, pamoja na umbo {samwa-} kumrejelea mwanamke katika ukoo. Hata hivyo, uchunguzi unaonesha kuwa, umbo {samwa-} halitumiki katika koo zote. Inawezekana jambo linaloonesha kuwa uteuzi wa matumizi ya {sa-} au {samwa-} yanafungamana na sababu za kipragmatiki zaidi katika jamiilugha ya Kimalila. Baadhi ya koo huambisha mofu {sa-} mwanzoni mwa umbo {mwa-} ambapo, katika muktadha huu, wazungumzaji wanachukulia kuwa jina linaloanza na {mwa-} ni jina huru la ukoo linalojitegemea kama ilivyo katika ukoo.

Hata hivyo, mpangilio wa {mwasa-} haukubaliki katika lugha ya Kimalila. Huenda kutokubalika kunatokana na wazungumzaji kuchukulia kuwa {mwa-} ni sehemu ya jina lililokamilika katika ukoo kuliko {sa-} kupewa hadhi hiyo kutokana na sababu za kipragmatiki. Kwa mantiki hii, mtu anaweza kumzaa mtoto ambaye katika mazingira mengine anaweza kuitwa kwa jina linaloanza na umbo {mwa-}, lakini hawezi kumzaa mtoto ambaye ana jina linaloanza na umbo {sa-} kwa sababu jina linaloanza na {sa-} hutumika kwa mtu mzima mwenye mtoto. Kwa mfano, mtu akiulizwa umejifungua mtoto wa jinsia gani? Atajibu *Sampamba,* akiwa na maana ya mtoto wa kike wa ukoo wa -*mpamba*. Hata hivyo, hataweza kujibu *Mwasampamba* kwa maana ya jinsia ya kiume kwa kuwa jina hili halikubaliki.

Katika mazingira mengine, {samwa-} hutumika kwa majina ya kawaida yasiyokuwa ya ukoo, lakini yenye asili ya Kimalila kama inavyobainishwa katika data ifuatayo:

(9) Shina Jina unde Maana
(a) *ShiilaSamwa-shiila* "Samwashila"
(b) *M⤢⤢taSamwa-m⤢⤢ta* "Samwamita"

    (c) *JaangaSamwa-janga* "Samwajanga"
    (d) *SheengoSamwa-sheengo* "Samwashengo"
    (e) *lwiijiSamwa-lwiji* "Samwalwiji"

Umbo {sa-} linatokea kwanza, kisha kufuatwa na umbo {mwa-}, lakini sio kinyume chake. Umbo {*samwa-*} linafuatwa na jina la kawaida au kufuatwa na {mwa-} inayotokea mwanzoni mwa jina la kawaida tofauti na la ukoo (9). Katika mazingira haya, mofu {sa-} inaendelea kubaki na dhana ya jinsia ya kike. Katika (9a) jina lilibainika kutumika kwa mwanaume. Inawezekana (9a) ni jina kamili badala ya kudai kuwa linaweza kutenganishwa ili kupata *Sa-mwashiila*.

Kwa ufupi, tunaweza kusema lugha ya Kimalila inatumia mofu { na-}, {samwa-} na {sa-} kurejelea dhana ya jinsia ya kike, ilihali mofu {mwa-} na {sa-} hutumika kurejelea jinsia ya kiume. Maumbo haya hutumika katika mazingira maalumu ambayo ni ya mahusiano ya kipragmatiki jambo linalohitaji uelewa mpana wa lugha na utamaduni wa Kimalila katika kuyapambanua.

Jinsia katika Shina {-vwala}
Baadhi ya watu wanapewa hadhi tofauti kutegemeana na matumizi ya lugha pamoja na shughuli wanazozifanya katika jamii. Baadhi ya mofu zinazoongezwa katika mashina zina tabia ya kubeba dhana ya jinsia katika baadhi ya lugha (Han, 2014). Uchunguzi unaonesha kwamba neno *vwala* linatumika kama shina katika lugha ya Kimalila, ingawa halina maana yoyote. Hata hivyo, neno linaloundwa kutokana na uambishaji katika neno hili {-*vwala*} linapata maana mbalimbali kutegemeana na maumbo yanayoambishwa mwanzoni mwake. Sehemu hii inachambua maumbo mbalimbali yanayoambishwa mwanzoni mwa shina (-*vwala*). Hivyo, linaweza kuitwa jina tegemezi au funge kwa kuwa ukamilifu wake kimaana hutegemea uwepo wa viambishi vingine.

Umbo {mayi-}
Lugha ya Kimalila inatumia neno *mayi* kwa maana ya mama. Hata hivyo, umbo hili linapoambishwa mwanzoni mwa neno *vwala*

linasababisha neno *mayivwala* (9) kutokea likiwa na maana ya mama mkwe. Ndiyo kusema kwamba umbo *mayi* linabeba dhana ya jinsia ya kike katika muktadha huu na kufanya jina *mayivwala* kuwa na maana inayohusiana na mwanamke kama ilivyobainishwa katika data (9):

(9) *May ̑vwala* "Mama mkwe"

Neno *mayivwala* linaweza kutumika na mwanaume anapomtaja mama mzazi wa mke wake. Vilevile, mwanaume anaweza kumwita mke wa mtoto wake kwa jina la *mayivwala*.

Umbo {tay ̑-}
Uchunguzi unaonesha kwamba mofu {*tay ̑-*} inabeba dhima ya jinsia ya kiume linapoambishwa mwanzoni mwa neno *vwala*. Hivyo, husababisha neno *tayivwala* kutokea likiwa na maana ya mkwe wa kiume. Jina *tay ̑vwala* (10) linaweza kutumika kwa pande zote, Baba mkwe na baba mkwe anaweza kumwita mtu aliyemuoa mtoto wake *tayivwala*. Hata hivyo, baba mkwe hupendelea zaidi kutumia jina la *m←kolima* kwa lengo la kumtaja mtoto aliyemuoa mtoto wake. Hakuna sababu za msingi zinazosababisha neno *m←kolima* kutumiwa na baba mkwe badaya ya *tayivwala.* Tazama data hii:

(10) *-vwala tay ̑-vwaala* "Mkwe wa kiume"

Jina *tayivwala* liko katika umoja, wingi wake utakuwa *a ̑atayivwala*. Katika muktadha huu, mofu {*tayi-*} inabeba dhima ya idadi ya umoja.

Umbo {nya-}
Umbo {nya-} hutumika katika lugha ya Kimalila kubeba dhima ya kudokeza juu ya jinsia ya kike linapoambishwa katika neno *vwala*. Umbo {*nya-*} likiambishwa mwanzoni mwa neno *vwala* husababisha jina *nyavwala* "Mama mkwe" (11) kutokea. Hata hivyo, mtu hawezi kumwita mama mzazi wa mke wake kwa jina la *nyavwala*. Katika muktadha huu, atalazimika kulitumia anapomtaja mama mkwe kwa mtu au watu wengine. Vilevile, watu wengine wanaweza kulitumia kwa kumtaja mama mkwe kwa watu wengine kama ilivyodokezwa katika daa hii:

(11) (a) *unyavwala wakwe* "Mama mkwe wake"
　　 (b) *unyavwaala wani* "Mama mkwe wangu".

Pia, umbo {nya-} linaweza kuambishwa mwanzoni mwa neno *seenje* "shangazi" na kusababisha jina *nyasenje* lenye maana ya shangazi wa mtu fulani kupatikana. Kama ilivyo kwa *nyavwala*, mtu hawezi kumwita shangazi yake *nyasenje*, bali atamwita seenje "Shangazi". Atatumia *nyasenje* "Shangazi" ikiwa atakuwa anamtaja kwa watu wengine. Katika mazingira mengine, watu wengine wanaweza kulitumia wanapomrejelea shangazi wa mtu fulani. Kwa mfano:
(12)(a) ←*nyasenje wan* ⎰"Shangazi yangu"
(b) ←*nyasenje wakwe*"Shangazi yake".

Data yetu hapo juu inaonesha kwamba umbo {*nya-*} linadokeza juu ya jinsia ya kike kwa kuwa hakuna data zinazoonesha kuwa linaweza kutumika kumrejelea mwanaume. Wingi wa nyasenje unakuwa *a⌇anyasenje* "Akina shangazi" ambapo unachukua umbo la ngeli katika ngeli ya 2. Umbo {nya-} katika muktadha huu, bado linadhihirisha kuwa mtajwa (shangazi) ni mtu wa jinsia ya kike.

Maumbo Yanayohusu Mahusiano ya Watu
Sehemu iliyotangulia ilijikita zaidi katika uchambuzi wa maumbo yanayohusu jinsia katika majina ya Kimalila. Sehemu zifuatazo zinajikita katika uchambuzi wa maumbo yanayopatikana katika majina ya Kimalila yanayojikita katika mahusiano ya watu kwa ujumla. Hivyo, suala la jinsia halijawa wazi kama lilivyoangaziwa hapo awali.

Umbo {mwana-}
Neno {mwana-} katika lugha ya Kimalila linatumika kwa namna mbili. Kwanza, likiwa na maana ya watoto wa ndugu mmoja. Pili, likiwa na maana ya wa ukoo fulani kama inavyofafanuliwa katika sehemu zifuatazo:

Umbo {mwana-} lenye Maana ya Watoto wa Mtu Moja
Neno *mwana* katika lugha nyingi za Kibantu hutumika likiwa na maana ya mtoto. Hata hivyo, umbo hili linapoambishwa mwanzoni mwa

baadhi ya maneno katika lugha ya Kimalila linafanya neno jipya linaloundwa kuwa na maana ya watoto wa mtu fulani. Data katika (12) inaonesha kwamba maneno yanayobeba dhana za baba au mama ndiyo yanayoweza kupokea umbo hili katika mazingira mengine. Chunguza mfano huu:

(12) (a) *yise*"baba"*mwana + yise*"wa baba mmoja"
(b) *may*⟩"mama"*mwana+may*⟩"wa mama mmoja"
(c) *nyina*"mama"*mwana+nyina*"wa mama mmoja"

Data hii inaonesha kwamba mtu hutumia maneno *mwanayise*, *mwanamayi* na *mwananyina* kuonesha uhusiano wake na mtajwa katika umoja. Hata hivyo, katika wingi, umbo {*mwana-*} linakuwa {ɓ*ana-*}. Hii ina maana kwamba umbo la ngeli 1 la {*mw-*} hutumika katika umoja na la ngeli ya 2 {ɓ*a-*} hutumika katika wingi kama ilivyo katika lugha nyingine za Kibantu. Suala la ujinsia halijipambanui katika umbo {mwana-}, bali linaamriwa na nomino zenye kutaja mtu wa jinsia fulani za *yise* "Baba" na *mayi* au *nyina* zenye maana ya mama ambazo zinaambatanishwa mbele yake. Hii ni tofauti na ilivyofafanuliwa awali ambapo kulikuwa na mofu mahsusi iliyohusiana na dhana ya jinsia inayohusika.

Umbo {*mwana-*} Lenye Maana ya Mtu wa Ukoo Fulani
Katika baadhi ya mazingira, umbo {*mwana-*} katika lugha ya Kimalila linaambishwa mwanzoni mwa mashina ya majina ya ukoo na kusababisha majina mapya kuwa na maana ya mtu wa ukoo fulani. Tazama data ifuatayo:

(13) (a) *Mwana-gwale* "wa ukoo wa Mwagwale"
(b) *Mwana-kwamu* "wa ukoo wa Nkwamu"
(c) *Mwana-senga* "wa ukoo wa Mwasenga"
(d) *Mwana-ntepele* "wa ukoo wa Mwantepele"

Ikiwa wanaolengwa watakuwa wengi, umbo {ɓana-} hutumika. Hivyo, katika (13) kutakuwa na majina ɓ*anagwale*, ɓ*anankwamu*, ɓ*anasenga na* ɓ*anantepele*. Umbo {mwana/ɓana-} linapotumika, msisitizo unakuwa kwenye ukoo tofauti na {mwa-} tuliyoijadili katika

(7) ambapo msisitizo unakuwa kwa mtu binafsi. Umbo *{mwana-}* linatumika kumrejelea mwanamke na mwanaume kwa kuwa lina maana ya anayetoka au wa ukoo fulani.

Katika mazingira mengine, umbo hili linaweza kusikika katika matamshi kama {mwana-} likiwa limeambishwa katika majina ya kawaida yasiyokuwa ya ukoo. Kimsingi, jina linalodaiwa kuambishwa umbo {*mwana-*} likichunguzwa vyema inaonesha kwamba linakuwa umbo {mwa-} lililoambishwa mwanzoni mwa jina linaloanza na umbo {na-} ambalo limejadiliwa katika (1). Chunguza data hii:

> (14) (a) *Sinde* "Yisambi" *mwa Nasinde* "mwa Mama Sinde"
> (b) *Yisega* "Yisega"*mwa Nayisega"* "mwa Mama Yisega"
> (c) *Shaali* "Shali"*mwa Nashali* "mwa Mama Shaali"

Data hiyo hapo juu ina maana kwamba umbo {*mwana-*} linahitaji umakini mkubwa katika kulibaini maana yake kwa kuwa linapoambishwa kwenye jina linakuwa na matamshi yanayoelekeana na maumbo {mwa-na-} ambapo kuna maumbo mawili tofauti. Pia, inaonesha kwamba umbo {mwana-} linatumika katika sambamba na majina ya koo au kama ilivyofafanuliwa katika (12).

Umbo {lya-}
Umbo {lya-} linatumika kuunda majina mapya yanayofungamana na mahusiano ya watu katika lugha ya Kimalila. Baadhi ya majina huambishwa umbo hili mwanzoni mwa jina na kuibua maana mbalimbali kutegemeana na maana ya neno lililoambishwa. Hivyo, umbo hili linapotumika hulifanya jina unde kuwa na maana ya watu wanaunganishwa na jambo au tukio fulani. Mathalani, jina *maayi* (15a) lina maana mama, watu wanaotoka mama mmoja wataitana *lyamaayi* "Watoto wa mama mmoja au dada wa mama":

> (15) (a) *maay⃗* "mama"lya-*maay⃗*/ "wa mama mmoja"
> (b) *ngugu*"njiwa"*lya-ngugu* "marafiki/wanandoa"
> (c) *ntosa*"mtwasi"*lya-ntosa* "waliooa pamoja"
> (d) *mpalala*"mkuki"*lya-mpalala* "marafiki wa kiume".

Aidha, katika (15b) neno *ngugu* lina maana njiwa, yaani, marafiki wawili wanaopendana sana, hasa wanandoa, huitana *lyangungu*. Hii ina maana kwamba maana ya umbo {lya-} huathiriwa zaidi na maana ya shina la neno. Hivyo, maana yake haitabiriki, hasa inapotokea maana ya shina la neno kuwa ya kisitiari.

Majina yaliyojadiliwa katika makala hii yanapokea ngeli ya pili ya majina, lakini kwa sharti la maumbo haya kutokea jirani zaidi na shina la jina. Hivyo, umbo ngeli haliwezi kutokea katikati ya shina na maumbo yaliyojadiliwa. Vilevile, nomino yenye kupokea maumbo ya jinsia inapokuwa katika umoja hairuhusu maumbo mawili kutokea, ingawa katika wingi kunakuwa na maumbo yote mawili; la ngeli na la jinsia linalotokea jirani zaidi na shina.

Mchango na Mapendekezo
Makala hii imeweka wazi ujitokezaji wa jinsia katika maumbo yanayopatikana kwenye majina ya watu katika lugha ya Kimalila. Makala imeenda mbali zaidi kwa kuonesha kuwa kuna maumbo mahususi yanayobeba dhana zinazohusiana na jinsia katika majina ya Kibantu. Hata hivyo, bado tafiti zaidi zinahitajika katika majina haya katika lugha nyingine za Kibantu. Vilevile tafiti zinaweza kufanyika katika aina nyingine za majina kuhusiana na masuala ya jinsia katika lugha ya Kimalila na lugha za Kibantu kwa ujumla.

Hitimisho
Katika makala hii tumeonesha kwamba maumbo {mwa-}, {sa-} na {tayi-} yanatumika kutambulisha jinsia ya kiume katika lugha ya Kimalila. Kwa upande mwingine, mofu {na-}, {sa-}, {mayi-}, {nya-} na {Samwa-} yanabeba dhana ya jinsia ya kike. Mofu {samwa-} inatokana na muunganiko wa mofu {sa-} na {mwa-}. Hata hivyo, imeonesha kuwa muunganiko huu hauwezi kufanyika kinyume chake na kuwa {*mwasa-*}. Kimpangilio, nomino ikiwa katika umoja haipokei mofu nyingine ya umoja kwa kuwa mofu hizi za jinsia zinabeba dhima ya idadi ya umoja. Nomino inapokuwa katika wingi, mofu hizi hutokea pamoja na mofu ya wingi.

Pia, imebainishwa kuwa maumbo yanayobeba dhana ya jinsia katika lugha ya Kimalila yanatumika kwa majina yenye asili ya Kimalila. Majina ya kigeni hayapokei maumbo haya. Inawezekana majina ya kigeni, bado hayajafikia hatua ya kupokea mofu za Kimalila ili yaendane na kanuni za mofolojia ya Kimalila. Makala imeonesha kwamba kuna uhusiano mkubwa kati ya maumbo ya jinsia ya kibailojia na jinsia ya kijamii ambapo majina yanaonesha mahusiano ya watu katika jamii. Matokeo haya yanaibua haja ya tafiti zaidi kuhusu dhana ya jinsia ya kibailojia katika maumbo yanayopatikana kwenye majina ya lugha za Kibantu, hasa ikizingatiwa kuwa tafiti zilizopo zinatumia istilahi ya jinsia kama sinonimu ya ngeli za majina.

Marejeleo

Coates, J. (2004). *Women, Men and Language: A Sociolinguistic Account of Gender Differences in Language* (Toleo la 3). London: Routledge.

Corbett, G. (1991). *Gender*. Cambridge: Cambridge University Press.

Eckert, P., & McConnel-Ginet, S. (2003). *Language and Gender*. Cambridge: Cambridge University Press.

Guthrie, M. (1967). *A Comparative Bantu: An Introduction to Comparative Linguistics Prehistory of the Bantu Languages*, Juzuu 4. Farnborough: Greggy Press.

Han, N. V. (2014). 'The Relationship Between Language and Gender: A Case Study in Vietnamese'. *Global Journal of Interdisciplinary Social Sciences*. Juzuu la 3 (3). 96 -99.

Jakiela, P., & Ozier, O. (2019). 'Gendered Language'. Center for Global Development. Working Paper 500.

Katamba, F. (2003). 'Bantu Nominal Morphology' katika Nurse, D. & G. Philippson (Wah.). *The Bantu Languages*. London: Routledge.

Katamba, F., & Stonham, J. (2006). *Modern Linguistics Morphology* . New York: Palgrave MacMillan.

Kutsch-Lojenga, C. (2007). 'Minimality and Morae in Malila (M24)', Katika *Selected Proceedings* of 37th "Annual Conference on African Linguistics, Imehaririwa na Pyne, D. L., & Pena, kur 77 - 87.

Lakelo, O. (2018). 'What is Difficult About Grammatical Gender? Evidence from Heritage'. Katika *Russian Journal of Language Contact 11*. 233 - 267.

Litosseliti, L. (2006). *Gender and Language: Theory and Practice*. New York: Loutledge Taylor and Fracis Group.

Maho, J. (1999). *A Comparative Study of Bantu Noun Classes*. Tasinifu ya Uzamivu. Universty of Guartenberg.

Mastropavlou, M., & Tsimpli, M. (2011). 'The Role of Suffixes in Grammatical Gender Assignment in Modern Greek: A Psychological Study'. Katika *Journal of Greek Linguistics*. 27 - 55.

Schadeberg, T. C. (2003a). *The Bantu Languages*. London: Routledge.

Southerland, H. S., & Katamba, F. (2011). *Contemprary Linguistics*. London: Person Education Limited.

Van de Velde, M. (2019). 'Nominal Morphology and Syntax'. *The Bantu Languages* (Toleo la 2), Routledge, kur.237-269.

Yule, G. (2006). *The Study of Languages*. Cambridge: Cambridge University Press.

Noel Julius Ntawigaya
Department of Education, Teofilo Kisanji University
Email: *noeljulius9@gmail.com*

Watson Lupogo Masiba is an assistant lecturer in Educational Psychology at a defunct Tumaini University Makumira Mbeya Centre and a minister of the Evangelical Lutheran Church in Tanzania of the Konde Diocese. His book is about an investigation on the impact of watching violent television programs on the behavior of secondary school children in Tanzania.

In chapter one, the author introduced the theme of his book. It is this chapter where he discussed the context of his study at global level, continental level and country wise. In this context, he strongly put the background of the problem of violence on the TV programs. The author had shown a deep survey on various researches and scholars' arguments. Through his survey, it has been confirmed that the problem is greater. Indeed, this deep survey in research is worthy commendable.

As regards to the nature of the study significance, it is obvious that the government as the law enforcer and the central authority of policy making process was supposed to be recognized among beneficiaries. However, it seems that the author has ignored the government as one of beneficiaries as he writes the group of beneficiaries. He has only recognized media owners and parents as the main responsible stakeholders in structuring appropriate TV programs. It is my opinion that, media owners and parents themselves as the main stakeholders as put by the author, they cannot be able to prevent violent television programs on secondary school children in Tanzania without government's effort. Hence, for the government being one of the beneficiaries is imperative.

The author suggested theories used to guide his study which had a link with the study focus. He used Social learning theory as suggested by Albert Bandura 1971: 46 in his book "*Psychological Modeling: Conflicting Theories*". This theory explicates that, people constantly learn by observing and imitating the behaviours of social environmental models whether they are good or bad but they are determined by the occurrences on which they are rewarded, unnoticed, and punished (Pg. 11). With reference to this theory, he maintained that, in a normal circumstance, it is obvious that, children are likely to imitate violent behaviours of social environmental models. He therefore contends that, in this case, secondary school children can also imitate violent behaviours of social media models and then replicate into their real world provided that they are not ignored and punished (Pg. 12).

On the other hand, the author clearly articulated cultivation theory in George Rodman's book (2008: 53) "*Mass Media in a Changing World: History Industry Controversy*" that, "the more time people spend living in the television world, the more likely they are to believe social reality portrayed on TV". The author linked this theory with his study when he said that, this theory reveals that, people who watch television and other media most of their time in their life their way of thinking and understanding the real world becomes altered. He therefore concluded that, cultivation theory intended to elucidate that watching of violent TV programs extensively might alter the attitudes and behaviours of the viewers who then can equate the world of TV to the real world (Pg. 15). This concluding remark is inspiring.

Chapter two; in this chapter, the author dealt with television violence watching and related literatures. The survey of related literatures done by the author is stirring since it has covered the study objectives. He has been able to synthesize the knowledge gap especially when he said that "western findings cannot be generalized because of different operational context, social-cultural, economic factors, and the historical background" (Pg. 46). This reason is commendable because it is true that most literatures relating to his subject matter come from western countries and less from African countries including Tanzania.

Chapter three; the author has been able to present his study methodological perspectives where he successfully presented and explained the methods used in carrying out his study. He strappingly discussed his study research approach and design which is acknowledgeable. In describing the area of his study, he has strongly given the reasons of selecting the study area. However, he has not given the reasons convinced him to select secondary school students and not primary school pupils or any other level of education while watching violent TV programs today is liked by most children regardless the level of education.

In discussing the study target population, the author contradicts the readers on what was exactly the study population. This contradiction comes in page 19 where he said; " The informants of this study were form two to form four pupils in the co-education day schools....", and in page 52 where he said; " So, the target population of this study involves all students in form one to four...". This contradiction makes the readers of this book to remain in dilemma on what was the real target population of his study. However, as I read his discussion about sample and sampling procedures, methods of data collection, validity and reliability of the instruments and data analysis, I see that it is delightful.

Whilst talking about study ethical consideration, the author said, "The research clearance permit was obtained from Vice Chancellor (VC) of the Tumaini University Makumira" (Pg. 66). It is true that, by looking on research clearance permit, it obviously shows that, the author was doing his research under Tumaini University Makumira. Nonetheless, this contradicts with what he said in the acknowledgement part (xv) that; "This book is a revised version of research report for my masters degree in Applied Social Psychology of the University of Dar es Salaam". With this statement, it is my expectation that, the research clearance permit could be that one provided by the University of Dar es Salaam. It is something confusing to see Tumaini University Makumira giving to him such permit to the study that has done under different University. This is blurred. Thus, with this contradiction, it makes readers to doubt on the ethical consideration of the study.

Chapter four; this chapter is about hearing research data which is concerned with the presentation and discussion of the findings as regards to the study questions. Since his study was a mixed research study, demographic information of respondents could be shown; however, the author did not do so. The author managed to ask children to identify types of TV programs and the violent acts they used to watch (Pg.72) but he did not manage to ask them to identify non-violent TV programs, rather this question was asked to their parents (Pg.94). Leaving this question unimportant to children, shows that, he did not measure the children's level of understanding non- violent TV programs. Hence, it could be difficult to emphasize self-control because we do not know if they themselves able to differentiate the type of TV programs being either violent or non-violent ones to affect their discipline and then academic performance.

The author found that, most secondary school students spend a lot of time especially on weekends watching various violent TV programs. These include; movies, music, drama and other information from other programs which identified to be among of the most violent ones when they are in their homes. As regards to his results, spending a lot of time watching violent TV programs instead of concentrating on studying activities, greatly caused their poor academic performance and discipline as well.

In this chapter the author strongly managed to represent and analyse his study findings in a recommendable way. However, the way he used to discuss his study findings is not convincing. It due to the reason that, he has lightly argued against his findings, instead, he strongly used to compare his findings with other research findings as done in other places which is not only enough when discussing research findings. The recommended way of discussing findings is either by agreeing or disagreeing the findings with reasons that are supported by evidences from scholars, researcher's experience or real data (observation) from the field.

In chapter five, the author has strongly presented the summary of the study, summary of the major findings as well as the conclusion of the study reached basing on the findings of the study. He also presented both recommendations for actions and for further research as regards to the findings of the study. Indeed, what has been done in this chapter is highly recommendable.

Therefore, as far as author's book has some weaknesses as I have observed, it has got much strengths which overlap those noted weaknesses. His book is important due to the reason that, it discusses the important role of parents and guardians to discourage and prohibit children from watching violent TV programs and hence encourage watching non- violent TV programs.   Hence, it is my recommendation that, this book is essential and advised to be read by all educational stakeholders especially in this era whereby ICT is getting more advanced and that a TV has become an interesting device affecting large population especially school children.

NOTE TO CONTRIBUTORS

1. Only Materials that have never been published or submitted for publication elsewhere will be considered. All submitted papers will be critically peer reviewed by at least two anonymous reviewers who will be looking for originality, relevance, clarity, appropriateness of the methods, validity of the data, reasonability of the conclusions and support from the data.

2. An abstract of 150 - 200 words should accompany the article.

3. The manuscript should have: a title page of the paper, the names, institutional affiliation, Postal address, phone number and Email address of the author(s). If a paper has more than one author, indicate the corresponding author. The entire manuscript must be typed in 1.5 space except for Abstract which should be in 1.0 space non italic font. The font size of the main text shall be 12 point Times New Roman. All pages must be numbered.

4. Research theoretical paper should be between 5,000 and 7,000 words in length. Reviews and short communication should not exceed 2000 words. The word count of the manuscript should include, abstract, references, tables and figures.

5. Digital references should follow the latest style of American Psychological Association. Manual references will not be accepted.

6. All quotation should be italicized, indented and put in a single space.

7. Manuscripts that are written in clear and grammatical English or Kiswahili should be submitted in soft copy to:

Editors -in –Chief
Ruaha Journal of Arts and Social Sciences
Ruaha Catholic University
P. O. BOX 774,
IRINGA.
TANZANIA.
Email: rujass@rucu.ac.tz